# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

## RIPOTI YA MAPITIO WA SHERIA

## YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR

## NAMBA 01 YA MWAKA 2012

## NAMBA 3/2022

**INAWASILISHWA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**

**JANUARI, 2022**

**MHESHIMIWA HAROUN ALI SULEIMAN,**

**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS- KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA,**
**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA DKT. MWINYI TALIB HAJI,**
**MWANASHERIA MKUU WA ZANZIBAR,**
**ZANZIBAR.**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya Mwaka 1986, kwa heshima, Tume inawasilisha Ripoti ya Mapitio ya Sheria yaKuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar Nam. 1 ya mwaka 2012.

**……………………….**

**KHADIJA SHAMTE MZEE**
**MWENYEKITI,**
**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA,**
**ZANZIBAR**

**28 JANUARI, 2022.**

**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR**



**MHE. KHADIJA SHAMTE MZEE**
**MWENYEKITI**



**BW MUSSA KOMBO BAKARI**
**KATIBU**

**MWENYEKITI**

| | |
|---|---|
| Mhe. Khadija Shamte Mzee | Mwenyekiti |

**WATAFITI**

| | |
|---|---|
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu wa Tume |
| Dr. Mahfoudha Masoud Ali | Mtafiti wa Sheria |
| Nd. Yakuob Rajab Juma | Mtafiti wa Sheria |


Tume ya Kurekebisha Sheria

Vuga, Zanzibar-

P.O BOX 2539,

Simu +255 24 2231143,

Nukushi +255 24 2231137,

barua pepe info@lrcz.go.tz.

tovutiwww.lrcz.go.tz

## VIFUNGU VYA UTANGULIZI

**Rejea……………………………………………………………………………………………...vi**

**Shukrani…………………………………………………………………………………….xv**

**Vifupisho vya Maneno……………………………………………………………………...xvi**

**Muhtasari…………………………………………………………………………………..xvii**

**SURA YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**……………………………………………………………………………...1

1.1 **Nadharia ya Rushwa na Uhujumu Uchumi**……………………………………………...1

1.2 Mamlaka ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar.......................................................................1

1.3 Lengo la Utafiti………………………………………………………………………………2

1.4 Tamko la tatizo la Utafiti……………………………………………………………………...3

1.5 Umuhimu wa Utafiti…………………………………………………………………………3

1.6 Historia ya Rushwa na Uhujumu Uchumi…………………………………………………...3

1.7 Historia ya mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar………………...7

1.8 Historia kwa upande wa Tanzania Bara……………………………………………………..8

1.9 Chimbuko la Utafiti…………………………………………………………………………...9

1.10 Njia zilizotumika katika Utafiti……………………………………………………………...9

1.11 Hadidu Rejea………………………………………………………………………………....10

1.12 Ukomo wa Utafiti………………………………………………………………………………..10

1.13 Maelezo ya tatizo…………………………………………………………………………...11

**SURA YA PILI**

2.0 **DHANA YA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI**…………………………………………..12

2.1 Maana ya Rushwa…………………………………………………………………………...12

2.2 Dhana ya Uhujumu Uchumi………………………………………………………………...13

2.3Uhalifu Uliopangwa.......................................................................................................................14

2.4 Athari ya Rushwa…………………………………………………………………………..16

2.5 Uchunguzi wa masuala ya Rushwa………………………………………………………...18

2.6 Kurejesha Mali……………………………………………………………………………….19

2.7 Ufisadi………………………………………………………………………………………..20

2.8 Mbinu za Kuzuia vitendo vya Rushwa……………………………………………………………………..21
2.9 Kuwepo kwa vipimo vya Rushwa………………………………………………………………………..22
2.10 Kupambana na Rushwa katika manunuzi ya Umma……………………………………………..23
2.11 Uwajibikaji…………………………………………………………………………………………………...25
2.12 Upatikanaji wa taarifa za Rushwa na Uhujumu Uchumi………………………………………26
2.13 Aina za Rushwa na Uhujumu Uchumi…………………………………………………………………26
2.14 Sababu za Rushwa na Uhujumu Uchumi…………………………………………………………...27
2.15 Rushwa na Upatikanaji wa taarifa……………………………………………………………………...28
2.16 Rushwa na Uhujumu Uchumi katika Ulinzi na Usalama
Demokrasia na Utawala wa Sheria………………………………………………………………...29
2.17 Msaada wa Kisheria…………………………………………………………………………………………30

**SURA YA TATU**

3.0 **UCHAMBUZI WA SERA NA SHERIA……………………………………………………………….31**
**3.1 Sera………………………………………………………………………………………………………………31**
3.1.1 Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011………………………………………………………………..31
3.1.2 Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011………………………………………………………………..32
3.1.3 Sera ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014…………………………………………………………...33
3.1.4 Sera ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2010………………………………………………………34
3.2 Dira ya 2050 na MKUZA III……………………………………………………………………………...35
3.3 ILANI YA CCM ya 2020 - 2025………………………………………………………………………………37
3.4 Matamko ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar…………………………………………………………38
3.5 Sheria zinazohusiana na kuzuia rushwa na uhujumu uchumi……………………………38
3.5.1 Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984……………………………………………………………………38
3.5.2 Sheria ya Kuzuia Rushwa na uhujumu Uchumi Nam. 1 ya mwaka 2012………………..39
3.5.3 Sheria ya Kupambana na Utakatishaji Fedha Haramu Nam. 10 ya mwaka 2009…...41
3.5.4 Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na KUpambana na Dawa za Kulevya
Zanzibar, Nam. 8 ya mwaka 2021…………………………………………………………………………43
3.5.5 Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Nam. 1 ya mwaka 2003………………..44

3.5.6 Sheria ya Adhabu ya 2018……………………………………………………………………………45

3.5.7 Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016…..46

3.5.8 Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011……………………………………48

3.5.9 Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015……………………..48

**SURA YA NNE**

4.0 **MAONI YA WADAU**………………………………………………………………………………….50

4.1 **Utangulizi**……………………………………………………………………………………………….50

4.2 Maoni ya Kisheria……………………………………………………………………………………….50

4.3 Maoni ya Mfumo wa Kiutendaji……………………………………………………………………..56

**SURA YA TANO**

5.0 **MIKATABA YA KIMATAIFA NA SHERIA ZA NCHI MBALI MBALI……………………..63**

**5.1Utangulizi…………………………………………………………………………………………..63**

5.2 Mikataba ya Kimataifa……………………………………………………………………………..63

5.3 Mikataba ya Kisekta…………………………………………………………………………………..65

5.4 Vyombo muhimu vinavyohusika na utekelezaji wa Mikataba…………………………..68

5.5 SHERIA NA UZOEFU WA NCHI MBALI MBALI………………………………………………..71

**SURA YA SITA**

**6.0 MATOKEO YA UTAFITI…………………………………………………………………………..94**

**6.1 Njia zilizotumika katika Utafiti………………………………………………………………94**

6.2 Upeo wa Utafiti………………………………………………………………………………………..94

6.3 Ukomo wa Utafiti…………………………………………………………………………………….95

6.4 Sampuli ya Utafiti…………………………………………………………………………………….95

6.5 Hadidu Rejea……………………………………………………………………………………………102

6.6 Matokeo ya Utafiti……………………………………………………………………………………103

**SURA YA SABA**

7.0 **MAPENDEKEZO NA HITIMISHO**………………………………………………………………106

**7.1Mapendekezo………………………………………………………………………………………106**

**7.2 Hitimisho**…………………………………………………………………………………………………112

## REJEA

*SERA NA MIPANGO*

Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011
Sera ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2010,
Sera ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014
Dira ya 2050
Mpango wa Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA III)
Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)
Ilani ya CCM 2020-2025
Muongozo wa Kuzuia Rushwa nchini Tanzania wa 2020
Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu 2017-2022

**SHERIA**
Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984
Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Nam. 1 ya mwaka 2012
Sheria ya Kupambana na Utakatishaji Fedha Haramu Nam. 10 ya mwaka 2009
Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Nam. 8 ya mwaka 2021
Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Nam. 1 ya mwaka 2003
Sheria ya Adhabu ya 2018
Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016
Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011
Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015
Sheria ya Kudhibiti Uhujumu Uchumi ya 2019 yaTanzania
Sheria ya Kupambana na Rushwa Rwanda Nam. 54 ya 2018
Sheria ya Uhalifu ya New Zealand ya mwaka 1961
Sheria ya Kutangaza Mali ya Madagascar ya 2016
Sera ya Kuzuia Rushwa ya Denmark ya 2018
The Corrupt Practices and Other Related Offences Act, 2000 (the ICPC Act) Nigeria
The Economic and Financial Crimes Commission (Establishment) Act, 2004 (EFCC Act)Nigeria.

**KIMATAIFA**
Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa (UNCAC) wa mwaka 2004
Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (AUCPCC) mwaka 2007
Mkataba wa Nchi za Marekani (IACAC) wa mwaka 1997
Itifaki ya SADC dhidi ya rushwa Agosti, 2001
Shirikisho la Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa Afrika Mashariki. lililoundwa tarehe 28 Septemba, 2007

Kituo cha kupambana na rushwa cha nchi za Jumuia ya Madola Afrika kiliopo Gaborone Botswana
Jukwaa la Kupambana na Rushwa kwa Nchi za Kusini mwa Afrika (The Southern Afrika Forum against Corruption (SAFAC)
Shirikisho huru la Kimataifa la Mamlaka mbalimbali za kupambana na Rushwa IAACA
Mkutano wa Kimataifa wa Kupambana na Rushwa
Mkataba wa OECD wa Kupambana na Ufisadi wa Maafisa wa Kigeni na wa Umma katika Miamala ya Biashara ya Kimataifa
Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kupangwa wa Kimataifa
Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Rushwa inapatikana katika tovuti http://www.unodc.org/pdf/crime/convention_corruption/signing/Convention-e.pdf
Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa unapatikana http://www.africa-union.org/official documents/Treaties-Conventions-Protocols/Convention on Combating Corruption.pdf
Sera ya Kupambana na Rushwa ya mwaka 2018 ya Denmark
Zanzibar Strategy For Growth and Reduction Of Poverty (ZSGRP), Januari 2007,

**RIPOTI**

Amnesty International (AI) 'Egypt: Muzzling Civil Society', available at http://web.amnesty.org/library/Index/engMDE120212000?OpenDocument&of=COUNTRIES%5CEGYPT

Forms of Corruption Stephen D. Morris, CESifo DICE Report 2/2011, https://www.ifo.de/DocDL/dicereport211-forum2.pdf

Global Advice Network, "Public Anti-corruption Initiatives," Business Anti-Corruption Portal

Justice Africa Draft Report 'Defence Procurement, Corruption and Illicit Financial Flows' for The TANA High-Level Forum on Security in Africa February 2014 https://media.africaportal.org/documents/defence_procurement_corruption_and_illicit_financial_flows_final_1.pdf

Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya tatu, Ofisi ya Rais, Ikulu, Dar-es-laam, Tanzania, Julai 2017

OECD, 'Information sheet on the OECD Convention on Combating Bribery of Foreign Public Officials in International Business Transactions' (November 2002), www.oecd.org/dataoecd/52/24/2406452.pdf

Stephen D. Morris Forms of Corruption, CESifo DICE Report 2/2011, https://www.ifo.de/DocDL/dicereport211-forum2.pdf

Transparency International (TI), "National Intergrity Systems: Country Study Report Tanzania 2003," available at http://www.transparency.org/content/download/7395/45985/file/Tanzania_NIS_Study.pdf.

United Nation Convention against Corruption (UNCAC), http://www.unodc.org/documents/treaties/UNCAC/Publications/08-50026 E.pdf

World Bank projects on public procurement reform, https://projects.worldbank.org/en/projects-operations/project-detail/P098146

**VITABU**

A. Graycar, T. Prenzler. Understanding and preventing corruption. 2013; Palgrave Macmillan: Basingstoke, UK

Drake, P. W. (2009). *Between tyranny and anarchy: a history of democracy in Latin America, 1800–2006*. Stanford: Stanford University Press.

Tanzi, V., & Davoodi, H. (2000). Corruption, Public Investment, and Growth. IMF Working Paper No. 139. Washington: International Monetary Fund.

M. Johnston. Syndromes of corruption (2005) "Wealth, power, and democracy"; Cambridge University Press: New York

**MAKALA**

Abed, G., & Davoodi, H. (2000) Corruption, Structural Reforms and Economic Performance in the Transition Economies. IMF Working Paper No. 132. Washington: International Monetary Fund.

Abraham Kipkoech KemboiCRIMINAL JUSTICE SYSTEM RESPONSE TO THE PROBLEM OF CORRUPTION IN KENYA , ukurasa wa 233 https://www.unafei.or.jp/publications/pdf/RS_No92/No92_19PA_Kemboi.pdf

Andreoni, A. 2017. Anti-Corruption in Tanzania: A Political Settlements Analysis. SOAS, University of London.

https://eprints.soas.ac.uk/24853/1/ACEWorkingPaper001-TZ-AntiCorruption171102_final%20revised.pdf

A Keith Thompson Does anti-corruption legislation work? This article was previously published in the International Trade and Business Law Review, 2013, vol. XVI, pp. 99-135, and is reprinted with the permission of the Editor-in-Chief of the Review, Professor Gabriel A Moens, and of the author., World Customs Journal, Volume 7, Number 2 43

Alexeev, M., Janeba, E., Osborne, S.: Taxation and evasion in the presence of extortion by organized crime. J. Comp. Econ. 32, 375–387 (2004)

Attila, J. 2008. "Corruption, Taxation and Economic Growth: Theory and Evidence." CERDI-CNRS. Working paper

Bardhan, P. (1997). "Corruption and Development: A Review of Issues." Journal of Economic Literature, 35(3), 1320-1346.

Cooney, J,P., Global Mining: The Three Priorities in a Politically Challenging World. In: Northwest Mining Association Annual International Convention (4th-8th December, 1995), Spokane, Washington. Vancouver: Placer Dome Inc., 1995

Deniozos, Nikolaos and Vlados, Charis and Chatzinikolaou, Dimos, "Corruption as Form of Economic Crime and Government Effectiveness (May 6, 2018). Proceedings of the 3rd International Conference of Development and Economy I.CO.D.ECON, Kalamata, Greece, https://ssrn.com/abstract=3466321

Decision of the US Ninth Circuit Court of Appeals in Hilao v. Estate of Ferdinand Marcos et al., No. 03-16934, DC No. MDL-00840-MLR (28 December

DOIG, A., & Riley, S., Corruption and Anti-corruption Strategies: Issues and Cases Studies from Developing Countries in CHEEMA, G.S,.& J. Bovin (Eds), *Corruption and Intergrity Improvement Initiatives in Developing Countries*, 1998, ukurasa wa 45-62. Paris OECD

Dk. Edward G. Hoseah, The Southern African Forum Against Corruption inapatikana https://www.igg.go.ug/media/files/publications/SAFAC_Presentation_Buiumbura_by_Dr_Hoseah.pdf

Eurobarometer: Opinions on organized, cross-border crime and corruption. Special Eurobarometer 245/Wave 64.3-TNS Opinion and Social (2006)

Engelbert, Annika (2014) : The Role of Anti-Corruption Agencies in the Investigation and Prosecution of Procurement Related Corruption Cases, IEE Working Papers, No.

209, ISBN 978-3-927276-95-6Institute of Development Research and Development Policy (IEE), Ruhr University Bochum

Friedrich, C. (1972). Pathology of Politics, Violence, Betrayal, Corruption, Secrecy and Propaganda. New York: Harper & Row

G.E. Caiden. What really is public maladministration?. Public Administration Review. 51(6): 1991; 486–493.

Gyimah-Brempong, K. 2001. "Corruption, Economic Growth and Income Inequality in Africa." http://link.springer.com/article/10.1007/s101010200 045
Gupta, S., Davoodi, H., and Alonso-Terme, R. 2002. "Does Corruption Affect Income Inequality and Poverty?"
http://www.imf.org/external/pubs/ft/wp/wp9876.pdf
Gould D., "Administrative Corruption: Incidence, Causes and Remedial Strategies," in FARAZMAND, A. (ed.), Handbook of Comparative Development and Public Administration, New York: Marcel Dekker, 1991, p. 467.

Gray, Cheryl W., and Daniel Kaufmann, "Corruption and Development," Finance and Development, March 1998, p7-10.

GAN Integrity 2019 GAN Integrity. 2019. Tanzania Corruption Report. https://www.ganintegrity.com/portal/countryprofiles/tanzania/

GBN Ayittey 'Smart Aid for Africa', available at http://www.thisweekghana.com/ThisWeek/Commentary.AYITTEY.061505.htm

Hodgson, Geofrey M. & Shuxia Jiang, "The Economics of Corruption and the Corruption of Economics: An Institutionalist Perspective," Volume 41 Journal of Economic Issues, 2007, 1043 at 1044.

I. McAllister, J. Pietsch , A. Graycar . ANU poll: Perceptions of corruption and ethical conduct. 2012. Retrieved from http://politicsir.cass.anu.edu.au/polls-and-surveys/anupoll

Jorum Dui, "Corruption and Economic Crime", Transparency International, 2021, available at https://www.jstor.org/stable/resrep30836

J. Pope. Containing corruption in international transactions —The challenge of the 1990s. Commission on Global Governance. Issues in global governance: Papers written for the commission on global governance. 1995; Klewer Law International: London 67–90.

Karina Nazarova , Mariia Nezhyva , Volodymyr Hordopolov1 , and Viktoriia Mysiuk (2021) Anti-corruption audit as an imperative of effective environmental management 1 Kyiv National University of Trade and Economics, Financial Analysis And Audit Department, 19, Kyoto str., 02156 Kyiv, Ukraine, 2021 MATEC Web of Conferences 339, 010 (2021) ISTSML 2021
https://www.matec-conferences.org/articles/mateconf/pdf/2021/08/matecconf_istsml2021_01011.pdf
Kaufmann, D., Kraay, A. & Mastruzzi, M. (2003). Governance matters: governance indicators for 1996–2002. World Bank policy research department WP No. 3106.
Keith Blackburn, Kyriakos C. Neanidis1 · Maria Paola Rana1 (2017) A theory of organized crime, corruption and economic growth, 6 March 2017 Econ Theory Bull (2017) 5:227–245 DOI 10.1007/s40505-017-0116-5
https://link.springer.com/content/pdf/10.1007/s40505-017-0116-5.pdf

Kaunain Rahman Transparency International Anti-Corruption Helpdesk Answer Overview of corruption and anticorruption in Tanzania, 30 September 2019
https://knowledgehub.transparency.org/assets/uploads/helpdesk/Country-profile-Tanzania-2019_PR.pdf

Kilimwiko, L. 2019. In Tanzania, Local Structures in the Countryside Are Empowered for the Fight against Corruption. D+C Development and Cooperation.

Marie Chêne, Overview of Corruption in Tanzania, U4 Helpdesk, Transparency International, mchene@transparency.org Reviewed by: Robin Hodess Ph.D., Transparency International, rhodess@transparency.org Date: 4 March 2009, U4 Expert Answers provide targeted and timely anti-corruption expert advice to U4 partner agency staff, https://www.u4.no/publications/overview-of-corruption-in-tanzania

McNeish, H. 2015. Rampant Corruption in Tanzania Keeps Fruits of the Many in Hands of the Few. The Guardian

Transparency International 2019 Transparency International. 2019b. Global Corruption Barometer Africa 2019: Citizens' Views and Experiences of Corruption. https://www.transparency.org/files/content/pages /2019_GCB_Africa.pdf

László Kőhalmi, Dr. Kitti Mezei (2015) The Forever Changed Economic Crime, Часопис Національного університету "Острозька академія". Серія "Право". – 2015. – №2(12)
https://li.oa.edu.ua/articles/2015/n2/15kllcec.pdf

Lambsdorff, Johann Graf (2002c). Making Corrupt Deals – Contracting in the Shadow of the Law, Journal of Economic Behavior and Organization. 48: 221–241

Layne, K. & Lee, J. (2001). "Developing Fully Functional E-Government: A Four Stage Model." Government Information Quarterly. 18, 122-1

Lea Kaspar & Andrew Puddephatt (2012) Benefits of transparency in public procurement for SMEs General lessons for Egypt By Global Partners and Associates, March 2012

Mauro, Paolo, 1997, "The Effects of Corruption on Growth, Investment, and Government Expenditure: A Cross-Country Analysis," in Elliott (1997).

Mushtaq H. Khan G-24 Discussion Paper Series Governance and Anti-Corruption Reforms in Developing Countries: Policies, Evidence and Ways Forward, No. 42, November 2006, UNITED NATIONS

Nawaz, F. 2010. "Exploring the Relationships between Corruption and Tax Revenue." http://www.u4.no/publications/exploring-therelationships-between-corruption-and-tax-revenue/

Olan'g, L. and Msami, J. 2017. In Tanzania, Anti Corruption Efforts Seen As Paying Dividends, Need Citizen Engagement. http://afrobarometer.org/sites/default/files/publi cations/Dispatches/ab_r7_dispatchno178_corrupt ion_in_tanzania.pdf

Peter Grabosky, "The Prevention and Control of Economic Crime", inapatikanwa NO.55-tobira (unafei.or.jp)

Prof. Haroub Othman, University Of Dar Es Salaam (Team Leader) Prof. Rwekaza Mukandala, University of Dar Es Salaam Mr. Robert Makaramba, Human Rights & Good Governance Commission Dr. Per Tidemand, United Nations Capital Development Fund April 2003:

Ruben Carranza Plunder and Pain: Should Transitional Justice Engage with Corruption and Economic Crimes? https://www.ictj.org/sites/default/files/IJTJ-Global-Justice-Corruption-2008-English.pdf , International Journal of Transitional Justice, Vol. 2, 2008, 310–330

Revolutionary Government of Zanzibar, Ministry of Finance and Economic Affairs, The World Bank, Public Expenditure Review FY03 (January 31, 2003)

Rob DeVries, 'Liberia Truth Commission on Hold Due to Lack of Funds,' Jurist, 28 November 2006.

Stefan Sumah, Corruption, Causes and Consequences, Open Access pear- reviewed chapter inapatikana https://www.intechopen.com/chapters/58969

Stiglitz, J. E. – On Liberty, the Right to Know and Public Disclosure: The Role of Transparency in Public Life – Oxford Amnesty Lecture, January, 1999.

Thierry Ménissier. Corruption, Virtue and Republic in Machiavelli's Work. South-East European Journal of Political Science, 2013, South-East European Journal of Political Science, vol. I/2004, October-November-December 2013, p. 51-60

United Nations Conventions against Transnational Organized Crime (UNTOC) http://www.unodc.org/documents/treaties/UNTOC/TOC%20Convention/TOCebook-e.pdf

UNODC,The Doha Declaraion, PROMOTING A CULTURE OF LAWFULNESS, pia inapatikanwa https://www.unodc.org/e4j/en/anti-corruption/module-5/key-issues/forms-and-manifestations-of-private-sector-corruption.html

Vito Tanzi, (1998) International Monetary Fund, Fiscal Affairs Department, Corruption Around the World: Causes, Consequences, Scope and Cures, working Paper https://www.imf.org/external/pubs/ft/wp/wp9863.pdf

Walter Odhiambo and Paul Kamau, (2003 OECD DEVELOPMENT CENTRE Working Paper No. 208 (Formerly Technical Paper No. 208) PUBLIC PROCUREMENT: LESSONS FROM KENYA, TANZANIA AND UGANDA Research programme on: The Integration of Developing Countries into the World Trading System, March 2003 DEV/DOC 2003)06https://www.oecd.org/countries/uganda/2503452.pdf

Zanzibar Good Governance Strategic Plan Consultants' Report for UNDP Tanzania and Revolutionary Government of Zanzibar Final https://www.sheriasmz.go.tz/docs/RAccJxIkhY_Zanzibar_Good_Governance_Strategic_Plan_(ZGGSP)_Final_report.pdf

**TOVUTI**

https://www.brookings.edu/wp-content/uploads/2016/07/chapter-one_-corruption-sh-9780815727910.pdf
https://theconversation.com/from-our-ancestors-to-modern-leaders-all-do-it-the-story-of-corruption-102164
www.researchgate.net
http://www.cipce.org.ar
https://www.jstor.org/stable/resrep30836
https://www.sadc.int/files/7913/5292/8361/Protocol_Against_Corruption2001.pdf
https://www.oas.org/en/sla/dil/inter_american_treaties_b-58_against_corruption.asp
https://news.un.org/sw/story/2018/01/1002611
https://eaaaca.com/about-eaaaca
https://www.thecaacc.org/
https://www.thecaacc.org/about-us/
https://anticorruption.au.int/en/about

## SHUKRANI

Wazo la kufanyia mapitio Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi limetokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr Hussein Ali Mwinyi, kuimarisha taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa na Uhujumu Uchumi na kuagiza kuongezwa juhudi za kutekelezwa kwa Mpango wa Utekelezaji wa Kupambana na Rushwa kwa sekta za umma na sekta binafsi. Moja ya mapendekezo ambayo yametolewa kuhusu uimarishaji wa ZAECA, ni kuifanyia mapitio sheria ya ZAECA ili kukidhi mahitaji hayo, na kuzuia rushwa na ufisadi katika shughuli za kibiashara hasa katika mazingira ya utandawazi.

Shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuimarisha uwezo wa ZAECA katika kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Shukrani za dhati kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa usimamizi wake, pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa ZAECA ACP Ahmed Khamis Makarani na maafisa wake kwa kushirikiana na Tume katika kukamilisha Utafiti huu.

Shukrani nyingi kwa Katibu wa Tume Nd. Musa Kombo kwa kuwa Mtafiti Mkuu wa Utafiti huu na watafiti wenziwe Dr Mahfoudha Masoud Ali na Yakoub Rajab Juma kwa juhudi zao katika kukamilisha utafiti huu

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AU | African Union |
| CAACC | Commonwealth Africa Anti-Corruption Centre |
| CFAA | Country Financial Accountability Assessment |
| IAACA | International Association of Anti-Corruption Authorities |
| KMKM | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo |
| MDGs | Millennium Development Goals |
| MKUZA | Mkakati wa Kupunguza Umasikini Zanzibar |
| MLA | Mutual gal Assistance |
| NACSAP | The National Anti-Corruption Strategy and Action Plan |
| OCAG | Office of the Controller and Auditor General |
| OECD | The Organisation for Economic Co-operation and Development |
| PCCB | Prevention and Combating of Corruption Bureau |
| PFMRP | Public Financial Management Reform Programme |
| SADC | The *Southern African Development Community* |
| SAFAC | The Southern African Forum Against Corruption |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| UNTOC | The United Nations Convention against Transnational. Organized Crime |
| ZAECA | Zanzibar Anti-Corruption and Economic Crimes Authority |

**MUHTASARI**

Kihistoria, rushwa imeonekana kama kuwezesha baadhi ya aina za uhalifu wa kiuchumi na uhalifu uliopangwa, kupitia malipo yasiyo halali. Hata hivyo, aina za kisasa za rushwa na ufisadi zinaingiliana zaidi na uhalifu wa kiuchumi, na kutishia sio tu utulivu wa kiuchumi na kijamii wa nchi nyengine, lakini pia utawala wa sheria na demokrasia.

Kutokana na sifa hizi za kawaida, vyombo maalum vya kupambana na rushwa na uhalifu wa kiuchumi vinaweza kuleta tija ikiwemo Mamlaka zinazoundwa kama ZAECA. Aidha, ushirikiano wa kimataifa unahitajika katika uchunguzi na mashtaka ya rushwa na miradi ya uhalifu wa kiuchumi, pamoja na madhumuni ya kurejesha mali.

Uwazi katika masuala ya utumishi, manunuzi na ufadhili wa kisiasa unaweza pia kuhakikisha kuwa utedaji kazi na kampeni za kisiasa na uchaguzi hazichafuliwi na mapato ya rushwa na uhalifu wa kiuchumi, na inaweza kusaidia kuzuia na kukamatwa kwa wanaohujumu juhudi za Serikali.

Tanzania ilitia saini na kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Ufisadi (UNCAC) na ni mwanachama wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Mkataba wa AU). Katiba ya Zanzibar na Malengo ya Kitaifa na Mipango mbalimbali ikiwemo Dira 2050, MKUZA III na ILANI ya CCM zinaelekeza Serikali kupitisha njia ya kutokomeza rushwa na matumizi mabaya ya madaraka.

Sheria ya Kupambana na Rushwa ya mwaka 2012 na sheria nyengine zinafanyakazi kwa kuzingatia masharti ya kikatiba kuhusu kupambana na rushwa na uhujumu uchumi, ingawa mfumo wa kisheria unaoongoza na kupambana na rushwa na ufisadi barani Afrika unabadilika katika bara zima.

Kwa hiyo ni muhimu kuweka wazi tofauti kati ya mamlaka husika (ZAECA) na kuainisha mipango na mikakati ya kupambana na rushwa na uhujumu uchumi.

Zanzibar kama sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna haja ya kuimarisha ZAECA na kuweka misingi mizuri katika makosa na adhabu, uwezo wa Mamlaka, usimamizi wa mashtaka, taratibu zake za kutafuta ukweli, ukamataji mali, ulinzi wa watoa taarifa, fidia na mageuzi ya kitaasisi yaliyokusudiwa kutumika pamoja na kuwawajibisha wahusika wa ukiukaji mkubwa uliofanyika.

Ripoti hii inaeleza muhtasari wa mfumo wa kimataifa wa kupambana na rushwa na uhujumu uchumi, dhana ya rushwa na uhujumu uchumi, pamoja na miongozo inayotumika, katika mapambano dhidi ya rushwa. Aidha ripoti hii imechambua uzoefu wa nchi mbali mbali katika Kupambana na rushwa na Uhujumu Uchumi pamoja na maoni ya wadau mbali mbali kutoka Unguja na Pemba kuhusu namna ya kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa. Utafiti wa maeneo yote hayo umetumika katika kufikia Mapendekezo ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar juu ya namna ya Kurekebisha Sheria ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Nam 01 ya mwaka 2012 kwa lengo la Kuimarisha vita dhidi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi nchini.

Miongoni mwa mambo muhimu yaliyopendekezwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar katika ripoti hii ni pamoja na kuwepo kwa ushirikiano wa pamoja wa vyombo vya umma na vyombo binafsi katika mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi nchini. Katika kutimiza suala hili vyombo hivyo vinapaswa kuazimia kushirikiana kwa pamoja na kuiunga mkono kwa vitendo Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi

Zanzibar (ZAECA) katika kupambana na kutokomeza vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi katika vyombo vyao. Vyombo hivyo, mbali na kuwa na jukumu la kuzuia vitendo hivyo visitokee kwa kudhibiti mianya na viashiria vyote vya rushwa na uhujumu uchumi katika maeneo yao ya kiutendaji, pia vinapaswa kutoa taarifa yoyote kwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa haraka na kwa kadri itakavyowezekana pale zinapohitajika.

Aidha katika ripoti hii Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imependekeza utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuzingatia usawa, uwazi, ukweli na uadilifu. Taasisi ambazo jukumu lao la msingi ni kutoa huduma kwa wananchi zinawajibu mkubwa wa kuihudumia jamii bila ya ubaguzi wa aina yoyote, kuzingatia ukweli na uwazi wa taarifa na kutoa huduma kwa kuzingatia misingi ya haki na uadilifu. Kufanya hivyo kutaisaidia kwa kiasi kikubwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokomeza vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi katika maeneo mbali mbali ya utoaji huduma na kuwasaidia wananchi kuepukana na usumbufu usio wa lazima pale wanapofata huduma katika maeneo hayo.

Eneo jengine lililopendekezwa na Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ni pamoja na kuongezwa kwa adhabu kwa makosa mbali mbali ya rushwa na uhujumu uchumi. Miongoni mwa maeneo ambayo yanahitaji kuangaliwa na kufanyiwa marekebisho katika Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar Nam. 1 ya 2012 ni pamoja na eneo la adhabu. Kutokana na kasi ya mabadiliko ya kiuchumi na mwelekeo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi nchini, adhabu za kifungo na faini kwa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi zilizomo katika Sheria hiyo zinapaswa kuongezwa. Wale wote wanaotiwa hatiani na makosa hayo wapewe adhabu kubwa ili iwe fundisho la kuacha vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi kwao na kwa jamii kwa ujumla.

## SURA YA KWANZA

## 1.0 Utangulizi

### 1.1 Nadharia ya Rushwa na Uhujumu Uchumi

Rushwa na uhujumu uchumi wa nchi ni miongoni mwa vitendo viovu ambavyo kwa njia moja ama nyengine hufanywa na baadhi ya raia na watendaji katika sekta binafsi na sekta za umma. Watendaji hao hutumia vibaya nafasi na vyeo walivyonavyo kwa maslahi binafsi na kwa manufaa yao ya kiuchumi lakini pia raia huwashawishi watendaji kwa kuwapa rushwa ili waweze kupata wanachotaka kutoka Serikalini au ofisi binafsi, iwe huduma au bidhaa kwa njia isiyo halali.

Suala la rushwa na uhujumu uchumi ni tatizo la kijamii ambalo linamgusa kila mwananchi hivyo hakuna mwanajamii yeyote ambaye hahusiki na suala hili kwa kulikinga, kufanya, au kuathirika na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Vitendo kama vile upendeleo wa kijinsia katika taasisi, kutoa hongo, kufanya udanganyifu, kujitengenezea faida isiyofaa, matumizi mabaya ya mapato na mali za Serikali, kukwepa kodi, magendo, wizi, udanganyifu wa zabuni n.k vimeonekana kukithiri na kuota mizizi katika maeneo mbali mbali ya kiutendaji kuanzia ngazi za chini za Serikali za mitaa mpaka ngazi za juu za Serikali Kuu.

### 1.2 Mamlaka ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar ni Taasisi ya kiSerikali ambayo ipo chini ya Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imeanzishwa

na Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar Nam. 16 ya mwaka 1986. Kwa mujibu wa kifungu cha 4(1) cha Sheria hii Tume imepewa jukumu la kufanya mapitio ya Sheria zote za Zanzibar na kuzirekebisha pale inapobidi ili zilingane na muelekeo wa mabadiliko ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kwa watu wa Zanzibar.

Katika kutekeleza matakwa ya Sheria hii, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar kupitia watendaji wake hufanya tafiti za sheria mbali mbali ili kuona kwamba ipo haja ya kufanyiwa marekebisho, kufutwa au kuendelea kutumika kwa sheria hizo kulingana na mahitaji ya jamii za wazanzibari wote.

### 1.3 Lengo la utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuangalia suala la kudhibiti na kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi wa nchi katika mtizamo wa kisheria na maeneo mengine yasiyo ya kisheria na kutoa mapendekezo Serikalini. Lengo hili linazingatia:

(a) sheria iliyopo ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi, kubainisha ubora na udhaifu wake na kupendekeza maeneo ya kuimarishwa;

(b) kupendekeza mfumo ulio bora na imara kwa kuzuia tatizo la rushwa na uhujumu uchumi; na

(c) kupendekeza muundo mzuri zaidi wa vyombo vitakavyosimamia mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi nchini.

### 1.4 Tamko la tatizo la utafiti

Pamoja na uwepo wa jitihada mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar za kudhibiti na kupambana na tatizo la rushwa na uhujumu uchumi nchini, bado tatizo hili linaonekana kuwa lipo na kuenea kwa kasi katika maeneo mbali mbali ya kiutendaji na kupelekea athari kubwa katika maendeleo ya nchi. Miongoni mwa athari hizo ni pamoja na kupotea kwa haki, kukosekana ukweli na uwazi, kupungua uadilifu na uwajibikaji katika maeneo ya kazi na utekelezaji usioridhisha kwa miradi mbali mbali ya kimaendeleo nchini. Hivyo ipo haja ya kupitia sheria iliyopo ya Kuzuia na Kupambana Rushwa na Uhujumu Uchumi Nam. 1 ya mwaka 2012 kwa lengo la kubaini mapungufu yaliyomo katika sheria hiyo ili kuweza kutoa mapendekezo yatakayoimarisha ubora wa sheria hiyo na kuifanya itekelezeke kwa ufanisi na ilete tija kwa wananchi na Serikali kwa ujumla.

### 1.5 Umuhimu wa utafiti

Umuhimu wa utafiti huu ni kuangalia kwa kina tatizo la rushwa na uhujumu uchumi nchini na hatimaye kuandaa ripoti itakayotoa mapendekezo ya namna bora zaidi ya kukabiliana na tatizo hili. Aidha sheria itakayofanyiwa mapitio iainishe kwa ufasaha vitendo au masuala yanayohusu uhujumu uchumi.

### 1.6 Historia ya Rushwa na Uhujumu Uchumi

John Thomas Noonan, mmoja wa waandishi wachache ambao wamejaribu kuchunguza kwa kina na mada ya rushwa na ufisadi kwa karne nyingi na anajulikana kwa jina la “Mtu Maskini wa Nippur,” anaonesha rushwa ilianza katika miaka ya 1500 KK, ambapo anaonesha jinsi watu wa Mesopotamia ya kale na sheria ya usawa ya asili ya *quid pro quo* ilivyoheshimiwa sana,

ambapo watu waliokuwa wakitangatanga kufuata taratibu waliadhibiwa. Makosa hayakuwa katika tendo la kutoa zawadi yenye nia bali katika kuvunja mantiki ya ubadilishanaji: kwa kushindwa kutoa thamani kwa kubadilishana na thamani iliyopokelewa.[1]

Ufisadi na rushwa ni dhana za muda mrefu ambapo inaamimika nasaba ya Kwanza (3100-2700 KK) ya Misri ya kale ilibainisha ufisadi katika mahakama yake. Kitendo hiki pia kilikuwepo katika Uchina wa zamani. Katika hadithi za Kichina, kila kaya ina Mungu wa Jikoni ambaye hutazama tabia ya wanachama wake. Vivyo hivyo, mwanahistoria Mgiriki Herodotus asema kwamba familia ya Alcmaeonid ilihonga Makasisi wa kike wa Delphi, mojawapo ya nguvu za fumbo zenye nguvu zaidi za Ugiriki wa kale. Kuanzia 1400 KK, watu kote Ugiriki na kwengineko walikuja kujibiwa maswali yao na Pythia, kuhani mkuu wa Apollo. Familia tajiri ya Alcmaeonid ilijitolea kujenga upya Hekalu la Apollo kwa "*marble ya Parian*" baada ya kuharibiwa na tetemeko la ardhi. Kwa kujibu, Pythia alishawishi Sparta ya taifa kusaidia familia kushinda na kutawala Athene. Kwa kuwa ilifanya kazi, Aristotle alibaini hata miungu inaweza kuhongwa.[2]

Historia ya rushwa inahusishwa na kuanza kuundwa kwa mataifa na sheria, na tayari hapo zamani kitendo cha rushwa kilikuwa kikichukuliwa kuwa ni uasi ambao unaleta athari mbaya katika utawala wa umma na ufanisi mzima

[1] https://www.brookings.edu/wp-content/uploads/2016/07/chapter-one_-corruption-sh-9780815727910.pdf
[2] From our ancestors to modern leaders, all do it: the story of corruption, September 7, 2018 11.04am SAST, Corruption is as old as human history. www.shutterstock.com, inapatikana https://theconversation.com/from-our-ancestors-to-modern-leaders-all-do-it-the-story-of-corruption-102164

wa mifumo ya kisiasa.[3] Kumbukumbu za mwanzo za rushwa zilianzia karne ya kumi na tatu katika kipindi cha ustaarabu wa Assiria. Kutoka katika kumbukumbu zilizotambulika, zilizoandikwa katika vipande vya majabali, wanasaikolojia waliweza kutambua ni nani na jinsi gani alikubali rushwa. Chini ya Sheria ya Warumi, makosa ya jinai ya rushwa yalielezwa kuwa ni pamoja na kutoa, kupokea au kudai faida ili kumshawishi mfanyakazi kuhusiana na kazi yake. Kutokana na kuenea kwa rushwa nchini, Sheria hii iliongezewa sheria nyengine iliyolenga kuelezea fidia kwa uharibifu unaotokana na kitendo cha rushwa kuwa ni mara mbili zaidi ya uharibifu huo, na kupotea kwa haki za kisiasa kwa muhusika wa kitendo hicho cha rushwa. Hata hivyo, hili halikusaidia kuondoa rushwa, hasa kutokana na ukweli kwamba vitendo vya rushwa vilikuwa vikifanywa zaidi na wajumbe wa bunge na viongozi wakubwa wa nchi, katika taifa lenyewe la Roma na maeneo ya mbali ya majimbo ya Roma.[4]

Ukabila, katika kipindi chake cha awali, ulikuwa karibu na sheria mbali mbali ambazo zilitoa adhabu ya kifo kwa rushwa inayofanyika mahakamani. Baadae, wakati ukabila ulioendelea ulipoigeukia tena Sheria ya Kirumi, sheria mbali mbali zilijadili kuhusu matumizi mabaya ya madaraka. Mwishoni mwa ukabila, nchi zikawa hazina msaada katika mapambano dhidi ya rushwa, kama ilivofafanuliwa na kesi ya Ufaransa ambayo mnamo mwaka 1716 ilianzisha mahkama maalum iliyolazimika kusimamia kesi za matumizi mabaya ya fedha za kifalme; hata hivyo, matumizi haya mabaya (ubadhirifu, unyang'anyi, rushwa, ulaghai n.k) ya madaraka yalikuwa mengi sana kiasi ambacho

[3] Drake, P. W. (2009). *Between tyranny and anarchy: a history of democracy in Latin America, 1800–2006*. Stanford: Stanford University Press.
[4] www.researchgate.net

mahkama ilifutwa na msamaha wa jumla ulioanzishwa mwaka 1717 ulipelekea aina nyingi za rushwa kuonekana ni utamaduni tu na ni jambo la kawaida. Rushwa pia ilikuwa imeenea wakati wa kipindi cha Mahkama ya Kihispania, ambapo mwathirika wa mashtaka angeweza kufanya marekebisho kwa kutumia pesa, hali ambayo ilifanya rushwa kuwa kubwa hasa miongoni mwa wachunguzi. Katika historia, wasomi wengi walishughulika na rushwa au kutoa nadharia juu ya rushwa kwa njia moja au nyengine hupelekea mporomoko wa maadili, elimu na imani isiyo bora.[5]

Kihistoria, rushwa imeonekana kuwa ni kichocheo cha baadhi ya makosa ya uhujumu uchumi na uhalifu wa kupangwa, kwa mfano kupitia malipo ya rushwa kwa wakala wasimamizi wa sheria au ushawishi usiofaa katika kutoa maamuzi. Hata hivyo, aina mpya za makosa ya rushwa yameunganishwa na uhujumu uchumi. Aina zote hizi za makosa ya jinai hufanywa na watendaji hao hao, zinategemea mazingira sawa ya usafirishaji na utakatishaji fedha haramu, na kuinyuma jamii rasilimali nyingi za kifedha, hautishii kuimarika kwa jamii na uchumi wa nchi nyengine duniani kote tu bali pia hutishia utawala wa sheria na demokrasia.[6]

Hivyo basi, ijapokuwa rushwa imetawala katika jamii tangu enzi na enzi, lakini imepewa mazingatio zaidi katika miaka ya karibuni ambako tafiti mbali mbali kuhusiana na suala hili pamoja na athari zake mbaya zimekuwa mashuhuri zaidi baada ya mwaka 1995, wakati ambapo nchi na taasisi mbali mbali za

[5] Thierry Ménissier. Corruption, Virtue and Republic in Machiavelli's Work. South-East European Journal of Political Science, 2013, South-East European Journal of Political Science, vol. I/2004, October-November-December 2013, p. 51-60 https://hal.archives-ouvertes.fr/hal-01660762/document

[6] Jorum Dui, "Corruption and Economic Crime", Transparency International, 2021, p. 1. available at https://www.jstor.org/stable/resrep30836

kimataifa zilipoanza kuwa makini na tatizo hili. Mtazamo wa watu juu ya rushwa ulikuwa, na mpaka hivi sasa, haupo upande wowote.[7]

## 1.7 Historia ya mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar

Mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi nchini yalianza zaidi ya miaka 45 iliyopita kwa kupitisha Amri ya Rais "Decree" chini ya Sura Nam. 4 ya mwaka 1975 baada ya kuanzishwa kwa Kamisheni ya Kupambana na Rushwa. Miaka 10 baadaye, Amri hiyo ilifutwa ambapo makosa yote yaliingizwa kwenye Sheria ya Adhabu Nam. 10 ya mwaka 1985 na baadae kuanzishwa kikosi maalum cha kudhibiti na kupambana na rushwa. Kikosi hiki kilikuwa chini ya Jeshi la Polisi "Anti-corruption squad". Kikosi hicho kilisita kufanya kazi zake mwaka 2003. Mwaka mmoja baadae Sheria ya Adhabu ilifutwa na kuandikwa upya ambapo makosa yote yaliyohusiana na rushwa yakaingizwa katika Sheria hiyo. Sheria hiyo iliyoonekana kupambana na rushwa ilitambulika kuwa ni Sheria ya Adhabu Nam. 6 ya mwaka 2004.[8]

Wakati Zanzibar ikiendelea na kuandaa mazingira ya kupinga rushwa kisheria, mwezi Disemba mwaka 2005 kulipitishwa Azimio la Kimataifa la Mapambano dhidi ya Rushwa 'UNCAC' ambapo moja ya sharti la UNCAC ni kuzitaka nchi wanachama ikiwemo Tanzania kuwa na sheria inayopinga rushwa ambapo miaka sita baadae Zanzibar ilianza kwa uanzishwaji wa Sera.

[7] Gray, Cheryl W., and Daniel Kaufmann, "Corruption and Development," Finance and Development, March 1998, ukurasa wa 7-10.
[8] http://www.pembatoday.co.tz

Mwaka 2012 kulitungwa rasmi Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Nam. 1 ya mwaka 2012.[9]

## 1.8 Historia kwa upande wa Tanzania Bara

Mapambano dhidi ya rushwa yalikabiliwa na changamoto mbali mbali katika miaka ya 1980 – 1990. Changamoto katika kukabiliana na rushwa zilipelekea kuanzishwa kwa Kanuni za Maadili ya Viongozi wa Umma ambazo zilitungwa mnamo mwaka 1995.[10] Hii ilikuwa ni hatua nzuri katika kushughulikia masuala ya rushwa kwa kuyataja moja kwa moja makosa, idara na wakala ambao wamehusishwa na rushwa.[11]

Hali hii ilisaidia kuanzishwa kwa Mifumo ya Kitaifa juu ya Utawala Bora pamoja na Mpango Kazi na Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa mnamo mwaka 1999 (NACSAP)[12] na Serikali juu ya malengo ya NACSAP, na Ofisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCB) iliyoanzishwa mwaka 2007 na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.[13] Hii ni awamu ya pili ya Mpango Kazi na Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa ambao ulizinduliwa rasmi na Serikali tarehe 10 Disemba 2006. Mpango huu unatafsiri Sera za Serikali za kupambana na rushwa, matarajio na mitazamo

---

[9] ibid

[10] TRANSPARENCY INTERNATIONAL (TI), "National Intergrity Systems: Country Study Report Tanzania 2003," available at http://www.transparency.org/content/download/7395/45985/file/Tanzania_NIS_Study.pdf.

[11] DOIG, A., & Riley, S., Corruption and Anti-corruption Strategies: Issues and Cases Studies from Developing Countries in CHEEMA, G.S,. & J. Bovin (Eds), *Corruption and Intergrity Improvement Initiatives in Developing Countries*, 1998, ukurasa wa 45-62. Paris OECD.

[12] GLOBAL ADVICE NETWORK, "Public Anti-corruption Initiatives," Business Anti-Corruption Portal available at http//www.business-anti-corruption.com/country-profiles/sub-Saharan-africa/tanzania/initiatives/public-anti-corruption-initiatives.

[13] Sheria Nam. 11 ya 2007, Cap 329.

kwa masharti ya utendaji na utekelezaji kupitia malengo muhimu ya kimkakati.[14]

## 1.9 Chimbuko la Utafiti

Chimbuko la mapitio ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi ni dhamira ya Serikali ya kupambana na rushwa na uhujumu wa uchumi ili kuleta maendeleo kwa taifa.

Aidha, mapitio ya Sheria hii pia yalitokana na maamuzi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuiwezesha na kuipa nguvu zaidi taasisi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, kwa kuiwezesha kitaalamu, vitendea kazi na watendaji, hali iliyolazimisha mapitio ya Sheria hii ili iweze kutekelezeka ipasavyo.

## 1.10 Njia zilizotumika katika Utafiti

Katika utafiti huu mbalimbali zilitumika na kusaidia kupatikana taarifa zilizoweza kufanikisha malengo yaliyokusudiwa katika utafiti ikiwemo, kufanya mikutano na wadau walioainishwa kwa ajili ya kutoa maoni Unguja na Pemba, Kufanya majadiliano na taasisi za Serikali, taasisi Binafsi na Asasi za Kiraia kwa lengo la kupata michango yao juu ya kuzuia na kupambana na rushwa na uhujumu uchumi pamoja na kupitia Sheria mbalimbali na Rejea ambazo zinazozungumzia masuala ya rushwa na uhujumu uchumi.

Aidha, marejeo ya Sera, vitabu, Makala na nyaraka mbali mbali zinazozungumzia rushwa na uhujumu uchumi zimepitiwa na Tume, kwa lengo

[14] Khadija Shamte Mzee, (2014) Access to Information and Protection of Informers under Anti-Corruption Legislation in Zanzibar and Tanzania Mainland, Zanzibar Yearbook of Law, Vol. 4, 2014, p. 303

la kupata uelewa wa sekta hiyo na jinsi inavyofanya kazi na namna ya kuendeleza utawala bora na kuja na mapendekezo yatakayoimarisha utawala bora Zanzibar.

### 1.11 Hadidu Rejea

Katika kufanya utafiti huu Hadidu Rejea zifuatazo zilizingatiwa:

(a) Kufanya utafiti wa kina katika taratibu za utawala bora ikiwemo suala la kupambana na rushwa na uhujumu uchumi;

(b) Kuangalia uzoefu wa sheria za nchi mbali mbali kuhusiana na masuala ya kupambana na rushwa na uhujumu uchumi na kupendekeza namna uzoefu huo unavyoweza kutumika Zanzibar;

(c) Kuangalia sera na sheria mbali mbali za Zanzibar zinazohusiana na utawala bora na kupambana na rushwa na uhujumu uchumi;

(d) Kupitia mikataba ya kimataifa inayohusiana na eneo hili la utafiti na kuangalia mambo ya msingi yanayoweza kuzingatiwa katika Sheria itakayopendekezwa;

(e) Kutoa mapendekezo yanayofaa ya kisheria na kisera kwa ajili ya kuweka utaratibu mzuri na kuipa nguvu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi;

(f) Kukamilisha mapitio ya sheria na kuwasilisha Ripoti Serikalini.

### 1.12 Ukomo wa Utafiti

Katika kufanya utafiti huu mapungufu yafuatayo yamejitokeza:

(a) Kutokuwepo kwa uelewa wa sheria na makosa yanayohusiana na rushwa na uhujumu uchumi kwa baadhi ya wadau hasa watendaji walio katika sekta ya umma.

(b) Kutokuwepo uhamasishaji wa mara kwa mara kwa jamii kuhusu athari za rushwa na uhujumu uchumi.

(c) Ufahamu wa watendaji wa kutokutafautisha baadhi ya majukumu ya taasisi zinazoshughulikia masuala ya rushwa na uhujumu uchumi na masuala ya sheria.

### 1.13 Maelezo ya tatizo

Ingawa masuala ya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar yanaongozwa kwa misingi ya Utawala Bora, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Nam. 1 ya 2012 imeweka vifungu vya kuzuia na kupambana na pamoja na vifungu ambavyo vimeainisha makosa na adhabu kwa yoyote ambaye atakwenda kinyume na Sheria.

# SURA YA PILI

## 2.0 DHANA YA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI

### 2.1 Maana ya Rushwa

Neno "rushwa" linatokana na neno la kilatino "corruptus", lenye maana ya "kuharibika, kuvunjika au kuharibiwa".[15] Neno rushwa halina tafsiri moja, tafsiri ya neno hilo inatofautiana kutoka eneo moja hadi eneo jengine na tafsiri yake hulingana na mazingira.[16]

Aidha, rushwa inatafsiriwa kuwa ni kuahidi, kutoa, kupokea au kushawishi moja kwa moja au kupitia wakala, kitu chochote cha thamani ili kukiuka utaratibu katika utoaji wa maamuzi.[17] Rushwa hutafsiriwa pia kuwa ni matumizi mabaya ya madaraka aliyokabidhiwa mtu na kutumia madaraka hayo kwa manufaa binafsi.

Rushwa inajumuisha malipo haramu yanayofanywa kabla au baada ya huduma kutolewa, kwa maafisa wanaotumia vibaya mamlaka yao, na vitendo hivi vinahusisha shughuli kati ya raia na afisa wa serikali au taasisi binafsi. Rushwa pia inajumuisha ufisadi na ubadhirifu, pale ambapo viongozi wa umma wanafanya kazi ili kugeuza fedha za umma kwa matumizi yao binafsi.[18]

---

[15] HODGSON, Geofrey M. & Shuxia Jiang, "The Economics of Corruption and the Corruption of Economics: An Institutionalist Perspective," Volume 41 Journal of Economic Issues, 2007, ukurasa wa 1043 at 1044.

[16] GOULD D., "Administrative Corruption: Incidence, Causes and Remedial Strategies," in FARAZMAND, A. (ed.), Handbook of Comparative Development and Public Administration, New York: Marcel Dekker, 1991, p. 467.

[17] Mkakati wa Taifa dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya tatu, Ofisi ya Rais, Ikulu, Dar-es-laam, Tanzania, Julai 2017, ukurasa wa 1

[18] FORMS OF CORRUPTION STEPHEN D. MORRIS, CESifo DICE Report 2/2011, ukurasa wa 10, https://www.ifo.de/DocDL/dicereport211-forum2.pdf

Rushwa ya kisiasa inahusisha "viongozi wa umma" na hivyo kutofautisha dhana na ufisadi unaofanyika ndani ya jamii  na ukubwa wa sekta ya umma. Makundi mawili makubwa ya rushwa kwa kuzingatia eneo la kitaasisi ni pamoja na Ufisadi wa "kiwango cha juu" na "kiwango cha chini" unaohusisha watumishi wa umma.[19]

## 2.2 Dhana ya Uhujumu Uchumi

Uhujumu uchumi unajumuisha makosa mbali mbali, kuanzia uhalifu wa kifedha unaofanywa na benki, ukwepaji kodi, utakatishaji fedha, uhalifu unaofanywa na maafisa wa umma (kama vile hongo, ubadhirifu, usafirishaji haramu n.k).[20] Uhujumu uchumi unachukuliwa kama ni moja ya mambo yanayosababisha uharibifu mkubwa wa jamii. Hiyo ni kwa sababu uhujumu uchumi hauathiri tu taasisi za kidemokrasia bali pia unadhoofisha hazina ya Serikali kwa kumega rasilimali zilizopo ambazo zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa sera za umma.[21]

Wananchi ndio waathirika wakuu wa rushwa na uhujumu uchumi ingawa athari yake katika jamii katika uhalifu wa kawaida haionekani, hivyo ni vigumu sana kufahamu athari za moja kwa moja za uhalifu wa rushwa na uhujumu uchumi.[22]

---

[19] Stephen D. Morris Forms of Corruption, CESifo DICE Report 2/2011, https://www.ifo.de/DocDL/dicereport211-forum2.pdf, ukurasa wa 10,

[20] Justice Africa Draft Report 'Defence Procurement, Corruption and Illicit Financial Flows' for The TANA High-Level Forum on Security in Africa February 2014 https://media.africaportal.org/documents/defence_procurement_corruption_and_illicit_financial_flows_final_1.pdf

[21] http://www.cipce.org.ar

[22] ibid

Uhujumu Uchumi, kwa upande mwengine, maana yake ni kitendo kinachofanywa na mtu au kundi la watu kwa lengo la kujipatia faida ya kitaaluma au ya kifedha kinyume na sheria na huathiri maslahi ya jamii. Uhujumu Uchumi umeelezewa na baadhi ya wataalam kama ni udanganyifu unaodhihirika katika namna mbali mbali, ikiwemo utakatishaji fedha haramu, rushwa na ubadhirifu.[23]

Tafsiri ya uhalifu wa kiuchumi unajumuisha kila uhalifu, ukiukwaji, mitazamo isiyo ya kimaadili, ambayo inasababisha kupata kipato kiuchumi kinyume cha sheria au manufaa ya umma. Aidha, aina za uhujumu uchumi ni pamoja na udanganyifu wa uwekezaji wa mtaji, kupotosha watumiaji, ufilisi wa kitapeli, kukwepa kodi, udanganyifu wa bima na malipo, udanganyifu wa kadi za malipo, uhalifu wa mitandao, rushwa na utakatishaji fedha haramu.[24] Uhujumu uchumi vile vile unahusishwa na kuharibu mali za Serikali kwa makusudi au hata mali za wananchi ambao huzitumia kuzalisha na kujipatia kipato ambapo Serikali inategemea kodi kutokana na shughuli hizo.

## 2.3 Uhalifu uliopangwa

Maana ya kundi la uhalifu uliopangwa kuwa ni kundi lilioundwa na watu wawili au zaidi, waliokuwepo kwa muda na kufanya kazi pamoja kwa lengo la kufanya uhalifu mkubwa ili kupata, moja kwa moja au vyenginevyo, faida ya kifedha au nyenzo nyengine.[25] Ushahidi unaonesha uhusiano wa karibu kati ya

[23] Mauro, Paolo, 1997, "The Effects of Corruption on Growth, Investment, and Government Expenditure: A Cross-Country Analysis," in Elliott (1997).

[24] Dr. László Kőhalmi, Dr. Kitti Mezei (2015) The Forever Changed Economic Crime, Часопис Національного університету "Острозька академія". Серія "Право". – 2015. – №2(12) https://li.oa.edu.ua/articles/2015/n2/15kllcec.pdf ukurasa wa 1

[25] Tanzi, V., & Davoodi, H. (2000). Corruption, Public Investment, and Growth. IMF Working Paper No. 139. Washington: International Monetary Fund.

uhalifu uliopangwa na uhalifu wa kiuchumi. Kwa mfano, tathmini ya mwisho ya tishio la uhalifu mkubwa wa kupangwa wa Europol (2017) umeorodhesha aina nane kuu za tishio la uhalifu wa kupangwa ikijumuisha uhalifu wa mtandao, uzalishaji, usafirishaji na usambazaji haramu wa madawa, magendo ya wahamiaji, uhalifu wa mali uliopangwa, usafirishaji haramu wa wanaadamu, fedha za uhalifu na utakatishaji fedha haramu, udanganyifu wa nyaraka, biashara ya mitandao kwa bidhaa na huduma haramu. Hata hivyo, ni muhimu kuzingatia kuwa uhalifu wa kupangwa na wa kiuchumi havifanani. Kwa mfano baadhi ya makosa ya viwango vidogo kama vile wizi au udanganyifu wa kushirikiana, hauhusishi makundi ya uhalifu wa kupangwa.[26]

Kwa ujumla, uhalifu uliopangwa unaweza kukuza ufisadi katika viwango vyote vya ofisi ya umma kwa kulenga maeneo tofauti kama polisi, mahakama na utawala wa kisiasa.[27] Hitimisho la jumla la waangalizi na watendaji wengi ni kwamba uhalifu uliopangwa hustawi zaidi wakati utendaji kazi wa taasisi za umma za jamii unahujumiwa na rushwa.[28] Kwa mujibu wa Europol, uhujumu uchumi ni biashara yenye faida kubwa na hasara ndogo, na imekuwa ikihusishwa zaidi na kundi la uhalifu uliopangwa.[29]

Si vigumu kuelewa ni kwa nini makundi ya wahalifu yangetaka kuvutia umma na wasimamizi wa sheria, kwenye ufisadi. Kufanya hivyo kunatoa matarajio ya fursa kubwa zaidi za kushiriki katika shughuli haramu na uwezekano mdogo

[26] Ibid p. 3. available at https://www.jstor.org/stable/resrep30836
[27] Eurobarometer: Opinions on organized, cross-border crime and corruption. Special Eurobarometer 245/Wave 64.3-TNS Opinion and Social (2006)
[28] Keith Blackburn, Kyriakos C. Neanidis1 · Maria Paola Rana1 (2017) A theory of organized crime, corruption and economic growth, 6 March 2017 Econ Theory Bull (2017) 5:227–245 DOI 10.1007/s40505-017-0116-5 https://link.springer.com/content/pdf/10.1007/s40505-017-0116-5.pdf ukurasa wa 228
[29] Ibara ya 2(a) ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kupangwa wa Kimataifa

wa kugunduliwa na kufunguliwa mashtaka. Shughuli kama hizo zina uwezekano mkubwa wa kutokufuata sheria na kutekeleza sheria, hasa kwa maafisa ambao wako tayari kupokea rushwa kwa ajili ya upendeleo.[30]

## 2.4 Athari za Rushwa

Rushwa na Uhujumu Uchumi ni janga ambalo lina athari hasi katika jamii. Hupelekea kudhoofika kwa demokrasia katika nchi, ukiukwaji wa haki za binaadamu, uharibifu katika mfumo wa masoko, husababisha mmong'onyoko wa maadili katika jamii, huchelewesha maendeleo ya nchi, kufanyika kwa matukio ya kupangwa, ugaidi na vitisho vyengine vinavyotishia ustawi na usalama wa raia.[31]

Kuwepo kwa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi nchini kunaleta athari kubwa hasa katika sekta muhimu ya kiuchumi ambayo ndio tegemeo la kuleta maendeleo chanya ya taifa. Miongoni mwa athari hizo ni pamoja na:

(a) kuondoka kwa mifumo ya matumizi ya umma katika rasilimali muhimu za kudumu kwa ajili ya elimu na afya;

(b) kupungua kwa ufanisi wa uwekezaji wa umma na miundombinu ya nchi;

(c) kupungua kwa mapato ya kodi kwa kuathiri uwezo wa utawala wa Serikali wa kukusanya kodi na ada, ingawa athari halisi inategemea na namna gani kodi ya kwaida na namna nyengine za udhibiti zilizochaguliwa na viongozi, zimewekwa wazi kwa rushwa.[32]

[30] Alexeev, M., Janeba, E., Osborne, S.: Taxation and evasion in the presence of extortion by organized crime. J. Comp. Econ. 32, 375–387 (2004)
[31] Gray, Cheryl W., and Daniel Kaufmann, "Corruption and Development," Finance and Development, March 1998, p7-10.
[32] www.researchgate.net

Katika kiwango cha jumla, fasihi kwa ujumla inaonesha kwamba rushwa ina athari mbaya, moja kwa moja ukuaji wa uchumi na maendeleo.[33] Ufisadi pia una athari zisizo za moja kwa moja kwa uchumi wa nchi utendaji kwa kuathiri mambo mengi yanayochochea ukuaji wa uchumi kama vile uwekezaji, kodi, kiwango, muundo na ufanisi wa umma.[34] Rushwa na uhujumu uchumi inapotosha motisha na nguvu ya soko, na kusababisha mgawanyo mbaya wa rasilimali.[35]

Rushwa, inapokuwepo, inaweza kukwaza malengo ya Serikali kwa sababu ya wahusika kufanya vitendo vya rushwa ambavyo havilingani na manufaa ya Serikali.[36] Rushwa humuathiri kila mwanaadamu ambaye maisha yake, riziki zake au ustawi wake unategemea uadilifu wa watu walioshikilia nafasi katika mamlaka au taasisi fulani. Rushwa inatishia utulivu na usalama wa jamii, na huduma za kuimarika kwa demokrasia na maadili mema na kuathiri jamii ambayo ni nguvu kazi ya taifa.[37] Kwa mfano kuathirika kwa vijana wanaojihusisha na madawa ya kulevya.

Rushwa inakiuka haki ya msingi ya usawa wa binadamu na ni tishio kubwa kwa utulivu wa kisiasa, na usalama wa demokrasia na maendeleo ya

---

[33] Gyimah-Brempong, K. 2001. "Corruption, Economic Growth and Income Inequality in Africa." http://link.springer.com/article/10.1007/s101010200 045
Gupta, S., Davoodi, H., and Alonso-Terme, R. 2002. "Does Corruption Affect Income Inequality and Poverty?" http://www.imf.org/external/pubs/ft/wp/wp9876.pdf
[34] Friedrich, C. (1972). Pathology of Politics, Violence, Betrayal, Corruption, Secrecy and Propaganda. New York: Harper&Row
[35] Kaufmann, D., Kraay, A. & Mastruzzi, M. (2003). Governance matters: governance indicators for 1996–2002. World Bank policy research department WP No. 3106.
[36] COONEY, J,P., Global Mining: The Three Priorities in a Politically Challenging World. In: Northwest Mining Association Annual International Convention (4th-8th December, 1995), Spokane, Washington. Vancouver: Placer Dome Inc., 1995.
[37] Sera ya Kupambana na Rushwa ya mwaka 2018 ya Denmark, ukurasa wa 1

kiuchumi.[38] Ushahidi wa athari za rushwa katika ukuaji wa uchumi unathibitisha kuwa rushwa ina athari hasi ya moja kwa moja na katika ukuaji wa uchumi katika nchi zenye kipato cha chini.[39]

Inapochukua sura ya ukwepaji kodi, rushwa inaweza kusababisha hasara kubwa katika mapato ya kodi zilizokusanywa katika nchi, ambayo kwa upande mmoja kuna uwezekano wa kuwa na athari mbaya za kibajeti.[40] Rushwa na uhujumu uchumi si inapunguza tu uwiano wa kodi kwa Pato la Taifa, lakini pia husababisha uharibifu wa muda mrefu wa uchumi kwa kuongeza ukubwa wa uchumi, kupotosha kiwango halisi cha kodi, kudhoofisha maadili na msingi wa mapato ya nchi.[41]

## 2.5 Uchunguzi wa masuala ya rushwa

Ushirikiano wa kimataifa unahitajika katika uchunguzi na mashtaka yote ya rushwa kubwa na mpango wa uhujumu uchumi na pia kwa madhumuni ya kurejesha mali zilizotokana na makosa ya rushwa na uhujumu uchumi. Uwazi katika ufadhili wa kisiasa vile vile unaweza kuhakikisha kwamba kampeni za kisiasa na kichaguzi hazichafuliwi na mapato ya rushwa na uhujumu uchumi.[42]

---

[38] Deniozos, Nikolaos and Vlados, Charis and Chatzinikolaou, Dimos, "Corruption as Form of Economic Crime and Government Effectiveness (May 6, 2018). Proceedings of the 3rd International Conference of Development and Economy I.CO.D.ECON, Kalamata, Greece, ukurasa wa 1, inapatikana https://ssrn.com/abstract=3466321

[39] Abed, G., & Davoodi, H. (2000) Corruption, Structural Reforms and Economic Performance in the Transition Economies. IMF Working Paper No. 132. Washington: International Monetary Fund.

[40] Nawaz, F. 2010. "Exploring the Relationships between Corruption and Tax Revenue." http://www.u4.no/publications/exploring-therelationships-between-corruption-and-tax-revenue/

[41] Attila, J. 2008. "Corruption, Taxation and Economic Growth: Theory and Evidence." CERDI-CNRS. Working paper

[42] Ibid

## 2.6 Kurejesha mali

Aidha, Mpango wa Benki ya Dunia wa Kufuatilia Mali Iliyoibiwa, na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Dawa na Uhalifu (UNODC) inaunganisha kwa uwazi juhudi za kurejesha mali na uwajibikaji kwa ufisadi mkubwa na kiwango cha nchi iliyoathiriwa kimaendeleo. Hata hivyo, juhudi hizi za kurejesha mali hazizingatii uwajibikaji kwa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, sheria inaonesha uwezekano wa kuchanganya mifumo hii.[43]

Kwa kuwa athari za kijamii na kiuchumi za ufisadi mkubwa ni wa kiwango kikubwa sana, Serikali zina haja ya kutafuta mbinu za kupunguza athari hii, kutafuta na kurejesha mali iliyokusanywa na viongozi wa sasa au wa zamani wala rushwa. Nchi zilizoathiriwa mara nyingi hujikuta katika hali mbaya ya kukosa uthibitisho na nguvu za kisiasa zinazohitajika kushughulikia maeneo ambayo benki na taasisi za fedha zimehifadhi fedha hizo. Ingawa nchi kama Uswizi na Uingereza zimekuwa zikijaribu kwa umakini kuondoa misingi ya ufujaji wa mali za umma zilizopatikana kwa njia isiyo halali, changamoto za kurejesha mali hazijapungua kwa kiasi kikubwa kwa waathirika wa rushwa.[44]

Tatizo mara nyengine ni nchi nyingi zilizoathiriwa na rushwa na uhujumu uchumi haziwezi kumudu gharama za mashtaka hasa kuendesha kesi katika wigo wa kimataifa, haziwezi hata kulinganisha rasilimali zinazopatikana kwa wahalifu. Hii inaongeza umuhimu wa kutafuta njia mbadala ya kufichua ukweli kuhusu rushwa (ikiwa ni pamoja na mahali pa mapato), kupata

[43] Ruben Carranza Plunder and Pain: Should Transitional Justice Engage with Corruption and Economic Crimes? https://www.ictj.org/sites/default/files/IJTJ-Global-Justice-Corruption-2008-English.pdf , ukurasa 319 International Journal of Transitional Justice, Vol. 2, 2008, 310–330

[44] Rob DeVries, 'Liberia Truth Commission on Hold Due to Lack of Funds,' Jurist, 28 November 2006.

ushirikiano wa wahalifu wa kiwango cha chini na kupata njia ambayo inaweza kusimama kama ushahidi katika mashtaka ya wahalifu wa kiwango cha juu.[45]

Jitihada za kurejesha mali hazisaidii moja kwa moja katika uwajibikaji kutoka kwa watawala wa zamani. Urejeshaji wa Mali kama Nyenzo ya Fidia ni tatizo linalozikumba nchi nyingi, ingawa hiii si suluhu ya kina kwa tatizo la kufadhili mipango ya wahalifu wa uhalifu wa kiuchumi.[46]

## 2.7 Ufisadi

Ufisadi si dhana inayoeleweka kwa urahisi. Kwa ujumla, majaribio ya kisheria ya kufafanua kikamilifu mipaka ya "ufisadi" hushindwa, kutokana na asili ya maneno yenyewe. Rushwa inaeleweka na inajumuisha aina nyingi za tabia, kama vile hongo, ulafi, matumizi mabaya ya taarifa na matumizi mabaya ya ofisi. Tabia hizi zinaweza kutendeka kwa njia tofauti za shughuli kama vile kuteua wafanyakazi, kupata huduma, kudhibiti shughuli kama vile kutoa vibali na leseni, ujenzi wa vitu n.k. Nyingi ya shughuli hizi hutokea kwa wakati mmoja katika sekta mbalimbali kama vile afya, usimamizi wa kodi, haki n.k., na katika maeneo mbalimbali, kama vile mikoa, mitaa au sehemu mahususi za kazi.[47]

---

[45] Ruben Carranza Plunder and Pain: Should Transitional Justice Engage with Corruption and Economic Crimes?
https://www.ictj.org/sites/default/files/IJTJ-Global-Justice-Corruption-2008-English.pdf , ukurasa 318 International Journal of Transitional Justice, Vol. 2, 2008, 310–330

[46] Decision of the US Ninth Circuit Court of Appeals in Hilao v. Estate of Ferdinand Marcos et al., No. 03-16934, DC No. MDL-00840-MLR (28 December

[47] G.E. Caiden. What really is public maladministration?. Public Administration Review. 51(6): 1991; 486–493.

Katika nchi tajiri hatua nyingi zimechukuliwa kukabiliana na hongo, ambazo kwa sasa imekuwa ni sifa ya maisha ya kila siku katika nchi masikini, ikiwemo dalili za ufisadi, zilizoelezewa na Michael Johnston muongo mmoja uliopita.[48] Ufisadi kama aina ya uhalifu wa kiuchumi ni suala la usalama wa kimataifa na hatimaye limetambuliwa kama changamoto ya kiwango cha juu kimataifa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Wengi huona ufisadi kuwa uhalifu na hongo kama njia tofauti ya kufanya biashara.[49]

Ufisadi unazifanya serikali kushindwa kufikia ustawi wa umma kwa sababu ya uzembe, ubadhirifu wa kodi, au kupotoshwa maamuzi ya umma.[50] Ugawaji wa rasilimali haufikiwi na huathiriwa na rushwa kwa sababu rushwa inatoa malipo makubwa kwa watu binafsi kuliko kunufaisha umma kwa ujumla.[51]

## 2.8 Mbinu za Kuzuia vitendo vya Rushwa

Eneo hili ni muhimu katika kuzuia na kupambana na rushwa. Upimaji wa mfumo wa udhibiti wa ndani na kutumia mbinu mbalimbali ni hatua za awali za ukaguzi wa kupambana na rushwa. Wakaguzi wanaweza kuzuia maeneo na vitendo vya rushwa, pale wanapobaini ukweli. Hii inawezekana kwa kuweka mazingira ya ufahamu wa umuhimu wa kupambana na rushwa katika kijamii kwa kila mwananchi. Lengo la kimkakati la sera ya kupambana na rushwa ni kupambana na rushwa katika ngazi zote kwa kuongeza uwazi wa mihimili ya Serikali, kuheshimu haki za binadamu na kiraia na uhuru, kujenga mazingira

[48] M. Johnston. Syndromes of corruption: Wealth, power, and democracy. 2005; Cambridge University Press: New York

[49] Gray, Cheryl W., and Daniel Kaufmann, "Corruption and Development," Finance and Development, March 1998, ukurasa wa 7-10.

[50] Bardhan, P. (1997). "Corruption and Development: A Review of Issues." Journal of Economic Literature, 35(3), 1320-1346.

[51] Lambsdorff, Johann Graf (2002c). Making Corrupt Deals – Contracting in the Shadow of the Law, Journal of Economic Behavior and Organization. 48: 221–241

ya kiuchumi na maendeleo.[52] Mabadiliko ya msingi yaliyopo katika utaratibu wa kisheria wa kupambana na rushwa yanaweka msingi wa kuboresha zaidi mifumo na ufikiaji wa kiwango kipya cha kufanya biashara kidijitali.[53]

## 2.9 Kuwepo kwa Vipimo vya rushwa

Ni muhimu kujaribu kupima rushwa kwa sababu kuu mbili. Kwanza, hatua za jumla hutoa dalili ya jinsi jamii inavyofanya vizuri kulingana na mkataba au Miongozo ya serikali na raia wake. Ikiwa kuna rushwa, unyang'anyi, matumizi mabaya, ikiwa miradi mikuu ya mitaji na maendeleo inahudumia maslahi ya kifedha ya mtu binafsi badala ya maslahi ya umma; ikiwa mashirika yatawahonga maafisa wa umma ili kuziathiri maliasili; ikiwa ukiukwaji wa haki za binadamu utavumiliwa; ikiwa usimamizi wa haki hauendani na utawala wa sheria; basi kwamba jamii ni fisadi zaidi kuliko wale ambao tabia hizi ni kidogo au si sehemu ya mfumo wa kijamii.[54] Pili, ikiwa tunajua ni kiasi gani cha rushwa ndani ya mamlaka na asili na wingi wa matukio hayo ya ufisadi, basi hatua za kurekebisha zinaweza kuwekwa na hatua za kuzuia zinaweza kutekelezwa.[55]

Ingawa kwa kawaida taarifa za kiutawala juu ya rushwa na uhujumu uchumi hazipatikani kwa urahisi, kwa kuwa shughuli hizi hufanywa katika usiri

---

[52] Karina Nazarova , Mariia Nezhyva , Volodymyr Hordopolov1 , and Viktoriia Mysiuk (2021) Anti-corruption audit as an imperative of effective environmental management 1 Kyiv National University of Trade and Economics, Financial Analysis And Audit Department, 19, Kyoto str., 02156 Kyiv, Ukraine, 2021 MATEC Web of Conferences 339, 010 (2021) ISTSML 2021 https://www.matec-conferences.org/articles/matecconf/pdf/2021/08/matecconf_istsml2021_01011.pdf

[53] ibid

[54] A. Graycar , T. Prenzler . Understanding and preventing corruption. 2013; Palgrave Macmillan: Basingstoke, UK, ukurasa wa 34

[55] Ibid ukurasa wa 34

mkubwa,[56] Ikiwa tabia ya rushwa na uhujumu uchumi itaripotiwa, na kama shitaka litaletwa, inaweza kuainishwa kama kupata pesa kwa vitisho, aina fulani ya wizi, au ukiukaji wa utoaji wa huduma ya umma. Ukiukaji mwengine ni utovu wa nidhamu badala ya rushwa na uhujumu uchumi, na hivyo kufanya kuwa vigumu kutenganisha taarifa sahihi za rushwa na kiwango cha tabia yoyote ya ufisadi, rushwa na uhujumu uchumi.[57]

## 2.10 Kupambana na rushwa katika manunuzi ya umma

Ununuzi ni mojawapo ya shughuli za msingi katika utawala wa umma: Serikali zinahitaji kupata bidhaa, kazi za ujenzi na huduma kwa njia yoyote ya kimkataba (kununua, kuajiri, au nyenginezo) ili kutekeleza majukumu yao.[58] Upatikanaji huo unafanywa na rasilimali kutoka kwa fedha za umma, zinazolenga kupata thamani bora ya fedha, na hivyo basi kufuata sheria kali zinazozingatia uwazi, ushindani na vigezo vyenye lengo katika kufanya maamuzi, ambavyo vina ufanisi, pamoja na mambo mengine, katika kuzuia rushwa.[59]

Ununuzi wa umma unakabiliwa sana na rushwa kwa sababu mbalimbali ikiwemo miundombinu, miradi na ununuzi, ujazaji wa mikataba hufikia kiasi kikubwa, na kufanya fursa za biashara kuvutia sana kwa wazabuni. Pili,

[56] J. Pope. Containing corruption in international transactions —The challenge of the 1990s. Commission on Global Governance. Issues in global governance: Papers written for the commission on global governance. 1995; Klewer Law International: London 67–90.

[57] I. McAllister, J. Pietsch , A. Graycar . ANU poll: Perceptions of corruption and ethical conduct. 2012. Retrieved from http://politicsir.cass.anu.edu.au/polls-and-surveys/anupoll

[58] Walter Odhiambo and Paul Kamau, (2003 OECD DEVELOPMENT CENTRE Working Paper No. 208 (Formerly Technical Paper No. 208) PUBLIC PROCUREMENT: LESSONS FROM KENYA, TANZANIA AND UGANDA Research programme on: The Integration of Developing Countries into the World Trading System, March 2003 DEV/DOC 2003)06 https://www.oecd.org/countries/uganda/2503452.pdf

[59] Art. 9 UNCAC

ununuzi unajumuisha hatua kadhaa za kiutaratibu, hali inayotoa milango mingi ya rushwa na uwezekano wa kuficha shughuli za kifisadi. Vivutio vya rushwa viko juu ambapo hatari ya kugundulika ni ndogo.[60]

Nchi zinazoendelea zinakabiliwa zaidi na rushwa katika manunuzi ya umma kwa sababu ya kiwango cha juu cha matumizi ya serikali, na kusababisha hasara kubwa ya rasilimali fedha. Zaidi ya hayo, nchi zinazoendelea zinahitaji uwekezaji maalum wa umma katika maeneo kama vile elimu na afya, ambapo rushwa inapendelea zaidi matumizi mabaya ya fedha za umma katika manunuzi yanayohitajika.[61]

Kwa kuzingatia madhara makubwa ya rushwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, taasisi za fedha za kimataifa zimeanzisha programu nyingi za mageuzi ya sekta ya umma katika nchi zinazoendelea, miongoni mwao kama mijadala ya mifumo ya kitaifa ya manunuzi ya umma,[62] ambapo mikakati ya kuzuia inazingatia sheria zinazoongezeka, uwazi na kanuni za manunuzi, kuwajengea uwezo maafisa manunuzi, na mafunzo ya maadili na uadilifu.Hatua hizi zinalenga kupunguza ushawishi wa kujihusisha vitendo vya rushwa.[63]

---

[60] Lea Kaspar & Andrew Puddephatt (2012) Benefits of transparency in public procurement for SMEs General lessons for Egypt By Global Partners and Associates, March 2012

[61] Engelbert, Annika (2014) : The Role of Anti-Corruption Agencies in the Investigation and Prosecution of Procurement Related Corruption Cases, IEE Working Papers, No. 209, ISBN 978-3-927276-95-6Institute of Development Research and Development Policy (IEE), Ruhr University Bochum

[62] World Bank projects on public procurement reform, https://projects.worldbank.org/en/projects-operations/project-detail/P098146

[63] Mushtaq H. Khan G-24 Discussion Paper Series Governance and Anti-Corruption Reforms in Developing Countries: Policies, Evidence and Ways Forward, No. 42, November 2006, UNITED NATIONS

## 2.11 Uwajibikaji

Uwajibikaji ni muhimu kwa kuwa una nafasi muhimu katika mapmbano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi. Uwajibikaji unahusiana na ukweli kwamba kwa uzingatiaji sahihi wa sheria na kanuni, wale wanaosimamia sheria lazima kuwajibika kwa matendo yao.[64]

Tangu siku za mwanzo za uhuru, Tanzania mara nyingi imekuwa ikitajwa kwa dhamira yake ya kukabiliana na rushwa na uhujumu uchumi. Alipoingia madarakani mwaka 1995, Rais Mkapa aliteua Tume yenye mamlaka ya kutathmini hali ya rushwa nchini na kuandaa mapendekezo. Tume ilitoa "ripoti ya Warioba" ambayo ilipelekea, mwaka 1999, kupitishwa kwa Mkakati na Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa (NACSAP). Alipoingia madarakani mwaka 2005, Rais Jakaya Kiwete alianzisha upya dhamira ya nchi ya kupambana na rushwa na uhujumu uchumi.[65]

Ufisadi mkubwa, ubadhirifu wa fedha, umasikini usimamizi wa fedha za umma na rasilimali, na urasimu katika afisi za serikali ni kikwazo katika kupunguza umasikini.[66] Tanzania kwa mfano licha ya kuwa na nia thabiti, karibu theluthi mbili ya Watanzania bado wanaishi katika umasikini,[67] kutokana na sababu za

[64] Vito Tanzi, (1998) International Monetary Fund, Fiscal Affairs Department, Corruption Around the World: Causes, Consequences, Scope and Cures, working Paper https://www.imf.org/external/pubs/ft/wp/wp9863.pdf

[65] Marie Chêne, Overview of Corruption in Tanzania, U4 Helpdesk, Transparency International, mchene@transparency.org Reviewed by: Robin Hodess Ph.D., Transparency International, rhodess@transparency.org Date: 4 March 2009, U4 Expert Answers provide targeted and timely anti-corruption expert advice to U4 partner agency staff, https://www.u4.no/publications/overview-of-corruption-in-tanzania

[66] Kaunain Rahman Transparency International Anti-Corruption Helpdesk Answer Overview of corruption and anti corruption in Tanzania, 30 September 2019 https://knowledgehub.transparency.org/assets/uploads/helpdesk/Country-profile-Tanzania-2019_PR.pdf

[67] Kilimwiko, L. 2019. In Tanzania, Local Structures in the Countryside Are Empowered for the Fight against Corruption. D+C Development and Cooperation. Lawrence Kilimwiko is a journalist, author and

rushwa. Watafiti wanaeleza kwamba rushwa ndio chanzo kikuu cha ukosefu wa usawa.[68] Nafasi ya Tanzania katika kupambana na rushwa na uhujumu uchumi inaimarika kwa mujibu wa takwimu za kimataifa, katika mwaka 2018 ilishika nafasi ya 992 kati ya nchi 180 na alama zimekuwa zikiimarika tangu mwaka 2015.[69] Kuwepo kwa urasimu katika maeneo ya leseni na vibali hasa vile vinavyotumia muda mwingi kupelekea kuwepo rushwa na uhujumu uchumi.[70]

## 2.12 Upatikanaji wa taarifa za rushwa na uhujumu uchumi

Katika mwaka 2016, Tanzania ilihakikisha masuala ya ufikiaji wa habari kivitendo, ingawa kunaelezwa kuwepo kwa mapungufu kadhaa ikiwemo kutoa kipaumbele kwa sheria nyengine yoyote inayoongoza utunzaji wa taarifa za serikali, Pili, Ushughulikiaji wa maombi ya kutoa taarifa, na sheria kuweka adhabu ya kifungo kwa maafisa ambao wanatoa habari isivyofaa.[71]

## 2.13 Aina za rushwa na uhujumu uchumi

Zipo aina mbali mbali za makosa ya rushwa. Miongoni mwa aina hizo ni pamoja na: Hongo, Upendeleo, Ubadhirifu, Mgongano wa kimaslahi,

communication consultant. He lives in Dar es Salaam, Tanzania. https://www.dandc.eu/en/article/tanzania-local-structures-countryside-are-empowered-fight-against-corruption

[68] McNeish, H. 2015. Rampant Corruption in Tanzania Keeps Fruits of the Many in Hands of the Few. The Guardian

[69] Transparency International 2019 Transparency International. 2019b. Global Corruption Barometer Africa 2019: Citizens' Views and Experiences of Corruption. https://www.transparency.org/files/content/pages/2019_GCB_Africa.pdf

[70] GAN Integrity 2019 GAN Integrity. 2019. Tanzania Corruption Report. https://www.ganintegrity.com/portal/countryprofiles/tanzania/

[71] Freedom House 2019

Unyang'anyi, Uharibifu wa hati,[72] Biashara ya habari au taarifa, Ushawishi wa biashara, zawadi na ukarimu.[73]

Zipo aina mbali mbali za makosa ya uhujumu uchumi wa nchi. Miongoni mwa aina hizo ni kama ifuatavyo; Utakatishaji fedha haramu, Wizi wa hakimiliki, Udanganyifu katika bima, Ulaghai dhidi ya Serikali, Ulaghai dhidi ya waajiri, Ulaghai dhidi ya watumiaji, Udanganyifu wa uuzaji wa simu, Udanganyifu dhidi ya wamiliki wa hisa na wawekezaji, Ulaghai wa malipo ya uzeeni, Udanganyifu katika mawasiliano, Udanganyifu wa kadi za mikopo, Ujasusi wa viwanda, Kughushi, na Udanganyifu wa fursa za kibiashara.[74]

## 2.14 Sababu za rushwa na uhujumu uchumi

Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2017, mambo yafuatayo yameainishwa kuwa ni miongoni mwa sababu kuu za rushwa na uhujumu uchumi:

(a) Tamaa na uchu wa fedha;
(b) Tamaa ya kuhodhi siasa za nchi na viwango vya juu vya masoko;
(c) Viwango vya chini vya demokrasia, ushirikishwaji hafifu wa wananchi na uwazi mdogo wa kisiasa;
(d) Viwango vya juu vya urasimu na mifumo ya utawala isiyo na tija;
(e) Uhuru mdogo wa vyombo vya habari;
(f) Migawanyo mikubwa ya kikabila na viwango vya juu vya upendeleo juu ya kikundi fulani cha watu;

[72] CMI/U4 Anti-Corruption, Resource Centre, inapatikanwa https://www.u4.no/terms#bribery
[73] UNODC,The Doha Declaraion, PROMOTING A CULTURE OF LAWFULNESS, pia inapatikanwa https://www.unodc.org/e4j/en/anti-corruption/module-5/key-issues/forms-and-manifestations-of-private-sector-corruption.html
[74] Peter Grabosky, "The Prevention and Control of Economic Crime", uk. 47, pia inapatikanwa NO.55-tobira (unafei.or.jp)

(g) kutokuwepo kwa usawa wa kijinsia;

(h) Umasikini, ukosefu wa ajira na machafuko wa kisiasa;

(i) Maambukizi ya vitendo vya rushwa kutoka nchi jirani;

(j) Viwango vya chini vya elimu na ukosefu wa kujitolea kwa jamii.

### 2.15 Rushwa na upatikanaji wa taarifa

Rushwa imechukua nafasi kubwa katika ukiukaji wa haki za upatikanaji wa taarifa katika bara la Afrika. Kwa mfano nchi ya Egypt, Serikali inajulikana kwa matukio yake mazito iliyopitia dhidi ya waandishi wa habari wanaojitokeza kuripoti matukio ya rushwa Serikalini, hivyo kuzuia haki ya watu kupata taarifa na haki za waandishi wa habari kusambaza maoni yao.[75] Matukio kama hayo yanaakisi zaidi vipimo ambavyo rushwa huathiri vibaya upatikanaji wa taarifa.[76]

Upatikanaji wa taarifa ni jambo muhimu linalochangia katika kupambana na rushwa kwa kuwezesha kutoa huduma au kuunda mazingira ambayo ukiukwaji unaweza kutokea.[77] Upatikanaji wa taarifa unaweza kuwa msingi wa hatua za pamoja za kupambana na rushwa kwa upande unaohitaji, kwa vile rushwa hutawala katika maeneo yasiyo na maadili mema, upatikanaji wa taarifa husaidia kupunguza rushwa.[78]

---

[75] Amnesty International (AI) 'Egypt: Muzzling Civil Society', available at http://web.amnesty.org/library/Index/engMDE120212000?OpenDocument&of=COUNTRIES%5CEGYPT

[76] GBN Ayittey 'Smart Aid forAfrica',available at http://www.thisweekghana.com/ThisWeek/Commentary.AYITTEY.061505.htm

[77] Kanokkan Anukansai, Corruption: The catalyst for violation of Human Rights, ukurasa wa 7

[78] Stiglitz, J. E. – On Liberty, the Right to Know and Public Disclosure: The Role of Transparency in Public Life – Oxford Amnesty Lecture, January, 1999.

## 2.16 Rushwa na Uhujumu Uchumi katika Ulinzi na Usalama, Demokrasia na Utawala wa Sheria

Kwa mujibu wa Shirika la Kimataifa la Uwazi- Ulinzi na Usalama, mchanganyiko wa rushwa na uhujumu uchumi unaweza kudhoofisha udhibiti na mfumo wa Serikali. Serikali iliyo dhaifu huruhusu wahalifu kujipenyeza katika taasisi za Serikali na kuchagua mtu binafsi na taasisi za usalama. Suala hili hutishia usalama wa nchi, kwa sababu maafisa huwa washiriki wakubwa katika vitendo vya rushwa na uhalifu, kwa kuruhusu wahalifu wasipewe adhabu na kuathiri faida inayotokana na masoko haramu kwa wanaadamu, silaha, madawa, almasi zilizokuwa hazijasafishwa, pembe za ndovu, mbao zinazovunwa kwa njia ya haramu na mafuta kutoka katika maeneo yaliyodhibitiwa kigaidi.[79]

Uimara wa uchumi pia huathirika kwa kadri rasilimali zinazohitajika kwa maendeleo zinavyoporwa, kusafirishwa nje ya mipaka ya nchi na kufichwa katika mamlaka za nchi za kigeni. Uwezo wa Serikali wa kutimiza wajibu wake, kutimiza haki za kijamii na za kiuchumi kwa raia na kuweka mazingira rafiki kwa ukuaji wa uchumi hudhoofishwa. Hali mbaya zaidi, Serikali inaweza hata kuwa haramu machoni mwa raia, na kusababisha kukosekana kwa utulivu wa kisiasa na kiuchumi. Rushwa na uhujumu uchumi hutishia utulivu, utawala wa sheria na demokrasia.[80]

Uhalifu wa mtandaoni ni wa aina mbalimbali, udukuzi haramu, ambao unakiuka takwimu na mifumo ya habari, ni hatari sana. Upatikanaji haramu

[79] Jorum Dui, "Corruption and Economic Crime", Transparency International, 2021, p. 11. available at https://www.jstor.org/stable/resrep30836
[80] Ibid p. 11

wa taarifa kwa msaada wa kompyuta na vifaa vipya inaweza kusababisha uharibifu mkubwa kwa maisha ya kiuchumi.[81]

## 2.17 Msaada wa Kisheria

Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu uliopangwa Kimataifa (UNTOC) unatambua rushwa kama moja ya makosa makubwa ya uhalifu wa kimataifa. Wahusika wa ufisadi na uhalifu wa uchumi katika hali nyingi huficha na kufuja mapato yao mbali na nchi yao kwa hofu ya kuwa wanafuatiliwa na mashirika ya Serikali. Hii inaleta changamoto katika uchunguzi na urejeshaji wa fedha hizo na mapato.[82]

Hivyo ushirikiano wa karibu kati ya nchi washirika inakuwa muhimu. Kati ya mwaka 1990 na 2005, kashfa kubwa zilitikisa nchi mbalimbali ambazo zimepoteza rasilimali nyingi za kifedha.[83] Chini ya Kifungu cha 13 cha UNTOC, Nchi Wanachama zinahitajika kushirikiana kwa madhumuni ya kutoa msaada muhimu wa ushahidi na kutaifisha mapato ya ufisadi na kuweka Msaada wa Kisheria wa Kuheshimiana (MLA), ambao ni utaratibu unaokubalika kimataifa wa kupata usaidizi kama huo.[84]

[81] Layne, K. & Lee, J. (2001). "Developing Fully Functional E-Government: A Four Stage Model." Government Information Quarterly. 18, 122-1

[82] United Nations Conventions against Transnational Organized Crime (UNTOC) http://www.unodc.org/documents/treaties/UNTOC/TOC%20Convention/TOCebook-e.pdf

[83] Abraham Kipkoech Kemboi CRIMINAL JUSTICE SYSTEM RESPONSE TO THE PROBLEM OF CORRUPTION IN KENYA , ukurasa wa 233 https://www.unafei.or.jp/publications/pdf/RS_No92/No92_19PA_Kemboi.pdf

[84] United Nation Convention against Corruption (UNCAC), http://www.unodc.org/documents/treaties/UNCAC/Publications/08-50026 E.pdf

# SURA YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA SERA NA SHERIA

### 3.1 Sera

Pamoja na kufanyika kwa jitihada kubwa za kutunga sheria maalum yenye kusimamia suala zima la kuzuia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar, bado mpaka hivi sasa hakuna sera maalum iliyotungwa kwa ajili ya kusimamia suala hili la kuzuia rushwa na uhujumu uchumi na kupambana na vitendo hivyo hapa nchini. Hata hivyo, suala la kuzuia rushwa na uhujumu uchumi nchini limetambuliwa na kutanabahishwa wazi wazi katika sera mbali mbali kwa dhumuni la kuepuka kufanyakazi kwa maslahi binafsi ili kuleta ufanisi mzuri wa kazi katika taasisi za umma na taasisi binafsi na kufikia lengo la kutoa huduma bora na zenye tija kwa jamii ya wazanzibari na kutekeleza kwa vitendo dhana ya utawala bora nchini. Miongoni mwa sera hizo ni pamoja na:

(a) Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011
(b) Sera ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014
(c) Sera ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2010

#### 3.1.1 Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011

Sera ya Utawala Bora ni sera mama inayoongoza na kufafanua kwa kina misingi bora na imara ya kuzingatiwa katika kufikia lengo kuu la mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar. Sera hii imeeleza vyema kuwa rushwa maana yake ni matumizi mabaya ya Ofisi ya umma kwa maslahi binafsi.[85] Miongoni mwa jambo la msingi sana la kuzingatiwa na

[85] Sera ya Utawala Bora, 2011 ukurasa wa 4

mtumishi yeyote ni pamoja na kufahamu kuwa Ofisi za umma hazipasi kutumika kwa maslahi binafsi bali zitumike kwa maslahi ya umma.

Ili kuwa na Utawala Bora nchini ni muhimu kutekeleza kwa vitendo na kusimamia ipasavyo misingi ya Utawala Bora. Miongoni mwa misingi hiyo ni pamoja na kuzuia rushwa na uhujumu uchumi. Sera ya Utawala Bora miongoni mwa malengo yake mahsusi ni pamoja na kuweka mifumo madhubuti ya kuzuia rushwa, kwani moja kati ya mambo yanayohatarisha Utawala Bora nchini ni rushwa. Katika kulibainisha suala hili, Sera ya Utawala Bora imetoa tamko kuwa Serikali itapambana na mizizi ya rushwa na kushajiisha ushirika wa umma katika vita dhidi ya rushwa katika taasisi za umma na jamii kwa ujumla.

Aidha Sera ya Utawala Bora, katika jitihada zake za kuzuia rushwa, imeweka mikakati ifuatayo:

(a) Serikali kutayarisha Mswada wa kupambana na rushwa; na
(b) Mswada wa Sheria ya kuzuia rushwa utapendekeza uanzishwaji wa mamlaka ya kupambana na rushwa ambayo itapamabana dhidi ya uongozi mbaya na vitendo vya rushwa. Sheria pia itapendekeza kuanzishwa kwa utaratibu wa kuwasilisha malalamiko na namna ya kuyatolea taarifa.

### 3.1.2 Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011

Kwa mujibu wa utafiti ambao umeufanywa, imebainika kwamba hakuna sera ya moja kwa moja inayohusiana na masuala ya udhibiti na ukaguzi wa hesabu za umma hapa Zanzibar. Hata hivyo, zipo baadhi ya sera na mipango mikakati

ya Wizara inayohusiana na utawala bora ambazo zimegusia taasisi za uangalizi kifedha na matumizi ya fedha za umma. Kwa mfano, tamko la sera lililoainishwa kwenye Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011 imeelezea ya kwamba, "[u]wezo wa taasisi za uangalizi kifedha utaongezwa ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi".[86] Ili kufikia tamko hili la sera, Wizara inayohusiana na utawala bora imeweka mikakati mbalimbali itakayowezesha mafanikio hayo. Miongoni mwa mikakati hio ni kama vile:

(i) Mchakato wa bajeti ya mwaka utaweka mkazo maalum kwa mahitaji ya kamati ya Hesabu za Serikali ya Baraza la Wawakilishi, na vile vile mahitaji ya Baraza la Wawakilishi kufanya shughuli za uangalizi kwa ufanisi.

(ii) Mchakato wa bajeti ya mwaka utaweka pia mkazo maalum kwa mahitaji ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamisheni ya Utumishi wa Umma na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa kwa shughuli zao za uangalizi.

(iii) Wizara inayohusika na Utawala Bora itakuwa na jukumu mahususi la kuhakikisha kwamba taasisi za uangalizi zinajengewa uwezo, vikiwemo vyombo vya habari, ili kutekeleza majukumu yao ya kutoa habari na kuweka kumbukumbu kuhusu utawala bora Zanzibar.

### 3.1.3 Sera ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014

Sera ya Serikali za Mitaa imetilia mkazo suala la udhibiti wa vitendo vya rushwa katika maeneo mbali mbali ya utoaji huduma kwa jamii pamoja na maeneo ya uchumi na uzalishaji. Sera hii ya Serikali za Mitaa imefafanua kuwa

[86] Sera ya Utawala Bora Zanzibar 2011, ukurasa wa 15

moja kati ya changamoto kubwa inayozikabili sekta zote za utumishi ikiwemo sekta ya utumishi wa Serikali za Mitaa ni kuwepo kwa vitendo vya rushwa.

Kutokana na mwamko mdogo wa kutambua majukumu na haki zao za msingi na kutokufuata maadili mema ya kiutendaji miongoni mwa watendaji wa Serikali za mitaa katika kutoa huduma kwa jamii, kunapelekea kwa kiasi kikubwa watendaji hao kujiingiza katika vitendo vya rushwa. Watendaji hao wasiokuwa waaminifu katika kazi zao, bila ya kuzingatia maadili ya kiutumishi, huomba na kupokea rushwa. Sera hii inaelekeza na kutoa wito kwa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa kushirikiana na washirika wengine katika kuinua mwamko wa wananchi juu ya haki zao za msingi pamoja na watumishi wa Serikali kufuata maadili ya utendaji yaliyowekwa na pia kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya watendaji wala rushwa.

### 3.1.4 Sera ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2010

Hii ni sera ambayo imejikita zaidi katika kufafanua misingi mbali mbali ya kiutumishi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwataka watumishi wote kufanya kazi kwa kuzingatia haki, usawa na maadili mema. Katika kuelezea misingi hiyo Sera ya Utumishi wa Umma imetoa tamko kwa watumishi wote wa umma kutoa huduma bila ya upendeleo ikiwa ni moja kati ya misingi mikuu ya Sera hiyo. Aidha, Sera imetanabahisha kuwa maamuzi ya uajiri yanafanywa bila kujali uhusiano, upendeleo au utashi wa kisiasa.[87]

Kwa mtumishi wa umma katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kutoa huduma kwa jamii kwa misingi ya upendeleo wa aina yoyote au taasisi za

[87] Sera ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2010, uk. 6

uajiri kutoa nafasi za ajira kwa kuzingatia uhusiano, upendeleo au utashi wa kisiasa ni miongoni mwa vitendo vya rushwa ambavyo ni makosa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

### 3.2 Dira ya 2050 na MKUZA III

Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini, unaojulikana kama MKUZA III ni mfumo wa tatu wa maendeleo ya kitaifa. Umejengwa katika Dira ya 2050, na inaambatana na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs) na mipango mengine ya kimataifa iliyokubaliwa kusaidia utekelezaji wa mpango wa kwanza na kutekeleza maoni ya tafiti mbalimbali zilizofanywa.

Kwa upande mwengine mkakati wa Tatu ulioandaliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya ukuzaji uchumi na upunguzaji wa umasikini, katika suala la utawala bora ulilenga kukuza uwezo wa afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kuimarisha kwa uwazi na uwajibikaji Serikalini.[88] Hii ni sawa na kusema kwamba masuala ya ukaguzi yana uhusiano mkubwa na maisha ya wananchi. Kutokana na uhusiano huo, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hutakiwa mara tu baada ya ukaguzi wao wa kimahesabu kuandika ripoti ambazo hutakiwa kuwasilishwa mbele ya chombo cha kutunga sheria kinachowakilisha wananchi kwa kuzitolea mapendekezo. Wananchi nao watapata haki ya kuweza kuitathmini Serikali yao kama inawajibika.

Mapitio ya Matumizi ya fedha za Umma (2003), Tathmini ya Uwajibikaji (CFAA, 2003), Uchambuzi wa Hali ya Uchumi ya Zanzibar, Utafiti juu ya

---

[88] Zanzibar Strategy For Growth and Reduction Of Poverty (ZSGRP), Januari 2007, uk. 7 na 97.

Viwanda vya karafuu, na Utafiti juu ya Mageuzi ya Serikali za Mitaa na Mpango Mkakati wa Utawala Bora; yote kwa pamoja yaligundua udhaifu katika uwajibikaji wa kifedha, matumizi ya umma, usimamizi wa mipango na ununuzi katika sekta za umma.[89]

Katika kutekeleza MKUZA, juhudi zilifanywa za kuoanisha sera ndani ya Zanzibar, kati ya Zanzibar na Tanzania Bara na kati ya Tanzania na Maazimio ya kimataifa, utekelezaji wa Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP), na Marekebisho ya Sheria. Malengo ya MKUZA mbali ya kupunguza umaskini, ni kutunza mazingira ya uchumi; kuongeza ukusanyaji wa mapato, Utawala Bora na kupunguza ufisadi kupitia kutekeleza Sheria ya PPDPA, na kuimarisha OCAG.

Dira ya Zanzibar 2050 na Mpango wa Tatu wa Kupunguza Umasikini Zanzibar umebainisha Utawala Bora kama jambo muhimu kwa maendeleo ya uchumi, ustawi wa jamii, amani na utulivu. Mchakato wa mageuzi katika maeneo ya ukaguzi unaongozwa na Serikali na unaungwa mkono na wananchi wengi. Uendelevu wa mageuzi umewekewa mkakati na mpango wa usimamizi ili kuleta mabadiliko, kupitia msaada mkubwa wa kisiasa na kiutawala.

Lengo kuu na uthibitisho wa utawala bora ni endelevu kisiasa, kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kwa ustawi wa watu. Kwa hivyo hatua ya

[89] Revolutionary Government of Zanzibar, Ministry of Finance and Economic Affairs, The World Bank, Public Expenditure Review FY03 (January 31, 2003)

kuimarisha utawala bora haisaidii kisiasa, kiutawala na kimfumo lakini pia kwa kiuchumi na kijamii.[90]

Eneo la ukaguzi na utawala bora ni la kimkakati kwa mujibu wa Mipango Mikuu ya Maendeleo ya nchi, ni jukumu la Ofisi kutoa huduma bora za ukaguzi na eneo hili linapaswa lisimamiwe ili kuongeza uwajibikaji na thamani ya fedha katika ukusanyaji na matumizi ya rasilimali za umma. Ukaguzi unatakiwa usiwe na upendeleo na ufanywe kwa uadilifu, kitaalam na viwango vya juu vya maadili kulingana na viwango bora vinavyotambuliwa.

## 3.3 ILANI YA CCM

Ilani ya CCM ya mwaka 2020-2025 katika ibara ya 197 imeeleza utekelezaji wa Ilani katika masuala ya kupambana na rushwa kwa kuchukuliwa hatua madhubuti na kuratibu mpango shirikishi wa kupambana na rushwa. Aidha katika ibara ya 198 pamoja na mikakati mengine utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kuzingatia misingi ya demokrasia imesisitizwa pamoja na kuipatia ZAECA wataalam na vifaa vya uchunguzi na kukamilisha Kanuni za udhibiti wa rushwa. Suala la elimu ya kuzuia na kupambana na rushwa limesisitizwa.

[90]Prof. Haroub Othman, University Of Dar Es Salaam (Team Leader) Prof. Rwekaza Mukandala, University of Dar Es Salaam Mr. Robert Makaramba, Human Rights & Good Governance Commission Dr. Per Tidemand, United Nations Capital Development Fund April 2003:
Zanzibar Good Governance Strategic Plan Consultants' Report for UNDP Tanzania and Revolutionary Government of Zanzibar Final
https://www.sheriasmz.go.tz/docs/RAccJxJkhY_Zanzibar_Good_Governance_Strategic_Plan_(ZGGSP)_Final_report.pdf

## 3.4 Matamko ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar katika matamshi yake ameonesha nia ya kuipa nguvu ZAECA na kukemea vitendo v ya rushwa kwa kuwaambia viongozi wa vikundi vya wajasiriamali kuwa hatafumbia macho hali halisi huku baadhi ya viongozi wakijihusisha na ufisadi mkubwa. Mheshimiwa Rais ameeleza kwamba haridhishwi na maendeleo ya baadhi ya miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa huku akibainisha kuwa kuna mengi yanatakiwa kufanywa katika baadhi ya miradi inapofanyiwa tathmini ya thamani ya fedha.

Aidha amebainisha kwamba matokeo katika miradi yote mikubwa ya maendeleo inayotekelezwa – ikiwa ni pamoja na Mradi wa Huduma za Mijini Zanzibar (ZUSP) ambao umetumia dola milioni 93, na miradi ya maji iliyotumia fedha nyingi za umma haikufanya vizuri.[91]

## 3.5 Sheria zinazohusiana na kuzuia rushwa na uhujumu uchumi

### 3.5.1 Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984

Katika kuleta maendeleo ya watu na ustawi wa jamii nchini, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 imeeleza namna bora kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuendeshwa kwa kuzingatia maadili mema na kuondoa kabisa vitendo vya rushwa. Serikali ina wajibu wa kuchukua jitihada za kila namna kuhakikisha watu waliopewa dhamana za uongozi huiongoza jamii ya watu wa Zanzibar katika misingi imara ya utawala bora na utawala wa sheria kwa kuepuka kutumia vibaya vyeo walivyopewa na kujiepusha na vitendo vya rushwa.

[91] There's shocking rot in Zanzibar govt, says Mwinyi, FRIDAY DECEMBER 18 2020 https://www.thecitizen.co.tz/tanzania/news/-there-s-shocking-rot-in-zanzibar-govt-says-mwinyi-3232908

Wajibu wa kikatiba wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kupambana na rushwa ambao umelezwa katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ni pamoja na kuondosha kabisa vitendo vya rushwa na utumiaji mbaya wa cheo dhidi ya umma kwa wale wote walio na madaraka.[92]

Ili kuleta maendeleo ya kiuchumi nchini na kusimamia ipasavyo dhamana za uongozi katika ngazi mbali mbali za utawala, watu waliopewa madara na vyeo kuwaongoza wazanzibari wanalazimika kujiepusha kushiriki katika vitendo vya rushwa na kusimamia ipasavyo vitendo hivyo visitokee katika maeneo yao ya kazi kwa kadri itakavyowezekana. Kufanya hivyo kutasaidia jamii kuepukana na dhulma na upotevu wa haki zao za msingi na hivyo, kupelekea kuwepo kwa upatikanaji bora wa huduma.

### 3.5.2 Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Nam. 1 ya mwaka 2012

Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ni sheria maalum iliyotungwa ili kudhibiti na kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi katika taasisi za umma na taasisi binafsi nchini. Sheria hii imelenga kudhibiti miyanya na viashiria vyote vya rushwa na uhujumu uchumi kwa watendaji wa ngazi zote katika taasisi hizo ili kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia misingi ya haki, uadilifu na maslahi ya umma katika kutoa huduma kwa jamii na kulinda uchumi wa nchi.

Aidha Sheria hii imeanzisha mamlaka maalum inayojulikana kama ni Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu uchumi ambayo inaongozwa na Mkurugenzi

[92] Kifungu cha 10(b), Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, ukurasa wa 5

Mkuu ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu mwenye wajibu wa kusimamia shughuli za kila siku za Mamlaka. Miongoni mwa kazi za Mamlaka hiyo ni pamoja na:

(a) kupokea na kuchunguza malalamiko yoyote yanayohusiana na vitendo vya rushwa katika chombo cha umma au chombo binafsi;

(b) kulifanyia uchunguzi suala lolote ambalo, katika maono ya Mkurugenzi Mkuu, linaibua shutma kwamba lolote kati ya mambo yafuatayo limetokea au litatokea:

 (i) kitendo kinachoashiria rushwa au uhujumu uchumi; na

 (ii) kitendo kinachoonekana kuruhusu, kushajiisha au kusababisha kitendo kinachoashiria rushwa au uhujumu uchumi;

(c) pale Mamlaka inapoombwa na mtu au taasisi, kutoa ushauri na kumsaidia mtu au taasisi juu ya njia ambazo mtu huyo au taasisi hiyo inaweza kuzuia vitendo vya rushwa n.k.[93]

Pia Sheria hii imeipa uwezo Mamlaka, katika kutekeleza kazi zake, kushirikiana na mtu yeyote au chombo chochote ikiwa itahitajika kufanya hivyo, na katika kutimiza azma hiyo mtu huyo au chombo hicho kitawajibika kwa hali yoyote kuonesha ushirikiano kwa Mamlaka. Sheria hii imebainisha makosa mbali mbali yanayohusiana na rushwa na uhujumu uchumi yakiwemo makosa ya kutoa au kupokea hongo, udanganyifu, ushawishi wa siri, wizi wa zabuni, matumizi mabaya ya mapato na mali za Serikali, kukwepa kodi, kukusanyia bidhaa kwa lengo la kuendesha bei au maslahi binafsi, faida isiyofaa kwa wadhamini wa kuteuliwa, magendo, utakatishaji fedha haramu, biashara ya dawa za kulevya, fedha na bidhaa bandia, mpango uliokusudiwa kuendesha viwango vya fedha za kigeni kinyume na sheria, matumizi mabaya

[93] Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi, uk. 6

ya ofisi, kuhamisha mapato yanayotokana na rushwa, upendeleo wa kijinsia n.k.

Vile vile katika kudhibiti vitendo vya rushwa na uhujumu uchumu nchini, Sheria hii imempa mamlaka Mkurugenzi Mkuu au mtu mwengine yeyote alieteuliwa na Mkurugenzi Mkuu kufanya uchunguzi wa vitendo hivyo kwa niaba ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Aidha kwa kuzingatia umuhimu wa usalama katika kufanya uchunguzi wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi, Sheria hii imetoa mamlaka, fursa na kinga ya kuwa na afisa polisi kwa Mkurugenzi Mkuu au mtu mwengine yeyote aliyepewa mamlaka na Mkurugenzi Mkuu kufanya uchunguzi wa makosa chini ya Sheria hii.

### 3.5.3 Sheria ya Kupambana na Utakatishaji Fedha Haramu Nam. 10 ya mwaka 2009

Sheria hii ni miongoni mwa sheria muhimu sana katika kudhibiti na kupambana na vitendo vya uhujumu uchumi wa nchi. Miongoni mwa vitendo hatarishi kwa uchumi wa nchi ni utakatishaji fedha haramu unaofanywa na watu binafsi, vyombo vya ushirika au watendaji wa Serikali wasio waaminifu katika nafasi zao. Kifungu cha 7(1) cha Sheria hii kimeeleza kuwa mtu yeyote anaejiingiza au kufanya kitendo kinachoanshiria utakatishaji fedha haramu anafanya kosa chini ya Sheria hii.

Aidha kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki kimefafanua mazingira tofauti ya utendaji kosa kwa kukusudia ikiwa mtu atafanya mambo yafuatayo:

(a) atajiingiza, moja kwa moja au vyenginevyo, katika miamala ambayo itahusisha chumo linalotokana na kosa la jinai wakati anafahamu au ana kila sababu ya kufahamu au angepaswa kufahamu kuwa chumo hilo linatokana na kosa la jinai;

(b) atabadilisha, atahamisha, atasafirisha au kupitisha, mali wakati anafahamu, ana kila sababu ya kufahamu au angepaswa kufahamu kuwa chumo hilo linatokana na kosa la jinai, kwa lengo la kuficha asili ya mali isiyo halali au kumsaidia mtu ambaye amehusika katika kutenda kosa hilo kukimbia hatua za kisheria dhidi ya kitendo chake;

(c) atafìcha au kuzuia kuanzishwa kwa asili, chanzo, eneo, harakati, umiliki au haki kwa mujibu wa mali, wakati anafahamu au ana kila sababu ya kufahamu au angepaswa kufahamu kuwa chumo hilo linatokana na kosa la jinai;

(d) atapata, atamiliki, atatumia au kusimamia mali, wakati anafahamu au ana kila sababu ya kufahamu au angepaswa kufahamu kuwa wakati wa kupokea chumo hilo linatokana na kosa la jinai; au

(e) atashiriki katika, atashirikiana na, atakula njama katika kufanya, atajaribu kufanya, atasaidia na kuhimiza, au atawezesha au kushauri kufanyika kwa kitendo chochote kilichoelezwa katika aya (a) mpaka (d) ya kijifungu hiki.[94]

Pamoja na kufafanua mazingira tofauti ya utendaji kosa chini ya Sheria hii, Sheria hii pia imetoa adhabu zilizobainishwa katika kifungu cha 8 cha Sheria hii dhidi ya mtu yeyote atakaefanya kosa la utakatishaji fedha haramu. Kifuungu hicho kinaeleza kama ifuatavyo:

[94] Kifungu cha 7, Sheria ya Kupamabana na Utakatishaji Fedha Haramu Nam. 10 of 2009, ukurasa 18 na 19.

Mtu yeyote anayekwenda kinyume na masharti ya aya (a) mpaka (e) ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 7 cha Sheria hii, akitiwa hatiani.

(a) kama ni mtu pekee, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia moja au kifungo cha muda usiopungua miaka saba;

(b) kama ni chombo cha ushirika, kitawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni mia mbili na hamsini au mara tatu ya thamani ya soko la mali.[95]

### 3.5.4 Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Nam. 8 ya mwaka 2021

Miongoni mwa vitendo vinavyoashiria hujma dhidi ya uchumi wa nchi ni vitendo vya biashara ya dawa za kulevya nchini. Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Nam. 8 ya mwaka 2021 imetanabahisha kuwa kujiingiza katika biashara ya dawa za kulevya ni kufanya kosa chini ya Sheria hii. Sheria hii imeelezea tafsiri ya "dawa za kulevya" kuwa ni "dawa za nakotiki au saikotropiki na inajumuisha dawa nyengine ambayo moja kwa moja au vyenginevyo inahusiana na dawa za nakotiki au saikotropiki".

Sheria hii pia imeonesha makosa mbali mbali yanayohusiana na dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na makosa ya kuingiza ndani au kusafirisha nje ya nchi, kuzalisha, kuuza au kununua, kutoa, kusambaza, kuhifadhi, kugawanya au kufikisha utoaji wa dawa zenye uwezo wa kulewesha. Makosa yaliyobainishwa hapo juu ni miongoni mwa makosa dhidi ya uhujumu uchumi

[95]Kifungu cha 7, Sheria ya Kupamabana na Utakatishaji Fedha Haramu Nam. 10 of 2009, uk. 19 na 20.

wa nchi kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Nam. 1 ya mwaka 2021.

### 3.5.5 Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Nam. 1 ya mwaka 2003

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeona ipo haja ya kuunda kikosi maalum cha kuzuia magendo ikiwa ni miongoni mwa hatua muhimu ya kudhibiti vitendo vya uhujumu uchumi wa nchi. Kikosi hiki hufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria maalum ijulikanayo kama ni Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Nam. 1 ya mwaka 2003. Kifungu cha 4(1)(d) na (h) cha Sheria hii kimebainisha majukumu ya msingi ya Kikosi cha Kuzuia Magendo ikiwa ni pamoja na kuzuia shughuli za magendo nchini kwa njia zote zilizotumika, na kupambana na vitendo vya uhalifu vinavyofanyika baharini ikijumuisha kusafirisha dawa za kulevya.

Sheria hii imetafsiri neno 'magendo' kuwa ni kusafirisha nje ya nchi au kubeba mizigo baharini au kusafirisha au kuondoa bidhaa kwa lengo la kuhamisha bidhaa hizo muhimu na bidhaa nyengine zilizozuiliwa kutoa nje ya Zanzibar. Shughuli za magendo na vitendo vya usafirishaji wa dawa za kulevya baharini vinavyofanywa na wananchi wasio wazalendo kwa nchi yao ni miongoni mwa makosa yalikemewa vikali chini ya Sheria hii kwani ni miongoni mwa vitendo vya uhujumu uchumi wa nchi ambavyo hupelekea kuzorotesha maendeleo nchini.

### 3.5.6 Sheria ya Adhabu ya 2018

Sheria ya Adhabu ya mwaka 2018 ni miongoni mwa sheria bora ambazo zimefanyiwa maboresho makubwa na kuimarishwa ili zitumike kwa kuendana na wakati na uhalisia wa maisha ya wazanzibari. Sheria hii imekuja kuifuta Sheria ya Adhabu ya mwaka 2004. Sheria hii imefafanua vitendo mbali mbali vinavyohusiana na rushwa na uhujumu uchumi ambavyo kwa mujibu wa Sheria hii kufanya vitendo hivyo ni kosa na hivyo, kuekewa adhabu maalum. Miongoni mwa vitendo hivyo ni pamoja na:

**(a) Mkusanyiko kwa madhumuni ya kufanya magendo**

Kufanya magendo ni miongoni mwa makosa makubwa ya uhujumu uchumi wa nchi. Sheria hii imelibainisha kosa la mkusanyiko kwa madhumuni ya kufanya magendo kuwa hufanywa pale ambapo watu wawili au zaidi ambao hukusanyika pamoja kwa lengo la kuteremsha, kuchukua au kuficha bidhaa yoyote iliyolazimika kulipwa ushuru wa forodha na inayowajibika kutaifishwa na Serikali chini ya sheria yoyote inayohusiana na ushuru wa forodha. Sheria hii imetoa adhabu kwa watendaji wa kosa hilo kutozwa faini isiyozidi laki tano au kifungo kisichozidi miezi sita.[96]

**(b) Ubadhirifu na Udanganyifu wa Wakurugenzi na Maafisa wa Mashirika**

Vitendo vya ubadhirifu na udanganyifu unaofanywa na Wakurugenzi na Maafisa wa Mashirika mbali mbali vimeelezwa kuwa ni kosa chini ya Sheria ya Adhabu ya mwaka 2018.[97] Kutokana na tafsiri pana ya neno rushwa, vitendo

[96] Kifungu cha 72, Sheria ya Adhabu ya mwaka 2018, ukurasa wa 28.
[97] Kifungu cha 315, Sheria ya Adhabu ya mwaka 2018, uk. 104.

vya kufanya ubadhirifu na udanganyifu katika ofisi ni miongoni mwa makosa ya rushwa kwani vitendo hivyo vinatokana na matumizi mabaya ya ofisi.

**(c)Kughushi sarafu**

Miongoni mwa makosa makubwa ya uhujumu uchumi ni pamoja na kosa la kutengeneza bidhaa au fedha bandia. Sheria ya Adhabu ya mwaka 2018 imetanabahisha kuwa mtu yeyote ambaye anatengeneza au kujaribu kutengeneza sarafu bandia atakuwa ni mtenda kosa na hivyo, Sheria hii kumpa adhabu kali ya kifungo cha maisha mtu huyo.[98] Sarafu bandia ni sarafu ambayo sio halisi lakini inafanana au imekusudiwa kimuonekano ifanane au itumike kama ni sarafu halisi.

### 3.5.7Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016

Katika kuendeleza juhudi za kupambana na rushwa na uhujumu uchumi nchini, Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma imeweka vyem a misingi ya ununuzi na uondoshaji mali ili kuepusha vitendo vya rushwa. Misingi iliyowekwa ikiwemo mfumo maalumu wa ushindani wa wazi wa zabuni pamoja na njia ya kumpata na kumtangaza mshindi wa zabuni. Kifungu 37, 38 na 39 vya sheria hii.

Vile vile, Sheria hii imeweka wazi kanuni za ununuzi na uondoshaji mali kwa kuweka mpango maalumu wa ununuzi na uondoshaji mali pamoja na kuweka viwango vinavyokubalika katika uteuzi wa zabuni, muda wa zabuni na utartibu mzima wa uombaji wa zabuni mpaka kumalizika kwake. Kuweka

[98] Kifungu cha 355, Sheria ya Adhabu ya mwaka 2018, ukurasa wa 118.

wazi taratibu hizi na kutoa katazo kwa maofisa wa Serikali kushiriki katika taratibu za zabuni isipokua mpaka kuwe na jambo mahasusi.[99] Taasisi hii ya ununuzi imelazimishwa kufuata taratibu zilizowekwa ndani ya sheria katika taratibu zote za manunuzi jambo ambalo limepunguza vitendo vya rushwa katika sekta ya manunuzi.[100]

Kifungu cha 90 (d) cha sheria kinatoa uwezo kwa Mamlaka kumsimamisha mtoa huduma katika kushiriki juu ya hatua za ununuzi na uondoshaji wowote wa mali za umma kwa kipindi kitakachowekwa na Mamlaka iwapo mtoa huduma amepatikana na hatia kwa kosa la rushwa au vitendo vya udanganyifu.

Aidha, sheria hii katika kifungu cha 91(d) kinaeleza kuwa ni kosa kwa mtu kujishughulisha na vitendo vya rushwa. Vile vile kifungu cha 91 (2) (a) (b) vimeweka wazi kuwa ni kosa kwa Afisa Mhasibu, mjumbe wa Bodi ya Zabuni, mjumbe wa Kamati ya Tathmini, mfanyakazi wa Mamlaka au wa taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kushiriki katika vitendo vya rushwa wakati wa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma au wakati wa hatua za ununuzi au uondoshaji wa mali za umma. Kifungu hicho hicho kinaeleza adhabu kwa atakayepatikana na hatia kwa kosa la rushwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi Milioni moja au kifungo kwa kipindi kisichozidi mwaka mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja.

[99] kifungu cha 65
[100] kifungu cha 66

### 3.5.8 Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011

Sheria hii imeundwa kwa ajili ya kusimamia utumishi wa umma pamoja na kudhibiti muundo, uendeshaji na usimamizi wa taasisi zote za umma. Sheria hii imeweka Kanuni za maadili ya Utumishi wa Umma katika kifungu cha 7 (2) (a) kinamtaka kila muajiwa wa umma lazima kuwa mwaminifu na mwenye uadilifu.

Vitendo vya rushwa husababishwa pale muajiwa kushindwa kuwa mwaminifu au muadilifu hivyo, Sheria hii inasimamia vita dhidi ya rushwa kwa watumishi wa umma. Katika sheria hii imetoa kinga kwa watoa taarifa juu ya uvunjaji wowote wa kanuni za maadili. Kifungu cha 30 cha sheria hii kimeeleza kuwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma itahakikisha kuwa hakuna afisa wa umma atakaeonewa kwa kutoa taarifa kwa mamlaka husika juu wa uvunjaji wa maadili.

### 3.5.9 Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015.

Sheria hii imeweka misingi ya maadili ya viongozi wa umma. Katika kifungu cha 19(2) (b) Rais wa Zanzibar katika kuimarisha maadili ya viongozi wakati wa kupata viongozi wa Serikali basi ataangalia iwapo kiongozi hajawahi kuhusika na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi.

Aidha, kifungu cha 20 cha sheria hii kimeweka wazi vitendo ambayo vitapelekea kwa kiongozi wa umma kuvunja maadili ya uongozi iwapo atatumia ofisi yake kwa manufaa yake binafsi. Katika kuendeleza juhudi za kupambana na rushwa na uhujumu uchumi Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma imewataka viongozi wote kuwa na maadili na kutokufanya vitendo

vinavyokwenda kinyume na maadili na kuwakataza viongozi hao kutokujihusisha na vitendo vya uhalifu kama vile utapeli, wizi na ubakaji[101]. Mbali ya juhudi hizo Sheria hii imeewataka viongozi wote kutangaza mali zao wanazomiliki ikiwemo fedha ziliopo katika benki ya ndani ya nchi au fedha na mali nyengine zilizohifadhiwa nje ya nchi pamoja na kutangaza madeni waliyonayo pindi tu wanapokabidhiwa madaraka au kila baada ya mwisho wa mwaka kwa Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi. Uwekaji wazi kwa mali za viongozi kutasaidia kujulikana kwa kiongozi iwapo atachukua rushwa au atafanya vitendo vya uhujumu uchumi kwani mali zake zitakapoengezeka atatakiwa kuzitolea maelezo juu ya jinsi gani mali hizo ameweza kuzipata.[102]

Sheria hii imeweka utaratibu maalumu wa kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya uvunjifu wa Maadili kwa viongozi wa Umma. Sheria hii imemtaka Mwenyekiti wa Tume ya Maadili kusikiliza na kuyafanyia uchunguzi wa awali na iwapo atagundua kuwa malalamiko hayo yanamsingi na malalmikiwa anayokesi ya kujibu basi Mwenyekiti atamtaka kiongozi huyo kujibu madai hayo. Vile vile ndani ya vifungu hivyo kumewekwa utaratibu maalumu wa kusikiliza kukusanya ushahidi na taratibu nyengine kwa ajili ya kusikiliza madai au malalamiko juu ya kiongozi wa umma.[103] Kwa kumalizia kifungu cha 30 kimeweka adhabu za kuchukuliwa dhidi ya kiongozi wa umaa atakayepatikana na hatia.

[101] Kifungu cha 18 (1) (2) cha Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam 4 ya mwaka 2015.
[102] kifungu cha 16 na 17 cha sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma
[103] vifungu cha 23 hadi 29

# SURA YA NNE

## 4.0 MAONI YA WADAU

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea maoni ya wadau mbali mbali kuhusiana na Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Nam. 1 ya 2012 yenye kubainisha ubora na udhaifu wa sheria hiyo katika kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi hapa Zanzibar.

Wadau wametoa mapendekezo yao kuhusiana na sheria hiyo na kubainisha njia sahihi za kuhakikisha kwamba tatizo la rushwa na uhujumu uchumi linamalizika kabisa katika visiwa vya Zanzibar. Hivyo wadau wamependekeza kufanyika kwa marekebisho katika maeneo ya kisheria kama ifuatavyo:

### 4.2 Maoni ya kisheria

#### 1. Uwezo wa Mahkama kusikiliza makosa ya rushwa na uhujumu uchumi

Wadau wameeleza kwamba sheria ya sasa inaitambua Mahkama Kuu pekee katika usikilizwaji wa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi, hali inayoipa mzigo mkubwa Mahkama Kuu na kupelekea kutokuzingatiwa kwa taratibu za sheria katika uwezo wa Mahkama zilizopo nchini. Utaratibu wa Mahkama umeweka mashauri na kesi kusikilizwa kwa mujibu kwa uzito wa makosa na adhabu zake na hivyo kila Mahkama inazingatia utaratibu huo. Imependekezwa makosa yanayohusiana na rushwa yashushwe katika ngazi ya Mahkama za Wilaya na Mikoa na makosa ya uhujumu uchumi yaanzie Mahkama Kuu.

## 2. Adhabu za makosa ya rushwa

Imeelezwa kwamba ikilinganishwa makosa yaliyomo katika sheria na adhabu zilizowekwa hazilingani, adhabu nyingi ni ndogo ikilinganishwa na uzito wa makosa, hali hii inaifanya Mamlaka na Ofisi ya DPP kutumia sheria nyengine kama Sheria ya Makosa ya Jinai, Sheria na Mwenendo wa Makosa ya Jinai, sheria ya Kupambana na Madawa ya Kulevya n.k ambazo zimetoa adhabu kubwa kwa makosa kama hayo na yanayolingana.

Hivyo wadau wamependekeza kuwekwe wazi msingi wa makosa na adhabu zake kwa kuainisha makosa yote pamoja na kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo hayakutajwa lakini yana mnasaba na rushwa na uhujumu uchumi. Makosa yanayohusiana na madawa ya kulevya, makosa ya utakatishaji wa fedha haramu, adhabu zake ndogo.

Vile vile wadau wamezidi kufafanua kuwa adhabu zilizoorodheshwa katika Sheria hiyo dhidi ya makosa hayo haziendi sambamba na adhabu dhidi ya makosa hayo hayo zilizomo katika sheria nyengine. Hivyo wadau wanapendekeza kuwa adhabu kwa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi ziwe kali sana na ziende sambamba na adhabu zilizomo katika sheria nyengine kwa yale makosa yanayofanana.

## 3. Mamlaka ya DPP katika makosa ya rushwa

Wadau wameeleza kwamba uwezo wa kuendesha makosa yanayohusiana na rushwa na uhujumu uchumi yapo kwa DPP, ni vyema DPP akakasimu madaraka yake kama inavyofanywa katika Mamlaka nyengine zinazopinga masuala ya rushwa na uhujumu ili kaiz hiyo ifanywe kw awepesi na ufanisi

zaidi, kwa kuzingatia mgawanyo wa madaraka na kutokuwepo kwa mgongano wa maslahi katika usimamizi wa makosa hayo. Imependekezwa kuwekwe wazi mipaka na mamlaka ya maafisa wa ZAECA na DPP hasa katika ukamataji, uzuiaji wa watuhumiwa na ukaguzi.

Aidha wadau wamependekeza ili kuwa na mwendelezo mzuri wa kupambana na makosa ya uhujumu uchumi na rushwa, utaratibu wa kuchukua maelezo kwa maafisa wa ZAECA utambuliwe chini ya Sheria ya Ushahidi Nam. 9 ya mwaka 2016 badala ya kutambua maafisa wa jeshi la polisi pekee.

## 4. Tafsiri za maneno

Wadau wanaeleza kuwa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar imeshindwa kutoa tafsiri ya baadhi ya maneno ambayo kutokana na umuhimu wa maneno hayo pamoja na matumizi yake katika Sheria hii ni vyema yakapatiwa ufafanuzi ili kuleta uelewa zaidi kwa watumiaji wa Sheria hii. Miongoni mwa maneno hayo ambayo yanahitaji tafsiri ya kina ni pamoja na neno 'rushwa, uhujumu uchumi, makosa yote ya rushwa na uhujumu uchumi' na neno 'mazungumzo' ambalo limeekewa utaratibu maalum kwa la usuluhishi.

Hivyo wadau wa Sheria hii wanapendekeza kuwa maneno hayo yaliyoorodheshwa hapo juu yapatiwe tafsiri ili kuleta ufanisi mzuri wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Zanzibar katika jamii ya Wazanzibari. Imependekezwa kuwekwa ufafanuzi mzuri wa tafsiri ya rushwa, aina za rushwa, ufafanuzi mzuri wa kifungu cha 36, 42,52,58, 53, 15(b), 43. Wadau

wamependekeza Rushwa ya ngono ielezewe kwa uwazi na hasa katika maeneo ya ajira, kazi, upandishwaji wa vyeo, uchaguzi n.k.

**5. Kulindwa watoa taarifa**

Wadau wameeleza kwamba kuna haja ya kulindwa watoa taarifa kwa kuweka utaratibu mzuri wa kuwaficha wasitambulike, kuwazawadia, kutokuwalazimisha kuwepo Mahkamani ili kutoa taarifa zaidi inapobidi na kuhakikisha utaratibu wa kupokea taarifa zao haubaki katika kumbukumbu yoyote kwa usalama wao.

**6. Kupatiwa kinga maafisa wa ZAECA**

Imependekezwa sheria itoe ulinzi mzuri kwa maafisa wa ZAECA kutokana na kazi ngumu na kubwa wanayoifanya. Makosa yanayofanywa kwa nia njema yafahamike na walindwe kutokana na makosa hayo. Uzoefu unaonesha kwamba kwakuwa maafisa hawa wanashughulikia kesi nzito za uhujumu uchumi na watuhumiwa wengi hawapo tayari kutiwa hatiani, hukumbana na vikwazo vingi, mitego na fitna mbalimbali katika kutekeleza majukumu yao.

**7. Utaratibu wa kutaifisha mali za wanaohujumu uchumi**

Wadau wanapendekeza kuwa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ioneshe wazi kuwa ni mamlaka gani yenye uwezo wa kutaifisha mali ambayo inatokana na chumo la rushwa au uhujumu uchumi. Aidha Sheria hii inatakiwa kueleza kuwa ni chombo au taasisi gani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa na mamlaka ya kisheria ya kusimamia mali hiyo iliyotaifishwa.

Wadau wamependekeza kuwekwe utaratibu wa kutaifisha mali za wanaohujumu uchumi na makossa ya rushwa, sheria iweke wazi utaratibu wa

(a) kukamata mali,
(b) kutaifisha
(c) uhifadhi wa mali zinazoweza kuharibika na zisizoharibika (perishable and non-perishable)

**8. Kutangazwa wanaohusika na makosa ya rushwa**

Wadau wameeleza kwamba ZAECA imekuwa ikiwatangaza wanaohusika na makosa ya rushwa bila kujiridhisha au kumaliza uchunguzi wao, hali inayoleta athari kwa jamii na walengwa ambao mara nyingi hujiona kuwa wamechafuliwa na kutokutendewa haki katika jamii.

Imependekeza kuwe na utaratibu maalum na vigezo vya kuwataja au kuwatangaza wanaojihusisha na masuala ya rushwa na uhujumu uchumi, ikiwemo kujiridhisha na kuwepo kwa hatua zilizoanza kuchukuliwa, iwapo ZAECA itafanya makossa katika utangazaji huo iwe tayari kuwasafisha watuhumiwa n.k.

**9. Kuwepo kwa utaratibu wa makubaliano ya kumaliza makosa (plea bargaining)**

Wadau wamependekeza kuwe na utaratibu wa mapatano ya watuhumiwa wa makosa ya kuhujumu uchumi katika kukubali makosa na namna ya kulipa kutokana na makosa hayo ili Serikali iweze kufidia kiasi au kiwango cha mali iliyohujumiwa na mtuhumiwa (plea bargaining).

Imependekezwa utaratibu huu uwe kwa makosa maalum na utungiwe kanuni za taratibu za kufuata na uthibitisho wa makosa yanayohitaji kuwa chini ya mapatano, mfumo wa kusikiliza makosa ya aina hii, na uwekaji wa kumbukumbu za maamuzi na nguvu ya maamuzi kwa wanaotuhumiwa.

## 10. Kuwepo kanuni za Maadili (code of conduct)

Imependekezwa kuwekwe utaratibu wa maadili ya watendaji wa ZAECA ili wafanyakazi hao wabanwe na maadili ya msingi. Imependekezwa watendaji wa ZAECA wawe na uweledi, ujasiri, uaminifu, maadili na utaalamu wa kusimamia makosa ya rushwa na uhujumu uchumi, na taratibu za kuwapima kiutendaji zifanyike kila baada ya muda.

## 11. Uhusiano wa Sheria ya ZAECA na Sheria nyengine

Wadau wamependekeza kuwepo uhusiano mzuri baina ya Makosa yaliyomo katika sheria ya ZAECA na sheria nyengine kama vile maeneo ya magendo, sheria za forodha, Sheria ya manunuzi, sheria za uwekezaji na nyengine ziangaliwe tena ili kuwezesha sheria ya ZAECA kufanyakazi vizuri zaidi.

## 12. Sheria kutambua kosa la rushwa ya ngono

Wadau wameeleza kuwa baadhi ya wanajamii ambao hufuata huduma katika taasisi za umma na taasisi binafsi huombwa kufanya ngono na baadhi ya watu waliopewa dhamana na mamlaka katika taasisi hizo kwa sharti la kupata huduma hizo. Kutokana na udhaifu wa baadhi ya wanajamii hao na kutokana na umuhimu wa huduma hizo kwao, hujikuta kukubali kufanya ngono ili kupata huduma. Vile vile katika ngazi za uawaji, muomba ajira huombwa na mwajiri kushiriki kufanya ngono ili ampatie ajira.

Hivyo wadau wanapendekeza kuwa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar itambue kosa la rushwa ya ngono na kuweka adhabu kali kwa wale wote watakaoshiriki katika rushwa ya namna hiyo.

### 13. Sheria kutambua makosa yanayojitegemea

Katika kipengele hiki wadau wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi wametoa maoni kuwa Sheria hii inahitaji kubagua baadhi ya makosa na kuyaweka huru pasi na kufungamanisha makosa hayo na makosa mengine kwani makosa hayo yanajitegemea wenyewe. Hapa wadau wanapendekeza kuwa Sheria itambue kuwa suala la kufanya maamuzi kwa upendeleo, urafiki au kujuana (nepotism) katika taasisi kuwa ni miongoni mwa makosa ya rushwa na kuwekwe adhabu kali kwa wale wote watakaojihusha na makosa hayo.

## 4.3 Maoni ya Kimfumo na Kiutendaji

### 1. Muundo wa Taasisi

Miongoni mwa maoni ya wadau ni kwamba ndani ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kuundwe kitengo maalum ambacho kitakuwa na watendaji ambao watashughulika na mashtaka ya rushwa na uhujumu uchumi pekee. Jukumu la msingi la watendaji hawa ni kushugulikia mashauri ya rushwa na uhujumu uchumi mahakamani na hawatopaswa kujihusisha na kazi nyengine za Mamlaka kama vile masuala ya uchunguzi na upelelezi.

Imependekezwa kwamba ZAECA iongozwe na Bodi ya Wakurugenzi, na sifa za Mkurugenzi Mkuu ziwekwe wazi na zisijumuishe utaalamu wa sheria pekee.

Aidha imependekezwa usafi wa kimaadili wa wakuu hao (intergrity) na maadili viwe vigezo vya msingi katika kusimamia taasisi hii.

Wadau wameeleza kwamba watendaji wa ZAECA wajumuishe wataalamu kutoka taasisi mbalimbali ambao watakuwa utaalamu na sifa za kupambana, kuchunguza, kukamata, kukusanya taarifa, kuendesha makosa ya rushwa na uhujumu uchumi. Wadau wamependekeza kuwa katika jitihada za kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi katika maeneo mbali mbali ya visiwa vya Zanzibar, kuanzishwe Ofisi za Mamlaka ya kuzuia rushwa na uhujumu uchumi kwa ngazi zote za Wilaya na Mikoa. Kwani kuwepo kwa Ofisi za Mamlaka katika ngazi hizo kutasaidia Mamlaka hiyo kutanua wigo wake na kuunda namna bora zaidi za udhibiti wa rushwa na uhujumu uchumi kwa kuongeza nguvu kazi katika utendaji wake na kutapelekea kuifikia jamii na tasisi mbali mbali zilizopo katika ngazi hizo kwa urahisi.

### 2. ZAECA iwe Taasisi huru

Wadau wamependekeza kwamba ZAECA ipewe uhuru zaidi, na iwe taasisi ambayo ina mamlaka ya kusimamia masuala yanayohusu uhujumu uchumi na kupambana na rushwa, kutokana na misingi ya utawala Boara taasisi kama hizi huwa haziingiliwi na zinafanyakazi kwa uhuru na haki. Kwa makosa yanayohusu Serikali au maafisa wakuu taasisi hii ie huru bila vitisho kusimamia makossa haya kwa kuzingatia nguvu walizonazo kisheria.

### 3. Utaratibu wa kutoa taarifa kwa wanachi

Wadau wametoa masikitiko yao juu ya kukosekana kwa utaratibu maalum wa kuwapatia taarifa wananchi kuhusiana na makosa ya rushwa hasa yale

yanayotangazwa vyema kutolewe taarifa za mwendelezo na hatua zaidi zilizochukuliwa ili wananchi wafahamu na kuwa funzo kwa wengine. Imeelezwa kwamba taarifa nyingi ambazo wananchi wanapaswa kuzifahamu zinafichwa na haziwekwi wazi hali inayowapa khofu kutoa taarifa nyengine ambazo wanahisi hazitafanyiwa kazi.

**4. Uhusiano wa ZAECA na taasisi nyengine**

Wadau wamependekeza kuwepo uhusiano mzuri baina ya ZAECA na taasisi nyengine, ikiwemo ufanyaji kazi kwa karibu na Jeshi la Polisi, maafisa usalama, taasisi zinazokusanywa taarifa zinazosaidia kuibua makosa ya rushwa na uhujumu uchumi kama vile Ofisi ya CAD, Maadili, Mamlaka ya Manunuzi n.k. Imependekezwa ZAECA ikasimu baadhi ya madaraka inapobidi kwa Jeshi la Polisi, wataalam wa TEHAMA, KMKM na Idara Maalum ili zisaidie katika kupambana na makosa ya rushwa na uhujumu uchumi.

**5. Uwezo wa Mamlaka**

Wadau wametoa maoni kuwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, katika kutekeleza majukumu yake, ipewe uwezo wa kuendesha mashtaka kwa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi si kwa makosa ambayo yanahitaji ridhaa kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma bali hata kwa makosa yasiyohitaji ridhaa hiyo.

Vile vile Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, katika kufanya uchunguzi wa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi, ipewe uwezo wa kushirikiana na taasisi mbali mbali zikiwemo taasisi za Serikali na taasisi binafsi hasa mitandao ya simu iliyopo nchini kwani mitandano hiyo haitoi

ushirikiano wa kutosha kwa Mamlaka pale Mamalaka inapoomba taarifa za mawasiliano za watuhumiwa wa makosa hayo kwa ajili ya uchunguzi na ushahidi.

Aidha wadau wanapendekeza kuwa katika kuleta ufanisi katika kazi zao za kila siku Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar wapewe mamlaka kisheria ya kuwatumia wataalamu hasa katika makosa ya uhujumu uchumi kwani makosa ya namna hiyo yanahitaji utaalumu mkubwa.

**6. Kuimairishwa kwa ulinzi kwa baadhi ya maafisa wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar**

Wadau wa Sheria hii wameeleza kuwa miongoni mwa changamoto kubwa inayowakabili maafisa wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ni pamoja na kutokuwa na ulinzi wa kutosha pale wanapokuwa katika shughuli zao za uchunguzi na ukamataji wa watu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Baadhi ya watu hao hutumia nguvu na silaha na hukataa katakata kutii maamrisho ya maafisa wa Mamlaka hali ambayo inawapa uzito na ugumu maafisa hao kukabiliana nao na hupelekea kushindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**7. Kuongezewa Rasilimali Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi**

Katika suala hili wadau wanapendekeza kuwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi iingiziwe rasilimali ya fedha za kutosha kwani kufanya hivyo kutaiwezesha Mamlaka hiyo kufanya shughuli zake kwa uweledi na kwa wakati uliokusudiwa. Mamlaka inashindwa kutekeleza majukumu yake ya

msingi kutokana na kutegemea fedha ambazo zinaidhishwa na Baraza la Wawakilishi pekee.

Aidha wadau wanapendekeza kuwa katika mali ambazo zinataifishwa, itolewe asilimia kadhaa ambayo itaingizwa katika mfuko wa Mamlaka ili kusaidia shunguli mbali mbali za tasisi hiyo. Vile vile wadau wanapendekeza kuwa fedha za mitego zisiwe zinaingizwa katika Fedha za Matumizi ya Kawaida (O.C) ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi bali ziundiwe utaratibu wake maalum.

**8. Kuchukua hatua za kuzuia Rushwa isitokee**

Mamlaka ya kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi imekua ikifanya kazi kubwa ya kuchunguza na kuchukua hatua baada ya rushwa kutokea hivyo, Wadau walipendekeza Sheria iweke vifungu zaidi vya kudhibiti na kukinga rushwa isitokee na sio kusubiri mpaka rushwa itokee na Mamlaka kuanza kuchunguza.

**9. Kuwekwa kwa utaratibu mzuri wa kusimamia mikataba ya manunuzi**

Wadau wanaeleza kuwa miongoni mwa miyanya mikubwa ya kutokea vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi katika masuala ya manunuzi ya vifaa mbali mbali katika taasisi za umma ni ukosefu wa utaratibu dhibiti wa usimamizi wa mikataba ya manunuzi, walipendekeza kuwepo na utaratibu mzuri utakaosimamia mikataba ya manunuzi pamoja na kuweka sawa mikataba iliyotajwa katika Sheria ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali kwani haikidhi haja kwa hivi sasa.

**10. Kuwekwe bei elekezi kwa vifaa vyote vinavyonunuliwa na Serikali**

Kukosekana kwa bei elekezi kunapelekea mianya ya rushwa kwa wanunuzi wa vifaa vya Serikali kwani imeonekana kuwa bei za manunuzi haziendani na uhalisia wa bei za vifaa viliopo madukani. Hivyo, wadau wanapendekeza kuwepo kwa bei elekezi ambayo itapelekea kuwa na bei maalumu za kila kifaa kitakachonunuliwa na Serikali.

**11. Kutolewa Elimu**

Wadau wamesisitiza kutolewa elimu kwa wananchi na watendaji wa Serikali ili kufahamu makosa ya rushwa na uhujumu uchumi, uwajibikaji wao, adhabu zilizopo, utaratibu wa kuwasilisha matukio ya rushwa, uhifadhi wa taarifa zinazotolewa kwa watendaji wa Serikali,

Imependekezwa suala la rushwa liingizwe katika mitaala ya skuli za msingi ili kuonesha athari ya rushwa na uhujumu uchumi katika hatua za awali katika jamii. Aidha kuna haja ya kuimarishwa vituo vya utoaji wa elimu vilivyopo pamoja na kutumia vyombo vya habari na Asasi za Kiraia kutangaza jinsi ya kupambana na matukio ya rushwa na uhujumu uchumi katika matukio mbalimbali ikiwemo ajira na kipindi cha ukaguzi.

Miongoni mwa jambo ambalo limechangiwa sana na wadau wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ni pamoja na kutolewa taalum juu ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi pamoja na athari zake katika jamii. Wadau wanafafanua kwa kueleza kuwa Wazanzibari walio wengi hawana uelewa wa vitendo mbali mbali vya rushwa kwani miongoni mwao hufanya baadhi ya vitendo hivyo  kama ni ada au mazoea pasi na kujua kuwa

ni makosa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar.

Hivyo wadau wanapendekeza kuwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kupitia watendaji wake au kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia wazifikie jamii za Wazanzibari ili kuwapa taaluma ya kutosha kuhusiana na athari za rushwa na uhujumu uchumi nchini pamoja na vitendo mbali mbali ambavyo kwa mujibu wa Sheria ni kosa kwani kufanya hivyo kutasaidia jamii hizo kuwa na uelewa wa kutosha na hatimae kupelekea kudhibiti ipasavyo vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi nchini.

## SURA YA TANO

## 5.0 MIKATABA YA KIMATAIFA NA SHERIA ZA NCHI MBALI MBALI

### 5.1 Utangulizi

Tanzania imetia saini na mshirika wa vyombo vya kimataifa vinavyotaka kukabiliana na ufisadi, vikiwemo Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa (UNCAC) na Umoja wa Afrika Mkataba wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Mkataba wa AU). Mikataba hii kuzitaka nchi zote wanachama zilizotia saini kuweka utaratibu wa kushughulikia rushwa na kuimarisha taasisi zinazohusika na kuzuia na kupambana na rushwa. Tanzania ni pia mwanachama wa mashirika mbalimbali ya kupambana na rushwa.

Tanzania ilitia saini na kuridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa (UNCAC) na Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (AUCPCC) mwaka 2007.[104]

### 5.2 Mikataba ya Kimataifa

Madhara ya rushwa yameanza kufanyiwa tafiti kimataifa hasa baada ya mwaka 1995 ambapo Mataifa mbali mbali pamoja na Jumuiya za Kimataifa na Kikanda zimeanza kufanya jitihada zake juu ya kuzuia rushwa na madhara yake.[105]

[104] Andreoni, A. 2017. Anti-Corruption in Tanzania: A Political Settlements Analysis. SOAS, University of London. https://eprints.soas.ac.uk/24853/1/ACEWorkingPaper001-TZ-AntiCorruption171102_final%20revised.pdf

[105] Stefan Sumah, corruption, causes and consequences, open access pear- reviewed chapter inapatikana https://www.intechopen.com/chapters/58969

Jumuiya za Kimataifa zimetambua kuwa rushwa ndio sababu kuu inayopelekea kuharibu ufanisi wa kiutendaji katika jamii, inazuia ukuaji wa uchumi, inaondoa utawala wa kisheria pamoja na kuhatarishia demokrasia ya nchi. Hivyo, Jumuiya hizi za Kimataifa zinaendelea kuweka mikakati pamoja na kuchukua jitihada maalumu kwa ajili ya kupambana na rushwa kwa kushirikiana kwa pamoja kwa lengo la kuondosha au kupunguza tatizo la rushwa katika jamii.[106] Jumuiya za Kimataifa katika kufikisha lengo la kupandana na rushwa; Mikataba mbali mbali imeridhiwa na Mataifa mengi duniani ikiwemo:

1. **Mkataba wa IACAC**

Mkataba wa mwanzo wa Kimataifa wa kupambana na kuzuia Rushwa ulikuwa ni Mkataba wa Nchi za Marekani (IACAC) wa mwaka 1997. Ambapo mwaka 1996 wanachama wote 34 wa Jumuiya hiyo walikubali na kuipitisha mkataba huo na kuanza kutumika rasmi 1997 jambo ambalo ndilo lililoanzisha mapambano dhidi ya rushwa kimataifa.[107]

2. **Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Rushwa**

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kupambana na Rushwa wa mwaka 2004.[108] Malengo makuu ya mkataba huu ni kuweka mikakati bora ya kuzuia na kupambana na rushwa. Kuzisaidia Jumuia za Kimataifa kwa kuzipatia nyenzo bora za kupambana na rushwa pamoja na kuweka uadilifu, uwajibikaji na usimamizi mzuri wa utumiaji wa mali za umma.[109] Aidha, Mkataba huu

[106] ibid
[107] https://www.oas.org/en/sla/dil/inter_american_treaties_b-58_against_corruption.asp
[108] Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Rushwa inapatikana katika tovuti http://www.unodc.org/pdf/crime/convention_corruption/signing/Convention-e.pdf
[109] Kifungu cha 1 cha Mkataba wa Umoja wa MAtaifa wa Kupambana na Rushwa wa mwaka 2004

umeweka hatua muhimu za kuchukuliwa na nchi wanachama juu ya kudhibiti vitendo vya rushwa pamoja na kuweka sheria na adhabu kwa watakaopatikana na hatia za vitendo vya rushwa katika Sura ya II na III za Mkataba huo.

### 3. Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa

Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa ulipitishwa mjini Maputo Msumbiji, mnamo Julai 2003, na kuanza kufanya kazi tarehe 5 Agosti 2006.[110]

Lengo kuu la Mkataba huu ni kupambana na rushwa ya kisiasa iliyokithiri katika bara la Afrika. Aidha, mkataba huu umeweka makubaliano ya kikanda kwa nchi wanachama wa Umoja wa Afrika juu ya njia za mashirikiano kwa nchi hizo katika mapambano dhidi ya rushwa ikiwemo ushirikiano wa kimataifa na uokoaji wa mali, kupambana dhidi ya uhalifu. Vile vile mkataba huu umeainisha makosa mbali mbali yakiwemo makosa ya utakatishaji wa fedha haramu na ufichaji wa mali.

## 5.3 Mikataba ya Kisekta

Mbali ya mikataba hiyo mikubwa pia ipo mikataba iliyofikiwa na Umoja wa Mataifa katika sekta maalumu kama vile:

### 1. Itifaki ya SADC dhidi ya Rushwa

Wanachama wa Jumuiya ya SADC walifikia makubaliano ya kuanzisha Itifaki ya SADC dhidi ya rushwa mnamo Agosti, 2001 katika mji wa Blantyre Malawi.

---

[110] Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa unapatikana http://www.africa-union.org/official documents/Treaties-Conventions-Protocols/Convention on Combating Corruption.pdf

Mkataba huu ulikua ni wa mwanzo na wa aina yake katika ukanda huu wa Kusini mwa Afrika.[111]

Kuanzishwa kwa Itifiki ya SADC imetokana na msisitizo uliotolewa na secretariat ya SADC kwa kusisitiza nchi wanachama wa Jumuiya hiyo kuchukua hatua madhubuti za kupambana na rushwa baada ya kutambua kuwa rushwa imekuwa ni tatizo la dunia nzima.[112]

**2. Shirikisho la Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa Afrika Mashariki (EAAACA)**

Jumuiya ya Afrika Mashariki iliunda Shirikisho la Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa Afrika Mashariki. Shirikisho hili liliundwa tarehe 28 Septemba, 2007 Kampala Uganda na kuzinduliwa rasmi tarehe 9 Novemba, 2007 Nairobi, Kenya. Shirikisho hili lilianzishwa na mamlaka tatu za kupambana na rushwa ambazo ni TAKUKURU (Tanzania), IG (Uganda) na KACC (Kenya) Wakati wa uanzishaji wa shirikisho viongozi wa mamalaka hizi walisaini azimio la kuwa na Ushirikiano wa Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa Afrika Mashariki. Azimio hilo lilipewa jina la 'AZIMIO LA KAMPALA'.[113]

Uanachama katika shirikisho uko wazi kwa Mamlaka zote za Kupambana na Rushwa zilizoko kwenye Jumuia ya Afrika Mashariki na nchi zingine za Afrika Mashariki. Pia milango iko wazi kwa Taasisi zingine zenye malengo yanayofanana na EAAACA kuwa watazamaji baada ya kuomba na kukubaliwa

[111] https://www.sadc.int/files/7913/5292/8361/Protocol_Against_Corruption2001.pdf
[112] Imeelezewa zaidi katika https://www.pccb.go.tz/index.php/en/kimataifa/99-umoja-wa-afrika
[113] https://eaaaca.com/about-eaaaca

uanachama na kamati tendaji ya EAAACA. Kwa hivi sasa Shirikisho hili lina wanachama 8.[114]

3. **Kituo cha Kupambana na Rushwa cha nchi za Jumuiya ya Madola Afrika (CAACC)**

Kituo cha kupambana na rushwa cha nchi za Jumuia ya Madola Afrika kiko Gaborone Botswana. Kituo hiki kilianzishwa na Sekeritariati ya Jumuia ya Madola kwa ushiririkiano na Serikali ya Botswana na Umoja wa Mamlaka za Kupambana na Rushwa wa Jumuia ya Madola Afrika mwezi Februari 2013[115]. Ni taasisi isiyo na nia ya kupata faida katika shughuli zake. Kituo hicho hutoa mafunzo,uendelelezaji na kubadilishana uzoefu katika masuala ya uchunguzi, utafiti, elimu kwa umma, kuzuia, uchunguzi wa kitaalam, uongozi na utawala, maadili ya kazi, uendeshaji wa mashtaka, ufuatiliaji wa mali, ufuatiliaji na tathimini ya shughuli za mapambano dhidi ya rushwa, mipango ya kitaalamu pamoja na kujenga uwezo wa kimaendeleo katika kupambana na rushwa kwa nchi wanachama na maofisa.

Kituo kimefanya kazi na mashirika kama vile UNDP, Transparency International na shirika la umoja wa mataifa, ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia madawa ya kulevya na uhalifu (UNODC). Kwa msaada wa shirika la kimataifa la uwazi kwa mfano, kituo kimeanzisha dawati la msaada ili kuzisaidia taasisi wanachama wa kupambana na rushwa huduma ya kitalaam na utafiti kwa haraka.[116]

---

[114] ibid
[115] https://www.thecaacc.org/
[116] https://www.thecaacc.org/about-us/

## 5.4 Vyombo muhimu vinavyohusika na utekelezaji wa Mikataba:

Katika kusimamia na kutekeleza mikataba ilyowekwa ya kimataifa vimepelekea kuundwa kwa vyombo mbalimbali kwa ajili ya usimamizi wa utekelezaji wa mikataba hiyo kwa nchi wanachama.

### 1. Bodi ya Ushauri ya Masuala ya Rushwa ndani ya AU:

Umoja wa Afrika umeweka utaratibu maalumu wa kutekeleza majukumu yatokanayo na mkataba wa AU wa kuzuia na kupambana na rushwa kwa kuweka mfumo wa ufuatiliaji na usimamizi wa mkataba huu kwa kupitia Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ndani ya AU iliyoundwa May 2009 chini ya kifungu cha 22(1) cha Mkataba wa AU wa kupambana na rushwa. Bodi hii ina wajumbe 11 ambao huteuliwa na Baraza la Utendaji la AU kutokana na mapendekezo ya nchi wanachama wa AU.[117]

### 2. Jukwaa la Kupambana na Rushwa kwa Nchi za Kusini mwa Afrika (The Southern Afrika Forum against Corruption (SAFAC)

SAFAC ni mtandao wa taasisi za kupambana na rushwa katika nchi wanachama wa SADC. SAFAC ilianzishwa kufuatia uamuzi wa watunga sera wa SADC walioazimia kuundwe mtandandao wa taasisi za kupambana na rushwa katika kanda hii ili uwe chombo cha ushirikiano katika mapambano dhidi ya rushwa, makosa ya uhujumu uchumi na makosa mengine yenye kufanana nayo. Taasisi hii ilianzishwa Gaborone, Botswana mwaka wa 2000 na kuzinduliwa rasmi Julai 2001 Maseru Lesotho.

117 https://anticorruption.au.int/en/about

Lengo kuu la SAFAC ni kuwezesha ushirikiano wa kikanda katika mapambano dhidi ya rushwa na kutoa fursa kukutana na kubadilishana uzoefu na namna nzuri ya kufanya kazi baina ya taasisi za kupambana na rushwa katika ukanda wa SADC.[118] Malengo yote ya Foramu hii yameoneshwa katika kifungu cha 5 cha Katiba ya SAFAC.

### 3. Ushirika wa Kimataifa wa Mamlaka za Kupambana na Rushwa (IAACA)

Shirikisho huru la Kimataifa la Mamlaka mbalimbali za kupambana na Rushwa IAACA liliundwa kwa lengo la kuhimiza utekelezaji wa mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya rushwa (UNCAC) pamoja na kusaidia mamlaka za kupambana na rushwa duniani katika kupambana na rushwa. Shirikisho hilo sio la kiSerikali na wala halifuati mlengo wowote wa kisiasa na lisilo na nia ya kupata faida lilianzishwa rasmi Oktoba 22, 2006 , Beijing nchini China.[119]

IAACA imeweza kuleta mafanikio kwa kuendeleza mbele mashirikiano ya kimataifa ya vita dhidi ya rushwa pamoja na kutoa msukumo mkubwa kwa nchi wananchama kusimamia Mkataba wa Umaoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa. Shirikisho hili linazaidi ya nchi wanachama 140 kwa kupitia taasisi zao za mamlaka za kupambana na rushwa, mahakama na mamlaka za kusimamia sheria na mashirika ya kupambana na rushwa.

[118] Dk. Edward G. Hoseah, The Southern African Forum Against Corruption inapatikana https://www.igg.go.ug/media/files/publications/SAFAC_Presentation_Bujumbura__by_Dr_Hoseah.pdf
[119] https://www.iaaca.net/

### 4. Mashirikiano baina ya AU na UN katika vita dhidi ya Rushwa

Umoja wa Mataifa umekua ukishirikiana na tume za kitaifa za kutokomeza rushwa ili kumaliza ukwepaji sheria na wahusika kufikishwa mbele ya sheria. Hivyo, Umoja wa Mataifa umekuwa ukishirikiana na Umoja wa Nchi za Afrika kwa karibu katika kupambana na rushwa barani Afrika. Katika Mkutano wa Kawaida wa 30 wa Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia, Katibu Mkuu Umoja wa Mataifa alisisitiza umuhimu wa Jumuiya mbili hizi kuzidisha mashirikiano yako katika kupambana na vitendo vya rushwa.

Mashirikiano hayo yanaweza kumaliza tatizo la rushwa na kuhakikisha kila fedha ya umma na uwekezaji vinaelekezwa pale ambako vinahitajika zaidi na wananchi.[120] Kwa kuwa Bara la Afrika imetangaza kuwa mwaka 2018 ni mwaka wa kupiga vita rushwa Barani Afrika hoja ambayo ilipokelewa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa na kuahidi UN kushirikiana na AU ili ifikie malengo yake.

### 5. Mkutano wa Kimataifa wa Kupambana na Rushwa

Mkutano wa siku mbili wa Wakuu wa Nchi za Umoja wa Afrika walikutana Mauritania mnamo mwaka 2018. Zaidi ya Marais na Viongozi wa Serikali kutoka nchi 40. Lengo kuu la Mkutano huo ni kutafuta njia za kumaliza tatizo la rushwa ili nchi za Kiafrika ziweze kufikia maendeleo ya kiuchumi.

---

[120] https://news.un.org/sw/story/2018/01/1002611

## 6. Mkataba wa OECD wa Kupambana na Ufisadi wa Maafisa wa Kigeni na wa Umma katika Miamala ya Biashara ya Kimataifa

Umoja wa Mataifa umeongoza juhudi za kuzuia rushwa ya kimataifa. Kwa muda mrefu imeonekana kuwa hongo haiendani na maadili ya kidemokrasia, kama vile utawala bora na utawala wa sheria. Pia ni kinyume na msingi na kanuni za ushindani wa haki na hatari kwa juhudi za kukuza maendeleo ya kiuchumi.[121] Mkataba wa OECD - ambao unawakilisha kilele cha miaka mingi ya juhudi endelevu za kidiplomasia umewekwa ili kuleta mabadiliko.[122]

## 5.5 SHERIA NA UZOEFU WA NCHI MBALI MBALI

### 1. RWANDA

#### (a) Sheria ya Kupambana na Rushwa Rwanda Nam. 54 ya 2018

Katika kudhibiti na kupambana na vitendo vya rushwa, Serikali ya Rwanda imetunga sheria maalum ya kupambana na vitendo hivyo inayojulikana kama ni Sheria ya Kupambana na Rushwa Nam. 54 ya 2018. Sheria hii imetoa miongozo mbali mbali ya udhibiti wa vitendo vya rushwa na kubainisha makosa ya rushwa na adhabu zake ikiwa ni jitihada madhubuti ya kupambana na vitendo hivyo nchini humo. Miongoni mwa jitihada hizo ni pamoja na:

#### (b) Wajibu wa vyombo vya umma na vyombo binafsi katika kuzuia rushwa.

Katika kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa, ibara ya 3 ya Sheria ya Rushwa nchini Rwanda imekitaka kila chombo cha umma, taasisi

[121] Does anti-corruption legislation work? A Keith Thompson This article was previously published in the International Trade and Business Law Review, 2013, vol. XVI, pp. 99-135, and is reprinted with the permission of the Editor-in-Chief of the Review, Professor Gabriel A Moens, and of the author., World Customs Journal, Volume 7, Number 2 43

[122] OECD, 'Information sheet on the OECD Convention on Combating Bribery of Foreign Public Officials in International Business Transactions' (November 2002), www.oecd.org/dataoecd/52/24/2406452.pdf.

binafsi, mwanajamii au jumuiya ya kimataifa inayofanya shughuli zake nchini humo kutekeleza kwa vitendo azma ya Serikali ya kuzuia vitendo vya rushwa. Vyombo hivyo vinalazimika kufanya mambo yafuatayo:

(i) kutekeleza taratibu za kuzuia rushwa;
(ii) kufanya shughuli zake kwa uwazi;
(iii) kuwasilisha ripoti kwa mamlaka husika;
(iv) kuhakikisha kwamba hakuna vitendo vya rushwa ndani ya vyombo hivyo;
(v) kuwasilisha taarifa juu ya hatua wanazozichukua katika kupambana na rushwa pale zinapohitajika na chombo chenye mamlaka;
(vi) kushirikiana na taasisi nyengine kulingana na muda unaotakiwa wakati wa kuwasilisha shughuli zinazofanywa au kutoa taarifa yoyote inayoombwa na taasisi nyengine; na
(vii) kuhakikisha huduma sawa kwa wateja na utoaji wa huduma kwa wakati.

**(c) Ukali wa adhabu kwa kosa la kuomba au kupokea faida isiyo halali kwa mtu anaetoa au kutekeleza maamuzi ya kisheria**

Sheria ya kupambana na rushwa nchini Rwanda imetoa adhabu kali kwa watoaji au watekelezaji wa maamuzi ya kisheria wakiwemo majaji/mahakimu au wasuluhishi wa migogoro mbali mbali inayoibuka katika jamii pale wanapojiingiza katika makosa ya kuomba au kupokea faida isiyo halali wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kisheria. Sheria imebainisha wazi kuwa kufanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa ibara ya 5 ya Sheria ya Kupambana na Rushwa na wakitiwa hatiani watatumikia kifungo kisichopungua miaka kumi

(10) na kisichozidi miaka kumi na mbili (12) pamoja na kulipa faini ya fedha za Rwanda mara tatu (3) mpaka tano (5) ya faida isiyo halali iliyoombwa.

**(d) Kosa la kufanya maamuzi kwa upendeleo, urafiki, chuki au kujuana**

Serikali ya Rwanda kupitia sheria yake ya kupambana na vitendo vya rushwa imekemea vikali tabia za baadhi ya watumishi wa umma na watumishi binafsi kufanya maamuzi kwa upendeleo, urafiki, chuki au kujuana katika vyombo vya umma na vyombo binafsi.

Ibara ya 8 ya Sheria hii imeeleza kuwa endapo mtu atatiwa hatiani kwa makosa yaliyotajwa hapo juu atatumikia kifungo cha zaidi ya miaka mitano (5) na kisichozidi miaka saba (7) pamoja na faini isiyopungua milioni moja ya fedha za Rwanda na isiyozidi milioni mbili.

**(e) Makosa ya ubadhirifu na kujipatia utajiri haramu**

Miongoni mwa makosa makubwa ya rushwa chini ya Sheria ya Kupambana na Rushwa ya Rwanda ni pamoja na kutumia madaraka kwa kujitajirisha kupitia njia zisizo halali kinyume na kipato halali kinachotokana na malipo ya mshahara, na kufanya ubadhirifu.

Katika ibara ya 9 ya Sheria ya Kupambana na Rushwa imeelezwa kuwa mtu yoyote ambaye atashindwa kuthibitisha vyanzo vya mali zake kwa mujibu wa kipato chake halali, anafanya kosa. Na akitiwa hatiani, atatumikia kifungo cha muda usiopungua miaka saba (7) lakini hauzidi miaka kumi (10) pamoja na faini ya thamani ya mali mara tatu (3) mpaka tano (5) ya chanzo ambacho ameshindwa kuthibitisha.

Aidha Sheria ya Kupambana na Rushwa ya Rwanda, katika ibara ya 10, imeeleza kuwa mtu yeyote, ikiwa ni mtumishi wa umma au wakala mwengine yeyote mwenye dhamana ya utumishi wa umma au anafanyakazi katika vyombo vya umma, afisa au mwajiriwa wa taasisi, kampuni au shirika, wakala wa mtu, jumuiya ya kidini au jumuiya nyengine yoyote ambaye anafanya ubadhirifu kwa ajili ya kujipatia mali kwa maslahi yake binafsi au maslahi ya mtu mwengine, fedha, au dhamana alizokabidhiwa kwa mujibu wa ofisi yake, au mtu yeyote anayemtumia kwa kujinufaisha yeye binafsi, mfanyakazi chini ya mamlaka yake, anafanya kosa. Na akitiwa hatiani atawajibikia kifungo cha muda usiopungua miaka saba (7) na usiozidi miaka kumi (10) na faini ya mara tatu (3) mpaka tano (5) ya thaamani sawa na thamani ya mali aliyoifanyia ubadhirifu.

**(f) Matumizi ya mali ya umma kwa dhumuni lisilokusudiwa**

Sheria ya Rwanda imetanabahisha kuwa mtumishi yeyote wa Serikali mwenye dhamana ya fedha au mali ya Serikali ya nchi hiyo anapaswa kutumia fedha au mali hizo kwa mujibu wa bajeti na makusudio yake. Kutumia fedha au mali hizo kinyume na malengo yaliyowekwa na pasipo kupewa mamlaka na chombo chenye uwezo ni kukiuka masharti ya Sheria hii.

Ibara ya 11 ya Sheria ya Kupambana na Rushwa ya nchini Rwanda imetanabahisha kuwa mtu yeyote aliyepewa mamlaka ya umma au mwenye wajibu wa kutoa huduma kwa umma ambaye anatumia fedha za bajeti ya nchi au mali nyengine ya umma kwa dhumuni ambalo halijakusudiwa na bila ya ruhusa kutoka mamlaka yenye uwezo, anafanya kosa. Na akitiwa hatiani,

atawajibikia kifungo cha muda wa zaidi ya miaka mitano (5) lakini hauzidi miaka saba (7) na faini ya fedha za Rwanda zisizopungua milioni tatu (FRW 3,000,000) na isiyozidi milioni tano (FRW 5,000,000).

### (g) Msamaha haramu

Kwa lengo la kusimamia haki na usawa wa tozo za huduma mbali mbali zinazotolewa na vyombo vya umma, Sheria ya Kupambana na Rushwa nchini Rwanda imevitaka vyombo hivyo kufuata kikamilifu masharti ya Sheria hii, sambamba na masharti ya sheria nyenginezo na kanuni mbali mbali zinazoongoza suala zima la utoaji wa tozo kwa huduma zinazotolewa.

Ibara ya 13 ya Sheria ya Kupambana na Rushwa nchini Rwanda imefafanua kuwa mwajiriwa yeyote ambaye, kwa sababu nyengine yoyote ile na bila ya kupewa mamlaka na sheria, akasamehe kwa namna yoyote, kodi, ushuru, faini au ada nyengine inayohitajika, au kutoa bila ya malipo au kwa bei ya chini mali ya umma au mali ya taasisi nyengine yoyote, anafanya kosa. Na akitiwa hatiani atawajibikia kifungo cha muda wa zaidi ya miaka mitano (5) lakini si zaidi ya miaka saba (7) na faini ya mara tatu (3) mpaka tano (5) ya thamani ya msamaha, thamani ya mali iliyotolewa bila ya malipo au kwa bei ya chini.

### (h) Makosa ya rushwa yanayofanywa na makampuni, mashirika, taasisi na jumuiya

Katika kudhibiti vitendo vya rushwa nchini Rwanda, Serikali ya nchi hiyo kupitia Sheria ya Kupambana na Rushwa imetambua ufanywaji wa vitendo hivyo kwa kampuni binafsi, mashirika, taasisi na jumuiya mbali mbali zinazotambulika kisheria. Kwa kuzingatia uovu wa vitendo hivyo pamoja na

athari zake zenye kupelekea kukosekana kwa utekelezaji bora wa haki na uadilifu katika jamii, Sheria haikulifumbia macho suala la rushwa kwa makampuni, mashirika, taasisi na jumuiya zinazoahidi au kukubali kutoa au kupokea na kuomba rushwa.

Katika ibara ya 18 ya Sheria ya Kupambana na Rushwa nchini Rwanda imeelezwa kuwa makampuni, mashirika, taasisi na jumuiya zenye utu wa kisheria zilizotiwa hatiani kwa kosa la rushwa zitawajibishwa kulipa faini ya mara saba (7) mpaka kumi (10) ya thamani ya faida isiyohalali iliyopokelewa au kukubaliwa, kuombwa, kutolewa au kuahidiwa.

Ikumbukwe kuwa Rwanda ni nchi moja wapo duniani yenye viwango vya juu vya mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa. Rwanda imeshikilia nafasi ya 49 duniani na imefanikiwa kutokomeza vitendo vya rushwa nchini humo kwa asilimia 54 wakati nchi ya Tanzania imeshikilia nafasi ya 94 duniani ikiwa imefanikiwa kutokomeza vitendo hivyo vya rushwa kwa asilimia 38 tu. Pia Rwanda ni nchi ya kwanza kufanikiwa kutokomeza rushwa katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikifuatiwa na Tanzania na nchi ya mwisho kabisa katika Jumuiya hiyo ni South Sudan ikiwa imeshikilia pia nafasi ya mwisho (179) duniani na kufanikiwa kutokomeza vitendo vya rushwa kwa asilimia 12 tu.

Wananchi wa Rwanda wameitikia wito wa Serikali ya nchi yao, kupitia Sheria ya Kupambana na Rushwa Nam. 54 ya 2018, unaomtaka kila mwananchi kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya vitendo viovu vya rushwa

akiwa mtumishi katika taasisi za Serikali, taasisi binafsi au mwananchi wa kawaida.

## 2. NEW ZEALAND

### (a) Sheria ya Uhalifu ya New Zealand ya mwaka 1961

Makosa ya rushwa nchini New Zealand yamebainishwa katika Sheria ya Uhalifu ya mwaka 1961 ambayo imeanza kutumika rasmi tarehe 1 Januari 1962. Sehemu ya sita ya Sheria hiyo, kuanzia kifungu cha 99 mpaka kifungu cha 106, imeelezea vitendo mbali mbali vya uhalifu ambavyo vinaathiri usimamizi mzima wa haki na sheria. Katika sehemu hii, Sheria imejikita zaidi katika maeneo makuu mawili ambayo ni rushwa na ufisadi (bribery and corruption). Miongoni mwa maeneno yanayohusika na vitendo vya rushwa na ufisadi ambayo yamebainishwa na Sheria hii ni pamoja na:

#### (i) Rushwa katika mahkama

Katika eneo hili, Sheria ya Uhalifu ya 1961 nchini New Zealand imemtaja afisa yeyote wa mahkama akiwemo Jaji wa mahkama ya Wilaya na Jaji wa mahkama yoyote, au Hakimu wa jamii, au mtu mwengine yeyote mwenye kushikilia ofisi ya mahkama, au mtu yeyote ambae ni mjumbe wa mahkama iliyoidhinishwa na sheria kuchukua ushahidi kwa kiapo.

Kifungu cha 100(1) cha Sheria ya Uhalifu ya 1961 ya New Zealand kinaeleza kuwa afisa yeyote wa mahkama atawajibikia kwa adhabu ya kifungo kwa muda usiozidi miaka 14 ambaye anakubali au kupokea rushwa, au anakubali au anajitolea kupokea au kujaribu kupata, rushwa yoyote kwa ajili yake mwenyewe au mtu mwengine yeyote kuhusiana na kitendo chochote

kilichofanywa au kuachwa, au kufanywa au kuachwa, na yeye mwenyewe katika wadhifa wake wa kimahkama.

Vile vile Sheria ya Uhalifu nchini humo imemzungumzia afisa wa mahkama au Msajili wa mahkama au Msaidizi Msajili wa mahkama katika kifungu kidogo cha 2 cha kifungu cha 100 kuwa wakifanya makosa ya namna ya kukubali ama kupokea rushwa ambayo si katika namna iliyoelezwa katika kifungu kidogo cha (1) basi watawajibika kwa adhabu ya kifungo kwa muda usiozidi miaka saba.

**(ii) Kuwapa rushwa maafisa wa mahkama**

Sheria ya Uhalifu ya mwaka 1961 nchini New Zealand imelitanabahisha na kulitolea adhabu kali suala la baadhi ya watu kuwapa rushwa maafisa wa mahkama. Katika kutafuta haki na uadilifu wa kutoa maamuzi baadhi ya watu huwapa rushwa maafisa wa mahkama ili kuwashawishi kutoa maamuzi au kusaidia kutoa maamuzi ya mashauri kwa upande wao.

Kifungu cha 101(1) cha Sheria ya Uhalifu ya mwaka 1961 ya nchini New Zealand imeeleza kuwa kila mtu atawajibika kwa adhabu ya kifungo kwa muda usiozidi miaka saba ambaye anatoa rushwa au anakubali kutoa rushwa kwa mtu yeyote kwa lengo la kumshawishi afisa wa mahkama kutekeleza au kuacha kutekeleza wadhifa wake wa kimahkama.

Aidha kifungu kidogo cha 2 cha kifungu cha 101 cha Sheria hiyo kimetoa adhabu ya kifungo cha muda usiozidi miaka saba kwa mtu yeyote anaetoa

rushwa kwa Msajili au Msaidizi Msajili wa mahkama kwa lengo la kumshawishi asitekeleze wadhifa wake wa kiofisi.

### (iii) Rushwa na ufisadi kwa Mawaziri

Katika kutahadharisha ufanywaji wa vitendo vya rushwa katika ngazi za juu za utawala nchini New Zealand, Sheria ya Uhalifu ya mwaka 1961 ya nchi hiyo imetoa adhabu kali kwa Waziri au Mjumbe yeyote wa Baraza la Mawaziri atakaejiingiza au kujihusisha na kupokea rushwa. Sheria imeeleza kuwa Waziri au Mjumbe huyo wa Baraza la Mawaziri anaepokea, kukubali, au kujaribu kupokea rushwa kwa ajili yake au mtu mwengine yeyote atawajibika kwa adhabu ya kifungo kwa muda usiopungua miaka kumi na nne.[123]

Pia kifungu cha 102(2) cha Sheria hiyo kinafafanua kuwa mtu yeyote anaetoa au kukubali kutoa rushwa yoyote kwa mtu yeyote kwa lengo la kumshawishi Waziri au Mjumbe wa Baraza la Mawaziri kuhusiana na kitendo chochote kilicofanywa au kuachwa na yeye mwenyewe katika wadhifa wake kama ni Waziri au Mjumbe wa Baraza la Mawaziri atawajibika kwa adhabu ya kifungo kwa muda usiozidi miaka saba.

### (iv) Rushwa na ufisadi kwa Wajumbe wa Bunge

Sheia ya Uhalifu nchini New Zealand pia imetambua suala la rushwa katika chombo kikuu cha kutunga sheria mbali mbali za nchi hiyo. Sheria hiyo imeweka adhabu ya kifungo kwa muda usiozidi miaka saba kwa kila mjumbe wa bunge ambae anapokea, kukubali kupokea au kujaribu kupokea rushwa kwa ajili yake mwenyewe au mtu mwengine yeyote kuhusiana na kitendo

[123] Kifungu cha 102(1), Sheria ya Uhalifu ya 1961 ya New Zealand, uk. 76

kilichofanwya au kuachwa, au kilichopasa kufanywa au kuachwa, na yeye mwenyewe katika wadhifa wake kama ni Mjumbe wa Bunge.

New Zealand ni nchi ambayo imeshika nafasi ya kwanza duniani kwa mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa. Kutokana na jitihada za pamoja zilizofanywa na Serikali na wananchi wa nchi hiyo, New Zealand imefanikiwa kwa asilimia 88 kutokomeza vitendo viovu vya rushwa.

**3. MADASCAR**

**Sheria ya Kutangaza Mali ya Madascar ya 2016**

Serikali ya nchini Madagascaar imetunga sheria maalum ijulikanayo kama ni Sheria ya Kutangaza Mali ya 2016 ambayo lengo lake kuu ni kutambua mali zinazomilikiwa na viongozi wa umma ili kugundua na kuepusha vitendo vya rushwa na ufisadi miongoni mwa viongozi mbali mbali wa Taifa hilo. Sheria hii pia imejikita katika kuwajengea uwezo, kutoa miongozo imara na ya kimaadili kwa viongozi na watumishi wengine wa umma. Miongoni mwa madhumuni mengine ya Sheria hiyo ni pamoja na:

(i) kuoanisha masharti ya kutangaza mali;
(ii) kupanua tafsiri ya makosa ya rushwa; na
(iii) kuimarisha ulinzi kwa wachunguzi wa vitendo vya rushwa, wataalamu, majaji, mashahidi na watoa taarifa za vitendo hivyo vya rushwa.

**4. DENMARK**

**(a) Sera ya Kuzuia Rushwa ya Denmark ya 2018**

Katika kufanyakazi kwa mujibu wa maadili na maslahi ya Denmark katika mahusiano na nchi mbali mbali duniani, Serikali ya nchi hiyo kwa kushirikiana

na Wizara yake ya Mambo ya Nje imeweka Sera madhubuti ya kupambana na rushwa. Wafanyakazi wana mahusiano makubwa na taasisi za umma, mashirika, jumuiya zisizo za kiSerikali, raia wa kawaida, kampuni za kibiashara na washirika wengine duniani. Wizara ya Mambo ya Nje ya Denmark inaunga mkono kwa nguvu zote jitihada za kimataifa za mapambano dhidi ya rushwa na inawashauri washirika mbali mbali kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Wizara imedhamiria kudumisha viwango vya juu vya uadilifu na maadili ya kazi kwa wafanyakazi katika maeneo yote ya kazi, na pia usimamizi mzuri wa fedha za umma. Kwa ajili hiyo, Wizara inadumisha Sera ya Uvumilivu Sifuri (Policy of Zero Tolerance) kwa rushwa za aina zote. Ndani ya Sera hiyo kumebainishwa kanuni mbali mbali za maadili dhidi ya rushwa ambazo wafanyakazi wote, wakiwemo wafanyakazi wa Balozi za Denmark nje ya nchi hiyo na Wakala wa uvuvi Denmark, wataheshimuna kuendeleza misingi ya Kanuni za Maadili zilizoelezwa hapa chini:

**(b) Mgongano wa kimaslahi**

Tutajiepusha na mgongano wa aina yoyote, ambao ni halisi au unaowezekana kutokea, miongoni mwa maslahi yetu binafsi na maslahi ya Wizara ya Mambo ya Nje.

Mgongano wa kimaslahi huibuka katika hali ambayo mfanyakazi ana maslahi binafsi yenye uwezo wa kushawishi, au kuonekana kushawishi, utendaji wa majukumu usio na upendeleo na wenye malengo. Maslahi binafsi inajumuisha manufaa yoyote kwa mtu mwenyewe, familia, jamaa wa karibu, rafiki na mtu

au jumuiya ambayo mtu ana mahusiano ya kisiasa au kibiashara. Wakati ambapo mtu anakabiliwa na mgongano wa kimaslahi basi anatakiwa kumpa taarifa mkuu wake wa kazi.

### (c)Rushwa

Hatutatoa wala kupokea rushwa ya aina yoyote ile. Rushwa ni kitendo cha kutoa, kuahidi, kupokea, kuomba au kukubali kitu chenye thamai kwa lengo la kushawishi utendaji wa majukumu ya umma au ya kusheri. Rushwa ni kosa la jinai nchini Denmark.

### (d) Unyang'anyi

Hatutamshawishi kwa maslahi binafsi mtu yeyote au chombo chochote kwa kutumia nafasi zetu za kikazi au kwa kutumia nguvu au vitisho. Unyang'anyi hutokea wakati ambapo fedha au mali inaobwa kinyume na sheria au kupokelewa kwa njia za vitisho. Unyang;anyi unaweza kujumuisha vitisho vya kumdhuru mtu au mali zao, vitisho vya kuwashtaki kwa jinai/kitendo kisicho cha kisheria au vitisho vya kufuchua habari za aibu. Unyang'anyi ni kosa la jinai nchini Denmark.

### (e) Ulaghai

Hatutatumia udanganyifu, hila au uvunjaji wa uaminifu ili kupata faida isiyo ya haki au isiyo ya uaminifu. Ulaghai ni kutumia udanganyifu kwa madhumuni ya kupata faida (kiffedha au vyenginevyo), kuepuka wajibu au kusababisha hasara kwa wengine. Hii inahusisha kutokuwa mwaminifu kwa makusudi, hupotosha, kujiingiza katika vitendo vya udanganyifu, kufanya vitendo vya hila na uongo. Ulaghai ni kosa la jinai nchini Denmark.

### (f) Ubadhirifu

Hatutatumia vibaya au vyenginevyo kugeuza matumizi ya mali au fedha ambazo tupemewa dhamana. Ubadhirifu ni matumizi mabaya ya fedha au mali ambayo mtu amepewa dhamana kisheria kwa mujibu wa nafasi zao. Ubadhirifu pia ni kosa la jinai nchini Denmark.

### (g) Zawadi

Hatutatoa, kuomba au kupokea moja kwa moja au vyenginevyo zawadi ya aina yoyote ambayo inaweza kuathiri utendaji wa kazi zetu, utekelezaji wa majukumu yetu au hukumu zetu. Hii haijumuishi ukarimu wa kawaida au zawadi ndogo.

Katika mazingira wa rushwa, zawadi ni faida ya kifedha au faida nyengine, iliyotolewa, kupewa, kuombwa au kupokelewa kwa matarajio ya kurejeshewa faida. Kutoa zawadi na kufanyiana ukarimu ni kudhihirika kwa vitendo vya rushwa. Vitu hivi vinaweza kutumika kupelekea rushwa, au kukuwepo kwa rushwa. Zawadi inaweza kujumuisha fedha au mali zinazotolewa kama tunzo, michango ya kisiasa au hisani. Ukarimu unaweza kujumuisha mlo, hoteli, safari za ndege, burudani au michezo.

### (h) Upendeleo

Hatutafanya upendeleo kwa marafiki, familia au mtu mwengine yeyote mwenye uhusiano wa karibu katika kumuajiri, kumpa msaada, kumpa huduma za kibalozi au za hali nyengine. Upendeleo huoneshwa kwa jamaa au marafiki bila ya kujali sifa. Jamaa au marafiki wanahudumiwa kwa upendeleo

kwa kutokana na uhusiano wa karibu kuliko kufanya tathmini ya kimalengo au kitaalamu ya sifa zao au utaalamu wao.

**(i) Kutoa taarifa za rushwa**

Tutatoa taarifa za ushahidi au taarifa zenye kutia mashaka kwa uvunjaji wa Kanuni hizi za Maadili. Wafanyakazi wote wanalazimika kuzitambua Kanuni za Maadili za kupambana na rushwa na kuiheshimu misingi yake. Aidha wafanyakazi wanalazimika kutoa taarifa za ushahidi au taarifa zenye kutia mashaka kwa uvunjaji wa Kanuni za Maadili za rushwa kwa wakuu wao.

Vile vile Sera ya Kupambana na Rushwa ya 2018 nchini Denmark imesisitiza suala zima la ukweli na uwazi. Sera imefafanua kwa kueleza kuwa ukweli na uwazi wa hali ya juu ni muhimu katika mapambano dhidi ya rushwa, na taarifa zenye kuhusiana na sekta ya umma zinaweza kupatikanwa na jamii kwa mujibu wa Sheria ya Utawala wa Umma ya Denmark na Sheria ya Denmark ya Upatikanaji wa Majalada ya Utawala wa Umma.

## 5. TANZANIA

### (a) Muongozo wa Kuzuia Rushwa nchini Tanzania wa 2020

Muongozo wa kuzuia Rushwa katika ununuzi wa Umma uliozinduliwa rasmi Dodoma Novemba 24, 2020. Kwa mujibu wa utafiti uliofanywa wakati wa kuandaa muongozo huo; umebainisha kuwa maeneo yenye kiwango kikubwa cha viashiria vya rushwa ni pamoja na uandaaji wa zabuni, uandaaji wa orodha ya wazabuni, mfumo wa tathmini, maandalizi ya bajeti za zabuni na usimamizi wa mikataba.

Lengo la kuandaa muongozo huo lilikua ni kuziba mianya ya rushwa kwenye manunuzi na kusisitiza umuhimu wa kuzingatia taratibu za manunuzi ili ili kuhakikisha ubora na thamani ya manunuzi husika.

Aidha katika kuifanyia tathmini Tanzania, nchi za Bara la Afrika zimeitaja Tanzania kuwa ni miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri katika mapambano dhidi ya Rushwa. Hili limetokana na Mkutano wa 32 wa Umoja wa Nchi za Afrika uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia mnamo mwaka 2019.

Serikali ya Awamu ya Tano ya Tanzania imechukua jitahada maalumu za kupambana na Rushwa ikiwemo:

(a) Kufanya marekebisho kwa baadhi ya Sheria zinazohusu masuala ya Rushwa;
(b) Uanzishwaji wa Mahkama maalumu ya mafisadi;
(c) Mikakati ya udhibiti wa fedha za miradi ya wananchi; na
(d) Kuweka utaratibu mzuri wa kubaini walaji rushwa kwa kuishirikisha jamii ikiwemo kutunza siri za watoa taarifa.

### (b) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu 2017-2022

Mkakati huu ni moja ya hatua madhubuti ya kudhibiti rushwa iliyofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa utekelezaji wa awamu ya kwanza na ya pili licha ya kupatikanwa mafanikio makubwa lakini baadhi ya changamoto hazikuweza kutatuliwa hivyo, kupelekea kuanzishwakwa awamu ya tatu ya mkakati huu.

Mkakati wa awamu ya tatu unalenga kupunguza na kudhibiti rushwa katika sekta muhimu kama vile sekta ya manunuzi ya umma, ukusanyaji wa mapato, utoaji wa haki, maliasili na utalii, madini, nishati, mafuta na gesi, afya, elimu na ardhi. Madhumuni mahsusi ya Mkakati huu ni:

(a) Kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji wa utoaji wa huduma katika sekta ya umma na binafsi;
(b) Kuwa na ufanisi katika utekelezaji wa mikakati ya mapambo dhidi ya rushwa;
(c) Kuzijengea uwezo taasisi zinazosimamia mapambano dhidi ya rushwa; na
(d) Kuwa na uongozi madhubuti wa kisasa unaoshiriki kwa dhati katika mapambano dhidi ya rushwa.

**(c)Sheria ya Kudhibiti Uhujumu Uchumi ya 2019 Tanzania**

Moja ya jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni pamoja na kutunga sheria imara ijulikanayo kama ni Sheria ya Kudhibiti Uhujumu Uchumi ya 2019. Kutokana na kutambua umuhimu wa kuimarisha uchumi wa nchi kwa kupitia Sheria hii Serikali imefanikiwa kwa asilimia kubwa kuendeleza mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi nchini kwa lengo la kudhibiti miyanya ya vitendo hivyo katika maeneo mbali mbali ya kiuchumi.

Mfumo wa kisheria na kitaasisi wa kupambana na ufisadi nchini umekuwa ukiendelezwa tangu mwaka 1971, kwa kuanzishwa kwa Sheria ya Kuzuia Ufisadi.[124] Sheria hiyo ilirekebishwa mwaka wa 2002 na kurekebishwa tena

[124] Andreoni, A. 2017. ibid

mwaka wa 2007 hadi Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) inatia hatiani majaribio ya rushwa, unyang'anyi, hongo ya kimyakimya, utakatishaji fedha na hongo ya afisa wa kigeni.[125] Sheria nyengine za kukabiliana na rushwa nchini ni: Sheria ya Kanuni za Maadili ya Uongozi wa Umma 1995 (iliyorekebishwa mwaka 2001); Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001; Sheria ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2002; Sheria ya Vyama vya Siasa 2002; Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004; Sheria ya Kuzuia Utakatishaji Fedha Haramu ya mwaka 2006 (iliyorekebishwa mwaka 2012); Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008; Sheria ya Gharama za Uchaguzi 2010.[126]

**(d) Kuanzishwa kwa Divisheni maalum ya Mahkama Kuu ya kusikiliza mashauri ya rushwa na uhujumu uchumi**

Katika jitihada za mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi, Sheria hii imeanzisha divisheni maalum ya Mahkama Kuu ambayo lengo lake la msingi ni kusikiliza mashauri mbali mbali yanayohusiana na makosa ya rushwa na uhujumu uchumi. Kutokana na uzito wa makosa yanayohusiana na rushwa na uhujumu uchumi, mashauri yote yanayotokana na makosa hayo chini ya Sheria hii yanafunguliwa katika mahkama hii na hayatatakiwa kufunguliwa katika mahkama nyengine.

Katika kulibainisha hilo, kifungu cha 3(1) cha Sheria ya Kudhibiti Uhujumu Uchumi ya 2019 kinaeleza kuwa kutaanzishwa divisheni ya rushwa na

[125] GAN Integrity. 2019. Tanzania Corruption Report. https://www.ganintegrity.com/portal/countryprofiles/tanzania/

[126] Olan'g, L. and Msami, J. 2017. In Tanzania, Anti Corruption Efforts Seen As Paying Dividends, Need Citizen Engagement. http://afrobarometer.org/sites/default/files/publi cations/Dispatches/ab_r7_dispatchno178_corrupt ion_in_tanzania.pdf

uhujumu uchumi katika Mahkama Kuu yenye usajili mkuu na usajili mdogo kama ambavyo itaamuliwa na Jaji Mkuu ambapo mashauri ya yanayohusiana na rushwa na uhujumu uchumi yatafunguliwa.

*Jadueli Nam. 1 : Mlinganisho wa baadhi ya maeneo Afrika Mashariki*

| | **UGANDA** | **KENYA** | **TANZANIA** |
|---|---|---|---|
| Governance | Has an oversight board consisting of the inspector general (IG) as its chairperson, two deputy IGs, the secretary, the chairperson of the Public Service Commission, the Minister of Public Service and two members appointed by the president | Has a commission that oversees the performance of the secretariat staf | Has no oversight mechanism that is independent of the executive and parliament |
| Security of tenure | IG and two deputy IGs enjoy security of tenure after appointment for a four-year renewable term | Five part-time commissioners have security of tenure after appointment for a single term of five years. Staff have renewable contracts | Director general does not have specified security of tenure. Staff have renewable contracts |
| Ethics | | Code of ethics exists for commissioners and staff and is enforced | Code of ethics exists for staff and is enforced |
| Investigative and prosecutorial powers | Has investigative and prosecutorial powers | Has investigative but no prosecutorial powers | Has investigative but no prosecutorial powers. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Public feedback mechanism | Complainants are given a code through which they can track the complaint. They also receive feedback both orally and in writing at the closing of the complaint | After submitting a report, the public can create an anonymous post box from where to access feedback | There is no set feedback mechanism |
| Witness protection | | There is a witness protection law that is yet to be operationalised. | |

Effectiveness of Anti –Corruption Agencies in East Africa, African Regional Office (AfRo)Policy Brief 2016 https://www.opensocietyfoundations.org/uploads/6fa6e803-2780-417c-a533-36604d01a535/effectiveness-of-anticorruption-agencies-in-east-africa-kenya-20160913.pdf .

*Jadueli Nam. 2: Mlinganisho wa baadhi ya maeneo katika nchi mbalimbali*

| | **Whistleblowing and witness protection** | **Plea bargaining** | **Discriminatory among foreigners or between foreigners and locals** |
|---|---|---|---|
| KENYA | A 'whistleblower' is defined by Section 2 of the BA to mean a person who makes a report to the EACC or law enforcement agencies on acts of bribery or other forms of bribery.<br><br>A whistleblower or a witness in a complaint or a case of bribery is not to be intimidated or harassed on account of providing information to law enforcement institutions or giving testimony in a court of law.<br><br>10.2.3 Law enforcement agencies are required to put in place reasonable mechanisms for the protection of identities of informants and witnesses.<br>10.2.4 Kenya has the | Section 137 A of the Criminal Procedure Code (Chapter 75, Laws of Kenya), which applies to corruption and economic crimes, allows a prosecutor and an accused person or their legal representative to enter into a plea agreement. | The BA applies to any citizen, or resident in Kenya, a body incorporated under the laws of Kenya and which carries on business within or outside Kenya and any other body corporate that carries on business, or part of business in Kenya.<br>6.3.2 The only notable distinction between foreigners and locals is under section 15 of the BA, which provides for the extraterritorial application of the BA with regard to conduct by Kenyan citizens. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Witness Protection Act (Act No. 16 of 2006) that provides for the protection of witnesses in criminal cases and other proceedings. | | |
| Mauritius | **Bribery for procuring contracts** A person who gives or agrees to give or offers a gratification to a public official in consideration of that public official giving assistance or using influence in:<br>a. Promoting, executing, or procuring a contract with a public body for the performance of a work, the supply of a service, or the procurement of supplies;<br>b. The payment of the price provided for in a contract with a public body; and<br>c. Obtaining for that person or for any other person an advantage under a contract for work or procurement. | **Corruption of agent** An agent who, without the consent of his principal, solicits, accepts or obtains from any other person for himself or for any other person a gratification for doing or abstaining from doing an act in the execution of his functions or duties or in relation to his principal's affairs or business, or for having done or abstained from doing such act commits a criminal offence.<br>A person who gives or agrees to give or offer a gratification to an agent for doing or abstaining from doing an act in the execution of his functions or duties or in relation to his principal's affairs or business or for having done or abstained from doing such act commits a | Bribery by a public official to influence the decision of a public body. A public official who solicits or accepts a gratification for: a. Voting or abstaining from voting, or having voted or abstained from voting at a meeting of a public body of which he is a member, director or employee, in favour of or against any measure, resolution or question submitted to the public body; b. Performing or abstaining from performing, or aiding in procuring, expediting, delaying, hindering or preventing the performance of an act of a public body of |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | criminal offenc | which he is a member, director or employee; and c. Aiding in procuring or preventing, or having aided in procuring or preventing the passing of any vote or the granting of any contract or advantage in favour of any person |
| **NIGERIA** the Corrupt Practices and Other Related Offences Act, 2000 (the ICPC Act) was enacted and the Independent Corrupt Practices and Other Related Offences Commission (ICPC) of the Economic and Financial Crimes Commission (Establishment) Act, 2004 (EFCC Act). | **Discriminatory among foreigners or between foreigner**s and locals Any person who commits an offence is guilty of the offence and may be charged for committing it. 'Person' is defined to include a natural person, a juristic person or any body of persons corporate or incorporate (Section 2, ICPC Act). It is not material whether the person is a foreigner or a loca | Recently, the Federal Government of Nigeria initiated a whistleblowing programme with the aim of encouraging the disclosure of hidden proceeds of corrupt practices. The economic capital of the country, Lagos State, is also promoting the enactment of a whistleblower statute, the Disclosure of Impropriety Bill, 2016. (ALN Nigeria Partner, Gbolahan Elias, was the Chairman of the committee that drew up this Bill.)<br>Up until the enactment of the Freedom of Information Act, 2011, | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (the FOI Act) there was no specific law providing for access to public records and information. The FOI Act makes provision for the disclosure of information held by public authorities and institutions. The Act is innovative as it enables transparency in the activities of those in public offices | |
| **RWANDA**<br><br>The primary anti-corruption agency is the Office of the Ombudsman established by law No 25/08/2003 establishing the organisation and the functioning of the Office of the Ombudsman as modified and complemented by law No 17/2005 of 18/08/2005. | | **Discriminatory among foreigners or between** foreigners and locals The corruption laws apply to any citizen, or resident in Rwanda, a body incorporated under the laws of Rwanda and which carries on business within or outside Rwanda and any other body corporate that carries on business, or part of business in Rwanda. | |

# SURA YA SITA

## 6.0 MATOKEO YA UTAFITI

### 6.1 Njia zilizotumika katika Utafiti

Katika kufanyia mapitio sheria Nam.1 ya mwaka 2012, utafiti huu ulitumia njia kuu mbili ambazo ziliwezesha upatikanaji wa taarifa na kupelekea utafiti kukamilika. Moja ya njia hizo ni kwa kufanya utafiti wa ndani ambao ulipitia sera, mikataba ya kimataifa na sheria mbalimbali, makala, vitabu na maandiko muhimu yaliyoelezea masuala ya rushwa pamoja na uhujumu uchumi. Aidha, njia ya pili iliyotumika kufanya utafiti huu ni kwa kukusanya maoni kutoka kwa wadau moja kwa moja wanaohusika na usimamizi na udhibiti wa rushwa na uhujumu uchumi.

### 6.2 Upeo wa Utafiti

Utafiti huu unalenga kuangalia njia bora za kudhibiti na kuondosha kabisa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi kwa kuangalia njia zilizotumiwa na nchi mbalimbali ambazo zimeleta mafanikio katika nchi zao na kuweza kufanya vizuri katika kupambana na rushwa. Hivyo tafiti hii itaangalia hatua za kuchukuliwa ambazo zitaweza kusaidia Serikali katika mapambano haya. Aidha, mikakati yote na maazimio yote ya Kimataifa na Kikanda yanalenga kuzidisha mashirikiano baina ya nchi wanachama katika kupata ujuzi na kuendeleza vita dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi.

## 6.3 Ukomo wa Utafiti

Katika kufanya utafiti huu mapungufu yafuatayo yamejitokeza:

(a) Kutokuwepo juhudi za makusudi katika kila sekta ya Serikali katika kupambana na Rushwa, kwani sera nyingi zinazungumzia kuhusu madawa na ukimwi lakini hazizungumzii kabisa kuhusu janga kubwa la rushwa na uhujumu uchumi ambalo ndio linalopelekea kwa vitendo vya dawa za kulevya na ukimwi kuongezeka nchini.

(b) Kutokuwepo kwa uelewa mpana kwa watendaji pamoja na wananchi juu ya maana halisi ya rushwa na hatua za kuchukuliwa kwa waathirika wa rushwa na uhujumu uchumi.

(c) Kutokua na mfumo mzuri pamoja na ukosefu wa watalamu husika katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

## 6.4 Sampuli ya Utafiti

Taasisi mbalimbali kutoka Unguja na Pemba zimehusishwa katika utafiti huu. Miongoni mwa taasisi hizo ni pamoja na:

1. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar ZAECA,
2. Taasisi za Kisheria,
3. Wadau kutoka Mamlaka na Mashirika ya Serikali,
4. Jeshi la Polisi,
5. Wanasheria,
6. Wadau kutoka Taasisi za Serikali,
7. Wadau kutoka Taasisi za Ukaguzi,
8. Asasi za Kiraia,
9. Waandishi wa Habari,

Aidha makundi hayo yamejumuisha watendaji kutoka taasisi muhimu kama Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Idara ya Mahkama, Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango, Mamlaka za ukusanyaji wa kodi, na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Wawakilishi waliohudhuria kama inavyoonekana katika makundi ya mikutano katika Jadueli namba 3 na 4 kwa upande wa Unguja na Pemba. Jadueli namba 1, linaonesha makundi ya wataalamu na wadau kutoka taasisi za Serikali pamoja na asasi za kiraia waliohudhuria. Jumla ya Washiriki 116 walialikwa katika makundi yote.

***Jadueli Nam. 3: Idadi ya washiriki wote Unguja na Pemba***

| **Makundi** | **Waliohudhuria** | **Walioalikwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Taasisi za Kisheria | 8 | 10 | 80.0 |
| Taasisi ya ZAECA | 12 | 16 | 75.0 |
| Wadau kutoka Mamlaka na Mashirika ya Serikali | 12 | 15 | 80.0 |
| Jeshi la Polisi | 2 | 5 | 40.0 |
| Wanasheria | 9 | 9 | 100.0 |
| Wadau kutoka Taasisi za Serikali | 18 | 21 | 85.7 |
| Wadau kutoka Taasisi za Ukaguzi | 2 | 8 | 25.0 |
| Asasi za Kiraia | 24 | 28 | 85.7 |
| Waandishi wa Habari | 4 | 4 | 100.0 |
| **Jumla** | 91 | 116 | **78.45** |


*Jadueli Nam. 4 : Washiriki Unguja*

| **Makundi** | **Waliohudhuria** | **Walioalikwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Taasisi za Kisheria | 7 | 8 | 87.5 |
| Taasisi ya ZAECA | 11 | 13 | 84.6 |
| Wadau kutoka Mamlaka na Mashirika ya Serikali | 3 | 6 | 50.0 |
| Jeshi la Polisi | 1 | 4 | 25.0 |
| Wanasheria | 4 | 4 | 100.0 |
| Wadau kutoka Taasisi za Serikali | 1 | 4 | 25.0 |
| Wadau kutoka Taasisi za Ukaguzi | 0 | 6 | 0.0 |
| Asasi za Kiraia | 24 | 28 | 85.7 |
| Waandishi wa Habari | 2 | 2 | 100.0 |
| **Jumla** | **53** | **75** | **70.67** |

*Jadueli Nam. 5 : Washiriki Pemba*


| **Makundi** | **Waliohudhuria** | **Walioalikwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Taasisi za Kisheria | 1 | 2 | 50.0 |
| Taasisi ya ZAECA | 1 | 3 | 33.3 |
| Wadau kutoka Mamlaka na Mashirika ya Serikali | 9 | 9 | 100.0 |
| Jeshi la Polisi | 1 | 1 | 100.0 |
| Wanasheria | 5 | 5 | 100.0 |
| Wadau kutoka Taasisi za Serikali | 17 | 17 | 100.0 |
| Wadau kutoka Taasisi za Ukaguzi | 2 | 2 | 100.0 |
| Asasi za Kiraia | 0 | 0 | 0.0 |
| Waandishi wa Habari | 2 | 2 | 100.0 |
| **Jumla** | **38** | **41** | 92.7 |

***Chati Nam.1: Mchanganuo wa washiriki kwa Jinsia –Jumla***





Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, washiriki wengi (69.2%) walikuwa wanaume wakati (30.8%) walikuwa wanawake. Hii inathibitisha kwamba ushiriki wa wanaume ambao kama wahusika muhimu katika mapambano haya wameshirikishwa.


***Chati Nam.2: Mchanganuo wa washiriki kwa Jinsia –Unguja***



*Chati Nam.3: Mchanganuo wa washiriki kwa Jinsia –Pemba*





*Chati Nam. 4:* ***Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu - Zanzibar***





Matokeo yanaonesha kuwa washiriki wenye elimu ya sekondari ni (5.5%), elimu baada ya sekondari (17.6%) na waliokuwa na elimu ya juu kuanzia Digirii ya kwanza na kuendelea ni (76.9%). Lengo kubwa la kufanya uchambuzi huu, ni kwamba mbali ya watendaji wa Serikali waliotoa maoni,

uhalisia unaonesha kwamba wataalamu wenye uelewa wameshirikishwa kwa kiasi kikubwa katika utafiti huu.


*Chati Nam. 5:* ***Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu - Unguja***





*Chati Nam. 6:* ***Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu - Pemba***




*Chati Nam. 7: Idadi na asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri - Zanzibar*




*Chati Nam. 8: Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri - Unguja*



*Chati Nam. 9: Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Makundi ya Umri - Pemba*




## 6.5 Hadidu Rejea

Katika utafiti huu Hadidu Rejea zifuatazo zimezingatiwa:

(a) Kuangalia changamoto na kasoro ziliopo katika kuzuia, kusimamia na kupambana na vita dhidi ya Rushwa na Uhujumu Uchumi kwa upande wa Zanzibar.

(b) Kupitia sera na sheria zinazosimamia vita dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi.

(c) Kuangalia uwezo na kitaalamu uliopo ZAECA pamoja nguvu za kisheria alizopewa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi ili Mamlaka hii iweze kufanya kazi zake kama inavyotakiwa katika kuzuia na kupambana na rushwa na uhujumu uchumi.

(d) Kukusanya maoni ya wadau na kutoa mapendekezo ya utaratibu wa kutumika ili Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi iweze

kufanya kazi zake vizuri Zanzibar na tatizo la rushwa na uhujumu uchumi liweze kupungua nchini.

### 6.6 Matokeo ya utafiti

Matokeo ya utafiti na maoni ya wadau yamebainisha kuwepo kwa umuhimu wa kurekebisha baadhi ya vifungu vya Sheria Nam. 1 ya mwaka 2012 kwa lengo la kuongeza nguvu katika kupambana na rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar.

Tume ilikutana na wadau ambao taasisi zao zina uhusiano wa karibu katika utekelezaji wa majukumu yao na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Vile vile Tume ilikutana na wadau wengine ambao michango yao itasaidia katika kuboresha njia za kuzia rushwa na uhujumu uchumi Zanzibar. Kupitia maoni hayo pamoja na hadudi rejea mbalimbali yafuatayo yamebainika:

(a) Makosa yote ya Rushwa na Uhujumu Uchumi yanasikilizwa na Makhakama Kuu pekee jambo ambalo limesababisha uzoreteshaji wa kesi na kuipa Mahkama Kuu mzigo mkubwa uliokuwa hauna sababu kwani makosa yenye thamani ndogo ya rushwa husikilizwa na Mahkahama Kuu. Katika Sheria iliopo hakuna mgawanyo wa Mahkama nyengine zaidi ya Mahkama Kuu kwa kulingana na thamani na uzito wa kosa.

(b) Imebainika kuwa uwezo wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu ni mdogo hivyo ikilinganishwa na Mamlaka kama hizi kwa nchi nyengine. Kwa mfano Mamlaka kama hiyo kwa nchi ya Rwanda ikitoa mapendekezo kwa Taasisi za Serikali basi Taasisi hizo hulazimika kutekeleza mapendekezo hayo. Hivyo, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu

Uchumi Zanzibar inahitajika iongezewe uwezo wake ikiwemo uwezo wa kifedha, wataalamu, vitendea kazi pamoja na nguvu za kisheria. Vile vile suala la Mamlaka hii kutokuwa huru katika kufanya kazi zake lilibainika na ilionekana uzoefu wan chi nyengine Mamlaka kama hii zinajitegemea katika kufanya kazi zake.

(c) Katika utafiti huu imebainika kuwa kutokuwepo kwa kanuni au miongozo maalum ya maadili ambayo inawasimamia watendaji wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi katika ufanyaji wa kazi zao ili watumishi hao wasipate mwanya wa kufanya kazi nje ya mipaka yao na hakuna taasisi inayowasimiamia katika kuwaangalia utendaji wao kuwa ni wa haki na maadili. Vile vile, hakuna chombo maalum ambacho kitasikiliza malalamiko ya wananchi dhidi ya watendaji wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

(d) Ilibainikwa kuwa makosa yaliomo katika sheria hii ni kidogo na yenye mapungufu na hayalingani na adhabu zake. Vile vile, makosa na adhabu yaliyomo katika sheria hii hayalingani na adhabu zilizomo katika sheria nyengine kwa makossa kama hayo. Aidha, makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi hayakuwekwa wazi kulingana na aina za rushwa.

(e) Ilibainika kuwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar haina uwezo wa kukusanya taarifa wala haijaweka utaratibu mzuri wa kumlinda mtoaji taarifa juu ya matukio ya rushwa na uhujumu uchumi hivyo kupelekea Mamlaka hii kukosa taarifa muhimu ambazo zingeweza kufanyiwakazi na kusaidia kutambua walaji rushwa na uhujumu uchumi.

(f) Ilibainika kuwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar haikuchukua juhudi maalumu za kutoa elimu kwa wananchi juu

ya madhara ya rushwa na uhujumu uchumi nchini. Mamlaka hii haina mikakati wala utaratibu maalum wa kutoa elimu kwa watumishi wa umma na wa taasisi binafsi ukosefu huo wa elimu umepelekea wananchi kwa ujumla kukosa uwelewa mpana wa masuala ya rushwa na uhujumu uchumi.

(g) Ilibainika kuwa kuna changamoto kubwa ya kuchelewa uendeshaji wa kesi za rushwa na uhujumu uchumi, hii inatokana na sababu mbalimbali ikiwemo ya Mamlaka kukosa uwezo wa kuendesha kesi zao wenyewe na huchukua muda mpaka ipatikane ridhaa kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, mashahidi kutokufika pamoja na uwezo mdogo wa Mahkama katika kushugulikia kesi za Rushwa na Uhujumu Uchumi. Hakuna muda maalum ambao umewekwa kwa Mamlaka hii kumaliza upelelezi na kupeleka kesi Mahkamani hivyo, upelelezi unachukua muda mrefu.

(h) Imebainika kuwa ushirikiano baina ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi na taasisi nyengine ni mdogo hasa kwa taasisi ambazo kazi zao zinatakiwa zifanyike kwa mashirikiano ili ziweze kuleta mafanikio kama vile mashirikiano baina ya Mamlaka hii na Jeshi la Polisi katika kufanya upepelezi na kukamata watuhumiwa.

(i) Sheria hii haikutoa tafsiri kwa maneno muhimu kama vile neno Rushwa na Uhujumu Uchumi hayakuwekewa taafsiri zao maalum.

(j) Ili kuleta ufanisi katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi imeonekana ipo haja ya kuweka sawa muundo wa Mamlaka hiyo kwa kuwepo kwa kitengo maalum ambacho kitasimamia uendeshaji wa kesi za rushwa na uhujumu uchumi Mahkamani pamoja na kuwepo kwa kitengo maalum ambacho kitafanya kazi za upelelezi.

# SURA YA SABA

## 7.0 MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

### 7.1 Mapendekezo

Baada ya kufanya utafiti huu, kufanya tathmini, kuzingatia maoni ya wadau, kupitia rejea mbalimbali na uzoefu wan chi zilizoainishwa katika utafiit huu, Tume inapendekeza yafuatayo:

1. Kuimarisha mfumo mzima wa kisheria wa kupambana na rushwa, Kwa ujumla, Zanzibar ina mfumo wa kisheria unaohusishwa na utawala bora katika kupambana na rushwa. hata hivyo, utekelezaji hafifu wa sheria au adhabu isiyotosheleza kwa wanaofanya makosa ya rushwa na uhujumu uchumi, zinapelekea kuwepo mapungufu.Kwa hivyo kuna haja ya kushughulikia baadhi ya kasoro na mapungufu ya kisheria ambazo hufanya utekelezaji wa sheria kuwa mgumu kwa:
    (a) Kuweka mifumo mizuri ya upatikananji wa taarifa,
    (b) kulinda watoa taarifa na kutekeleza ulinzi wa mashahidi,
    (c) kuweka utaratibu wa mahakama za ufisadi ili kuharakisha kesi za rushwa na ufisadi.
    (d) Kuwapa nguvu na kuwatia moyo watoa taarifa kwa mujibu wa sheria ili waweze kutoa taarifa muhimu kwa mamlaka husika kwa ajili ya uchunguzi kwa madhumuni ya ushahidi na kutoa msaada wa kweli, kwa mamlaka zenye uwezo wa kushughulikia makosa hayo kisheria.

2. Mfumo wa kisheria wa kupambana na rushwa kwa Zanzibar unapaswa kufanyiwa marekebisho ili kuruhusu utaratibu wa kumaliza makosa (plea bargaining), kwa manufa ya Serikali na taifa kwa ujumla.

3. Kama chombo cha kupambana na rushwa, ZAECA yenyewe inaweza isiwe na rushwa, swali la msingi ni nani anafanya ukaguzi kuhusiana na mwenendo wa maafisa wa ZAECA kuhusu rushwa na kwa ZAECA kama taasisi. Kuhusiana na suala hili, ni muhimu kuwa na uwazi kama ambapo wananchi wanaweza kuripoti rushwa, kwa mfano rushwa inayohusisha maafisa waandamizi wa ZAECA.

4. Kuimarisha mamlaka na ushirikiano wa mashirika na Serikali na watendaji wasio wa serikali na mitandao ya kikanda. Mamlaka ya ZAECA kushughulikia kesi inahitaji kuongezwa na kesi za ubadhirifu chini ya sheria ya Sheria ya Adhabu, zisimamiwe na ZAECA kwa idhini na mamlaka ya DPP. Kwa mujibu wa ZAECA, hitaji la ridhaa ya DPP lina changamoto kiutendaji, kwa sababu DPP ana kazi kubwa inayohusisha wahalifu wote, hivyo kuna haja ya kuondoa changamoto hizo ikiwemo kupokelewa kwa kibali, DPP ateue maafisa maalum kushughulikia kesi za rushwa na uhujumu uchumi.

5. Kuimarisha utawala, uwezo wa wafanyakazi na miundombinu: ZAECA ni taasisi iliyoimarika na kutokana na taarifa zilizopo ni dhahiri kwamba uwezo wa taasisi hii umekuwa ukiongezeka. Idadi ya wafanyakazi wenye uwezo kisheria na kiwango uzoefu na utendaji wa taasisi unahitaji

kuimarishwa. Mbali ya hayo inapendekezwa ZAECA ichukue hatua zifuatazo:

(a) kuwekeza katika teknolojia ya kisasa ya kufuatilia miamala inayoshukiwa kuwa ya kifisadi na wahalifu ndani na nje ya mipaka ya Zanzibar.

(b) Kutafuta usaidizi zaidi kutoka kwa wataalam wa kupambana na rushwa kuhusu njia za kisasa za kupambana na rushwa, ikiwa ni pamoja na kuendesha shughuli za kupambana na rushwa na uhujumum uchumi.

(c) ZAECA iwe na maafisa wa sheria vijana na mawakili ambao wana uzoefu unaolingana na mawakili wengine katika kupamnana na watuhumiwa wa ufisadi.

(d) ZAECA inahitaji kuwa na operesheni za kupambana na rushwa, kwa mfano kutega mitego, na ufuatiliaji, dhidi ya idara zinazokabiliwa na rushwa na vituo vya utumishi wa umma

(e) kuwekeza katika uhamasishaji zaidi wa jamii kuhusu athari za rushwa katika utoaji wa huduma za kijamii na katika maendeleo ya jumla ya jamii.

6. ZAECA inapaswa kuanzisha na kutekeleza utaratibu wa utendaji wa maoni wenye uwezo wa kuwapa wananchi mara kwa mara (kila mwezi au robo mwaka) juu ya nini hutokea na taarifa zao kuhusu uchunguzi na kesi zilizoendeshwa. Hatua hizi zijumuishe:

(a) Kutoa udhibiti, usimamizi, matumizi na uwajibikaji wa fedha;

(b) Kutekeleza viwango vya maadili na uadilifu miongoni mwa maafisa wa umma;

(c) Kutoa masharti ya kuharamisha utakatishaji fedha haramu na kuweka majukumu ya kupambana na utakatishaji fedha haramu;

(d) Kutoa ulinzi, haki na ustawi wa waathiriwa wa makosa; na

(e) kutoa haki ya kupata taarifa za umma.

7. Kuimarisha mfumo mzima wa kisheria wa kupambana na rushwa kwa kuunda Bodi huru ambayo itakuwa jukumu muhimu la ushauri, udhibiti na uangalizi. Kwa hivyo inashauriwa sheria ipitishwe kutoa uangalizi wa chombo huru kitakachowakilisha maslahi ya umma na kuwajibika kwa kazi zao. Hii itasaidia kurekebisha udhaifu uliopo wa muundo, kuimarisha utendaji na kuhakikisha imani na uaminifu wa umma kuhusiana na mamlaka ya ZAECA.

8. Kuna ushirikiano mdogo kati ya ZAECA, FIU na jeshi la Polisi, DPP na taasisi nyengine. Ni muhimu kwa ZAECA kubaini uwepo katika kila eneo na kukidhi ipasavyo matarajio na mahitaji ya watu wengi. Teknolojia inapaswa kuruhusu ufikiaji wa umma zaidi. ZAECA lazima itafute njia ya kuimarisha matumizi ya tovuti yake, kwa kuripoti na kujifunza kuhusu rushwa na iwekeze katika ukuzaji wa programu kwa tovuti na simu ili kuchukua fursa ya kukua. Ofisi inatakiwa kuanzisha na kudumisha mfumo wa ushirikiano katika masuala ya rushwa na sekta binafsi, na taasisi za fedha, sekta amabzo bado hazijashirikishwa kikamilifu.

9. Kuimarisha uhuru na uwezo wa ZAECA: ni muhimu kuhakikisha kuwa kuna fedha za kutosha ya ZAECA ili kuiwezesha ZAECA kutekeleza majukumu yake iliyoidhinishwa bila kuchelewa. Kwa Bara miradi na

programu muhimu za kupambana na ufisadi, kama vile NACSAP kwa Bara, zimekuwa zikitegemea wafadhili. Utafiti unapendekeza ili, kwa kadri inavyowezekana, ZAECA ifadhiliwe kikamilifu kutoka kwenye rasilimali za ndani ili kuepusha matatizo yanayosababishwa na uhaba wa fedha.

10. Wajibu wa vyombo vya umma na vyombo binafsi kudhibiti na kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi: Wakati umefika sasa kwa vyombo vya umma na vyombo binafsi kubebeshwa jukumu kisheria la kudhibiti vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi katika maeneo yao. Katika kulifanikisha swala hili vyombo hivyo vinapaswa kushirikiana na Mamlaka kwa hali yoyote ile katika kudhibiti vitendo hivyo.

Kwa mnasaba huo, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi iweke kifungu kitachokitaka kila chombo cha umma na chombo binafsi kutekeleza kwa vitendo dhana nzima ya uwajibikaji katika sehemu za kazi na kufanya shughuli zake kwa uwazi, kutekeleza taratibu za kuzuia rushwa na uhujumu uchumi sambamba na kuwasilisha ripoti kwa mamlaka husika, kuhakikisha kwamba hakuna viashiria vyovyote vya rushwa ndani ya vyombo hivyo, kuhakikisha huduma sawa kwa wateja na utoaji wa huduma ndani ya wakati unaostahiki, kuwasilisha taarifa juu ya hatua wanazozichukua katika kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi pale zinapohitajiwa na chombo chenye mamlaka

11. Sheria kuwalinda watoa taarifa na mashahidi wa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi: Miongoni mwa watu muhimu ambao, moja kwa moja au vyenginevyo, huisaidia mahkama kusimamia sheria kwa kutoa maamuzi ya haki ni pamoja na watoa taarifa na mashahidi. Katika kuendesha kesi za rushwa na uhujumu uchumi na kutoa maamuzi ya kesi hizo, mahkama hutegemea ushahidi usio na shaka kutoka kwa wale walioshuhudia kufanyika kwa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi. Na kwa upande wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, katika kubaini baadhi ya vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi, husaidiwa na watoa taarifa wa kufanyika kwa vitendo hivyo. Kwa ujumla, makosa ya rushwa na uhujumu uchumi yametawaliwa na maslahi yenye thamani kubwa na hivyo, wanaotenda makosa hayo hujitolea kwa hali, mali na kwa kutumia silaha katika kuyalinda maslahi yao.

    Hivyo Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwa Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar iwalinde watoa taarifa na mashahidi wa makosa ya rushwa na uhujumu uchumi kwa kuhakikisha ulinzi usioyumba na mazingira bora, rafiki na salama kwa watu hao ili wajisikie huru katika kushirikiana na Mamlaka pamoja na Mahkama na kuondokwa na hofu juu ya madhara yoyote ambayo yangeweza kuwakumba kutoka kwa wale wote wanaotenda makosa ya rushwa na uhujumu uchumi.

## 7.2 Hitimisho

Hitimisho Kwa ujumla, Zanzibar imepata maendeleo makubwa katika kuanzisha taasisi ya kisheria na kitaasisi mfumo wa kupambana na rushwa na uhujumu uchumi. Kwa miaka mingi, ZAECA imebadilika na kujitahidi kuwa taasisi ya uwazi. Udhaifu wa ofisi hiyo upo kitaasisi na uchukuaji wa hatua madhubuti zenye uwezo wa kukabiliana na rushwa na uhujumu uchumi.

Rushwa na Uhujumu Uchumi ni vitendo ambavyo kwa kiasi kikubwa hudumaza jitihada za kuleta maendeleo kwa jamii nchini. Vitendo hivi hulifanya taifa pamoja na mihimili yake yote kukosa imani na kushindwa kufanya shughuli zake vile inavotakikana. Aidha uwepo wa vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi katika taasisi za umma na taasisi binafsi hupelekea kukosekana kwa haki, uadilifu na uwazi. Kutokana na ukubwa wa athari za rushwa na uhujumu uchumi katika jamii, serikali kwa kushirikiana na wananchi wanalazimika kupambana na vitendo hivi bila kuchoka wala kuoneana muhali.

Hata hivyo, katika kuleta mageuzi ndani ya jamii zetu, wataalam wa maswala ya kupambana na rushwa na uhujumu uchumi wanapaswa kutoa elimu ya kutosha kwa jamii kuhusiana na aina mbali mbali za makosa ya rushwa na uhujumu uchumi kwa mujibu wa Sheria, kuifahamisha jamii sababu za rushwa na athari zake katika nyanja za kiuchumi, kisiasa, kitaaluma, kisheria n.k ili kuleta uelewa wa kutosha juu ya maswala hayo na kuifanya jamii kujiona kwamba ni jukumu lao la pamoja kupambana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi nchini.

Kuondoka kwa tatizo hili kutategemea pia marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kubainsha makosa ya rushwa na uhujumu uchumi na kuweka adhabu kali kwa kila kosa, njia na taratibu sahihi za uchunguzi sambamba na kujikita zaidi katika kuweka mikakati bora ya udhibiti wa vitendo hivyo kama ambavyo imefafanuliwa katika ripoti hii.

## REJEA

### VITABU


A. Graycar, T. Prenzler. Understanding and preventing corruption. 2013; Palgrave Macmillan: Basingstoke, UK

Drake, P. W. (2009). *Between tyranny and anarchy: a history of democracy in Latin America, 1800–2006*. Stanford: Stanford University Press.

Tanzi, V., & Davoodi, H. (2000). Corruption, Public Investment, and Growth. IMF Working Paper No. 139. Washington: International Monetary Fund.

M. Johnston. Syndromes of corruption (2005) "Wealth, power, and democracy"; Cambridge University Press: New York


### MAKALA


Abed, G., & Davoodi, H. (2000) Corruption, Structural Reforms and Economic Performance in the Transition Economies. IMF Working Paper No. 132. Washington: International Monetary Fund.

Abraham Kipkoech Kemboi CRIMINAL JUSTICE SYSTEM RESPONSE TO THE PROBLEM OF CORRUPTION IN KENYA , ukurasa wa 233 https://www.unafei.or.jp/publications/pdf/RS_No92/No92_19PA_Kemboi.pdf

Andreoni, A. 2017. Anti-Corruption in Tanzania: A Political Settlements Analysis. SOAS, University of London. https://eprints.soas.ac.uk/24853/1/ACEWorkingPaper001-TZ-AntiCorruption171102_final%20revised.pdf

A Keith Thompson Does anti-corruption legislation work? This article was previously published in the International Trade and Business Law Review, 2013, vol. XVI, pp. 99-135, and is reprinted with the permission of the Editor-in-Chief of the Review, Professor Gabriel A Moens, and of the author., World Customs Journal, Volume 7, Number 2 43

Alexeev, M., Janeba, E., Osborne, S.: Taxation and evasion in the presence of extortion by organized crime. J. Comp. Econ. 32, 375–387 (2004)

Attila, J. 2008. “Corruption, Taxation and Economic Growth: Theory and Evidence.” CERDI-CNRS. Working paper

Bardhan, P. (1997). “Corruption and Development: A Review of Issues.” Journal of Economic Literature, 35(3), 1320-1346.

Cooney, J,P., Global Mining: The Three Priorities in a Politically Challenging World. In: Northwest Mining Association Annual International Convention ($4^{th}$-$8^{th}$ December, 1995), Spokane, Washington. Vancouver: Placer Dome Inc., 1995

Deniozos, Nikolaos and Vlados, Charis and Chatzinikolaou, Dimos, “Corruption as Form of Economic Crime and Government Effectiveness (May 6, 2018). Proceedings of the 3rd International Conference of Development and Economy I.CO.D.ECON, Kalamata, Greece, https://ssrn.com/abstract=3466321

Decision of the US Ninth Circuit Court of Appeals in Hilao v. Estate of Ferdinand Marcos et al., No. 03-16934, DC No. MDL-00840-MLR (28 December

DOIG, A., & Riley, S., Corruption and Anti-corruption Strategies: Issues and Cases Studies from Developing Countries in CHEEMA, G.S,. & J. Bovin (Eds), *Corruption and Intergrity Improvement Initiatives in Developing Countries*, 1998, ukurasa wa 45-62. Paris OECD

Dk. Edward G. Hoseah, The Southern African Forum Against Corruption inapatikana https://www.igg.go.ug/media/files/publications/SAFAC_Presentation_Bujumbura_by_Dr_Hoseah.pdf
Eurobarometer: Opinions on organized, cross-border crime and corruption. Special Eurobarometer 245/Wave 64.3-TNS Opinion and Social (2006)

Engelbert, Annika (2014) : The Role of Anti-Corruption Agencies in the Investigation and Prosecution of Procurement Related Corruption Cases, IEE Working Papers, No. 209, ISBN 978-3-927276-95-6Institute of Development Research and Development Policy (IEE), Ruhr University Bochum

Friedrich, C. (1972). Pathology of Politics, Violence, Betrayal, Corruption, Secrecy and Propaganda. New York: Harper & Row

G.E. Caiden. What really is public maladministration?. Public Administration Review. 51(6): 1991; 486–493.

Gyimah-Brempong, K. 2001. “Corruption, Economic Growth and Income Inequality in Africa.” http://link.springer.com/article/10.1007/s101010200 045

Gupta, S., Davoodi, H., and Alonso-Terme, R. 2002. "Does Corruption Affect Income Inequality and Poverty?" http://www.imf.org/external/pubs/ft/wp/wp9876.pdf

Gould D., "Administrative Corruption: Incidence, Causes and Remedial Strategies," in FARAZMAND, A. (ed.), Handbook of Comparative Development and Public Administration, New York: Marcel Dekker, 1991, p. 467.

Gray, Cheryl W., and Daniel Kaufmann, "Corruption and Development," Finance and Development, March 1998, p7-10.

GAN Integrity 2019 GAN Integrity. 2019. Tanzania Corruption Report. https://www.ganintegrity.com/portal/countryprofiles/tanzania/

GBN Ayittey 'Smart Aid for Africa', available at http://www.thisweekghana.com/ThisWeek/Commentary.AYITTEY.061505.htm

Hodgson, Geofrey M. & Shuxia Jiang, "The Economics of Corruption and the Corruption of Economics: An Institutionalist Perspective," Volume 41 Journal of Economic Issues, 2007, 1043 at 1044.

I. McAllister, J. Pietsch , A. Graycar . ANU poll: Perceptions of corruption and ethical conduct. 2012. Retrieved from http://politicsir.cass.anu.edu.au/polls-and-surveys/anupoll

Jorum Dui, "Corruption and Economic Crime", Transparency International, 2021, available at https://www.jstor.org/stable/resrep30836

J. Pope. Containing corruption in international transactions —The challenge of the 1990s. Commission on Global Governance. Issues in global governance: Papers written for the commission on global governance. 1995; Klewer Law International: London 67–90.

Karina Nazarova , Mariia Nezhyva , Volodymyr Hordopolov1 , and Viktoriia Mysiuk (2021) Anti-corruption audit as an imperative of effective environmental management 1 Kyiv National University of Trade and Economics, Financial Analysis And Audit Department, 19, Kyoto str., 02156 Kyiv, Ukraine, 2021 MATEC Web of Conferences 339, 010 (2021) ISTSML 2021 https://www.matec-conferences.org/articles/matecconf/pdf/2021/08/matecconf_istsml2021_01011.pdf

Kaufmann, D., Kraay, A. & Mastruzzi, M. (2003). Governance matters: governance indicators for 1996–2002. World Bank policy research department WP No. 3106.
Keith Blackburn, Kyriakos C. Neanidis1 · Maria Paola Rana1 (2017) A theory of organized crime, corruption and economic growth, 6 March 2017 Econ Theory Bull (2017) 5:227–245 DOI 10.1007/s40505-017-0116-5
https://link.springer.com/content/pdf/10.1007/s40505-017-0116-5.pdf

Kaunain Rahman Transparency International Anti-Corruption Helpdesk Answer Overview of corruption and anticorruption in Tanzania, 30 September 2019
https://knowledgehub.transparency.org/assets/uploads/helpdesk/Country-profile-Tanzania-2019_PR.pdf

Kilimwiko, L. 2019. In Tanzania, Local Structures in the Countryside Are Empowered for the Fight against Corruption. D+C Development and Cooperation. Lawrence Kilimwiko is a journalist, author and communication consultant. He lives in Dar es Salaam, Tanzania.

Marie Chêne, Overview of Corruption in Tanzania, U4 Helpdesk, Transparency International, mchene@transparency.org Reviewed by: Robin Hodess Ph.D., Transparency International, rhodess@transparency.org Date: 4 March 2009, U4 Expert Answers provide targeted and timely anti-corruption expert advice to U4 partner agency staff, https://www.u4.no/publications/overview-of-corruption-in-tanzania

McNeish, H. 2015. Rampant Corruption in Tanzania Keeps Fruits of the Many in Hands of the Few. The Guardian

Transparency International 2019 Transparency International. 2019b. Global Corruption Barometer Africa 2019: Citizens' Views and Experiences of Corruption. https://www.transparency.org/files/content/pages /2019_GCB_Africa.pdf

László Kőhalmi, Dr. Kitti Mezei (2015) The Forever Changed Economic Crime, Часопис Національного університету "Острозька академія". Серія "Право". – 2015. – №2(12)
https://li.oa.edu.ua/articles/2015/n2/15kllcec.pdf

Lambsdorff, Johann Graf (2002c). Making Corrupt Deals – Contracting in the Shadow of the Law, Journal of Economic Behavior and Organization. 48: 221–241

Layne, K. & Lee, J. (2001). "Developing Fully Functional E-Government: A Four Stage Model." Government Information Quarterly. 18, 122-1

Lea Kaspar & Andrew Puddephatt (2012) Benefits of transparency in public procurement for SMEs General lessons for Egypt By Global Partners and Associates, March 2012

Mauro, Paolo, 1997, "The Effects of Corruption on Growth, Investment, and Government Expenditure: A Cross-Country Analysis," in Elliott (1997).

Mushtaq H. Khan G-24 Discussion Paper Series Governance and Anti-Corruption Reforms in Developing Countries: Policies, Evidence and Ways Forward, No. 42, November 2006, UNITED NATIONS

Nawaz, F. 2010. "Exploring the Relationships between Corruption and Tax Revenue." http://www.u4.no/publications/exploring-therelationships-between-corruption-and-tax-revenue/

Olan'g, L. and Msami, J. 2017. In Tanzania, Anti Corruption Efforts Seen As Paying Dividends, Need Citizen Engagement. http://afrobarometer.org/sites/default/files/publi cations/Dispatches/ab_r7_dispatchno178_corrupt ion_in_tanzania.pdf

Peter Grabosky, "The Prevention and Control of Economic Crime", inapatikanwa NO.55-tobira (unafei.or.jp)

Prof. Haroub Othman, University Of Dar Es Salaam (Team Leader) Prof. Rwekaza Mukandala, University of Dar Es Salaam Mr. Robert Makaramba, Human Rights & Good Governance Commission Dr. Per Tidemand, United Nations Capital Development Fund April 2003:

Ruben Carranza Plunder and Pain: Should Transitional Justice Engage with Corruption and Economic Crimes? https://www.ictj.org/sites/default/files/IJTJ-Global-Justice-Corruption-2008-English.pdf , International Journal of Transitional Justice, Vol. 2, 2008, 310–330

Revolutionary Government of Zanzibar, Ministry of Finance and Economic Affairs, The World Bank, Public Expenditure Review FY03 (January 31, 2003)

Rob DeVries, 'Liberia Truth Commission on Hold Due to Lack of Funds,' Jurist, 28 November 2006.

Stefan Sumah, Corruption, Causes and Consequences, Open Access pear- reviewed chapter inapatikana https://www.intechopen.com/chapters/58969

Stiglitz, J. E. – On Liberty, the Right to Know and Public Disclosure: The Role of Transparency in Public Life – Oxford Amnesty Lecture, January, 1999.

Thierry Ménissier. Corruption, Virtue and Republic in Machiavelli's Work. South-East European Journal of Political Science, 2013, South-East European Journal of Political Science, vol. I/2004, October-November-December 2013, p. 51-60

United Nations Conventions against Transnational Organized Crime (UNTOC) http://www.unodc.org/documents/treaties/UNTOC/TOC%20Convention/TOCebook-e.pdf

UNODC,The Doha Declaraion, PROMOTING A CULTURE OF LAWFULNESS, pia inapatikanwa https://www.unodc.org/e4j/en/anti-corruption/module-5/key-issues/forms-and-manifestations-of-private-sector-corruption.html

Vito Tanzi, (1998) International Monetary Fund, Fiscal Affairs Department, Corruption Around the World: Causes, Consequences, Scope and Cures, working Paper https://www.imf.org/external/pubs/ft/wp/wp9863.pdf

Walter Odhiambo and Paul Kamau, (2003 OECD DEVELOPMENT CENTRE Working Paper No. 208 (Formerly Technical Paper No. 208) PUBLIC PROCUREMENT: LESSONS FROM KENYA, TANZANIA AND UGANDA Research programme on: The Integration of Developing Countries into the World Trading System, March 2003 DEV/DOC 2003)06 https://www.oecd.org/countries/uganda/2503452.pdf

Zanzibar Good Governance Strategic Plan Consultants' Report for UNDP Tanzania and Revolutionary Government of Zanzibar Final https://www.sheriasmz.go.tz/docs/RAccJxJkhY_Zanzibar_Good_Governance_Strategic_Plan_(ZGGSP)_Final_report.pdf

## TOVUTI

https://www.brookings.edu/wp-content/uploads/2016/07/chapter-one_-corruption-sh-9780815727910.pdf

https://theconversation.com/from-our-ancestors-to-modern-leaders-all-do-it-the-story-of-corruption-102164

www.researchgate.net

http://www.cipce.org.ar

https://www.istor.org/stable/resrep30836
https://www.sadc.int/files/7913/5292/8361/Protocol_Against_Corruption2001.pd
f
https://www.oas.org/en/sla/dil/inter_american_treaties_b-
58_against_corruption.asp
https://news.un.org/sw/story/2018/01/1002611
https://eaaaca.com/about-eaaaca
https://www.thecaacc.org/
https://www.thecaacc.org/about-us/
https://anticorruption.au.int/en/about

**SERA NA MIPANGO**

Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011

Sera ya Utawala Bora Zanzibar 2011

Sera ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2010,

Sera ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2014

Dira ya 2050

Mpango wa Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA III)

Programu ya Marekebisho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP)

Ilani ya CCM

Muongozo wa Kuzuia Rushwa nchini Tanzania wa 2020

Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Tatu 2017-2022

**SHERIA**

Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984

Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Nam. 1 ya mwaka 2012

Sheria ya Kupambana na Utakatishaji Fedha Haramu Nam. 10 ya mwaka 2009
Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Nam. 8 ya mwaka 2021
Sheria ya Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo Nam. 1 ya mwaka 2003
Sheria ya Adhabu ya 2018
Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016
Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya mwaka 2011
Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya mwaka 2015
Sheria ya Kudhibiti Uhujumu Uchumi ya 2019 Tanzan
Sheria ya Kupambana na Rushwa Rwanda Nam. 54 ya 2018
Sheria ya Uhalifu ya New Zealand ya mwaka 1961
Sheria ya Kutangaza Mali ya Madascar ya 2016
Sera ya Kuzuia Rushwa ya Denmark ya 2018
The Corrupt Practices and Other Related Offences Act, 2000 (the ICPC Act) Nigeria
The Economic and Financial Crimes Commission (Establishment) Act, 2004 (EFCC Act) Nigeria.

**KIMATAIFA**

Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Rushwa (UNCAC) wa mwaka 2004
Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (AUCPCC) mwaka 2007
Mkataba wa Nchi za Marekani (IACAC) wa mwaka 1997
Itifaki ya SADC dhidi ya rushwa mnamo Agosti, 2001
Shirikisho la Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa Afrika Mashariki. Shirikisho hili liliundwa tarehe 28 Septemba, 2007

Kituo cha kupambana na rushwa cha nchi za Jumuia ya Madola Afrika kiko Gaborone Botswana

Jukwaa la Kupambana na Rushwa kwa Nchi za Kusini mwa Afrika (The Southern Afrika Forum against Corruption (SAFAC)

Shirikisho huru la Kimataifa la Mamlaka mbalimbali za kupambana na Rushwa IAACA

Mkutano wa Kimataifa wa Kupambana na Rushwa

Mkataba wa OECD wa Kupambana na Ufisadi wa Maafisa wa Kigeni na wa Umma katika Miamala ya Biashara ya Kimataifa

Mkataba wa Umoja wa Mataifa dhidi ya Uhalifu wa Kupangwa wa Kimataifa

Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Rushwa http://www.unodc.org/pdf/crime/convention_corruption/signing/Convention-e.pdf

Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa unapatikana http://www.africa-union.org/official documents/Treaties-Conventions-Protocols/Convention on Combating Corruption.pdf

Zanzibar Strategy For Growth and Reduction Of Poverty (ZSGRP), Januari 2007